Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 13 Agosti, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE ( K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi kwa Mwaka 2011/2012 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. RACHEL MASHISHANGA ROBERT (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 360

### Miundombinu Mibovu na Uhaba wa Watumishi Hospitali ya Wilaya Tarime

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Tarime ni ya zamani sana na inakabiliwa na matatizo mengi ikiwa ni pamoja na miundombinu mibovu na uhaba wa watumishi:-

(a) Je, Serikali, inatoa kauli gani juu ya tatizo hilo?

(b) Je, Serikali, itajenga lini uzio wa Hospitali hiyo?

(c) Je, Serikali, itajenga lini majengo ya kutosha, likiwemo la utawala katika hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, zipo changamoto zinazoikabili Hospitali ya Wilaya ya Tarime, ambazo ni uhaba wa Watumishi wa Kada za Afya, uhaba wa majengo ya kutolea huduma na uchakavu wa majengo.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeajiri watumishi 25 wa Kada za Afya, ili kuondokana na upungufu uliopo. Aidha katika mwaka wa 2012/2013 Halmashauri imeomba Kibali cha Kuajiri jumla ya Wataalam 20 kwa ajili, ya Hopsitali hii ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010, Halmashauri ilitenga shilingi milioni 614 kwa ajili, ya ukarabati wa miundombinu ya Hospitali. Fedha zilizotolewa ni shilingi milioni 364, ambazo zimetumika kwa ajili, ya ukarabati wa jengo la Mfamasia wa Wilaya na Wodi ya Wazazi.

Aidha, katika mwaka 2011/2012 Halmashauri ilitenga shilingi milioni 350, kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya Hospitali hiyo. Hadi Juni, 2012, shilingi milioni 150 zilikuwa zimetolewa, ambazo

zimetumika katika kukarabati Wodi Namba 8 na ujenzi wa uzio. Katika Mwaka wa Fedha 2012/2013, jumla ya shilingi milioni 400 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati Wodi 6.

(b) Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2010/2011 Halmashauri ilipokea shilingi milioni 107.1 kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Hospitali hiyo kwa awamu ya kwanza. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa ukuta wa uzio huo.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 Halmashauri ilipokea shilingi milioni 50 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa uzio huo. Awamu ya pili ya ujenzi imeshaanza na itahusisha kuweka *grill,* kupiga plasta na kuweka umeme. Kazi hizi, zinatarajiwa kugharimu shilingi milioni 137.1 hadi zitakapokamilika.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na upungufu wa majengo katika Hospitali hiyo, Halmashauri katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 ilitenga jumla ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la Utawala. Fedha hizi hazikupatikana. Aidha, Halmashauri imetenga shilingi milioni 110 katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 kutokana na Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa, ili kutimiza azma ya kujenga jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali, itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali hiyo, kadiri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ambayo yanatia matumaini kidogo, naomba sasa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza inavyoonekana kwamba, fedha zinazotengwa, ili kuisaidia hii Hospitali iweze kukamilisha majengo yake, mara ya kwanza ilikuwa milioni 614, lakini zikitolewa milioni 364. Halafu vile vile, kuna milioni 100 zilitengwa, lakini hazikuweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, namwomba Naibu Waziri, aseme ni lini hizo hela zitapatikana?

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ni Sera ya Chama cha Mapinduzi (CCM), kuhakikisha ya kwamba, kila Kata inakuwa na Kituo cha Afya. Wilaya ya Tarime, ina Kata karibu 30, lakini ina Vituo vya Afya visivyofikia 5.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali, itahakikisha kwamba, Wilaya ya Tarime na Nchi ya Tanzania kwa ujumla kila Kata, inajenga Vituo vya Afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watu ambao tumepitishiwa hela hazikuweza kupatikana katika Halmashauri ni wengi sana, ni wengi tu. Hapa mnakumbuka *debate* iliyokuwapo hapa ni kwamba, hela hizi zilipangwa, lakini hela zilizokwenda hazikwenda kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, ukiacha zile hela ambazo tunazi-*allocate* kwa ajili ya miradi, yaani *The Local Government Capital Development Grant,* ambazo ukisha-*fix* na zimekwenda kwenye Halmashauri hatuziondoi, hizi hela nyingine tunazozizungumza hapa, kama hazikwenda, ndio mwaka umepita hivyo na habari imepita. Wote tunafahamu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitamwomba tu kwamba, katika mwaka huu tutakachofanya ni kung'ang'ana na Bajeti hii ambayo tumeipitisha hapa, kuhakikisha kwamba wanapata. Kwa sababu, kwa kweli, Mheshimiwa Mbunge, anachosema, Hospitali hii, mimi nimekwenda pale Tarime, ni chakavu imechakaa pale. Kwa hiyo, wanahitaji msaada. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba, tuna-*push* jambo hili, kwa maana ya Bajeti hii ambayo tumeipitisha hapa, ili tuhakikishe kwamba, tunakwenda.

Mheshimiwa Spika, la pili, analozungumza hapa ni jambo ambalo sisi wote kwa pamoja tumekubaliana. Kwamba, kila Kata, iwe na Kituo cha Afya na kila Kijiji, tuhakikishe kwamba, kinakuwa na Zahanati. Lakini tulisema mambo yafuatayo. Jitihada za kuanzisha hivyo vituo ni lazima zitokane na wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa ni kweli, anasema kuna Kata 30, lakini Vituo vya Afya vilivyoko pale ni vitano (5). Changamoto iliyoko kama Mbunge, sasa ni kwenda kuhamasisha wananchi wake. Sisi tunachofanya wakati mwingine, tunakuja kusaidia kwenye mabati pale, wakati wa ku-*finishing* pale, ndio tunakuja kusaidia pale.

Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Chacha, pamoja na kwamba, ninakubaliana nitashirikiana na yeye, nitamsaidia katika jambo hili, tutasaidiana na yeye kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu, *initiative* ya kuanzisha Vituo vya Afya, inafanana na zile Shule za Sekondari za Kata, ndivyo tulivyofanya. Kwa hiyo, jitihada inavyokuwa kubwa zaidi, ndivyo unavyoweza kupata msaada wa Kiserikali, kutoka katika Serikali.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, kazi ya kukarabati Hospitali za Wilaya ni ya Serikali. Na kwa kuwa, Serikali, hutenga fedha za ukarabati kwa awamu. Ziko Hospitali za Wilaya, ambazo zilitengewa fedha toka mwaka 2009, ikiwemo Hospitali ya Kiomboi.

Je, Hospitali zilizotengewa fedha toka mwaka huo mpaka leo na ukarabati haujakamilika, ni lini sasa zitatengewa fedha kukamilisha ukarabati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri

Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kazi ya kukarabati ni kazi ya wananchi na Serikali. *Project* zote zilizoko katika nchi hii tusingefika hapa tulipo kama isingekuwa ni jitihada za Serikali, pamoja na wananchi kwa ujumla. Ninakubaliana na yeye kwamba, kuna *input* ya Serikali, katika masuala haya ya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, sasa amezungumzia habari ya Hospitali ya Kiomboi, Halmashauri ya Wilaya hii, inatakiwa ihakikishe kwamba, imeingiza pia suala la ukarabati wa Hospitali hii anayozungumza Mheshimiwa Diana Chilolo. Siwezi kujua *status* yake kwa sasa hivi hapa, lakini nitakwenda kucheki, kujua kwamba, ni nini kilichosemwa katika hili eneo na nitamwasilishia kwa maandishi pale kumwambia kwamba, tutafanya nini. *(Makofi)*

**MHE. PAULINA P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Ni ukweli usiopingika kwamba, Halmashauri nyingi hazina Wataalamu wa Afya na majengo mengi hayapo. Lakini katika Ripoti ya *CAG,* ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, iliyoishia Juni 30, 2011, mwaka jana, jumla ya shilingi bilioni 5 milioni 849, hazikutumika za Mpango wa *MAM.*

Napenda kufahamu, kwanini hizo pesa hazikutumika wakati maeneo mengi hakuna majengo ya Zahanati na Wataalamu hawapo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paulina Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naelewa kwamba, Mheshimiwa Gekul, anatoka Babati kule na anasema kwamba, katika *CAG's Report* kuna bilioni 5 ambazo hazikutumika. Nataka nijue *status* yake, nitakwenda kutafuta. Je, zimeshatoka kutoka katika Wizara ya Fedha zikapita *TAMISEMI* zikaenda kule na kwamba, ziko kwenye akaunti na kwamba, hazijatumika?

Hicho ndicho nitakachokwenda kutafuta na nikikuta kwamba, hazijatumika kwa maana ya kwamba, hazikuingia katika akaunti sasa, ndio mimi nianze kutia sekeseke pale, kujua kwamba, ni nini kitakachofanyika pale. Kwa hiyo, hiyo uniachie tu.

**SPIKA:** Kwa hiyo unaomba muda. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema.

Na. 361

**Ujenzi wa Hospitali Teule ya Wilaya**

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA** aliuliza:-

Serikali, imeamua kujenga Hospitali Teule ya Wilaya, katika Mji wa Himo:-

(a) Je, utekelezaji wake umefikia hatua gani?

(b) Je, ni lini Hospitali hiyo itakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali, iliamua kujenga Hospitali ya Wilaya kwa kutenga fedha za ujenzi wa Hospitali ya Himo, katika Mwaka wa Fedha 2008/2009 kiasi cha shilingi milioni 175. Fedha hizi zilikusudiwa kutumika katika ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)* na kwa sasa, jengo hili limekamilika na linatumika.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 serikali, ilitenga kiasi cha shilingi milioni 300 ambapo shilingi milioni 200 zilitolewa kupitia Mpango wa Ruzuku za Serikali za Mitaa na shilingi milioni 100, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya uchunguzi *(X-Ray),* Utawala, Huduma ya Mama na Mtoto, vyoo na uzio kuzunguka eneo la Hospitali. Kazi hii alipewa Mkandarasi *Edcat Interanational Construction Ltd;* wakati wa utekelezaji ilidhihirika kwamba, Mkandarasi

huyu, alifanya kazi ambayo iko chini ya kiwango na hivyo Halmashauri, iliamua kuvunja Mkataba kwa kuzingatia Kanuni na makubaliano.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba, mradi huu ni muhimu Serikali, katika Mwaka wa Fedha 2012/2013 imetenga shilingi milioni 400 ambazo zitatumika kuanza ujenzi wa Hospitali hiyo. Zabuni zilitangazwa na kufunguliwa tarehe 18 Julai, 2012 na mchakato wa kumpata Mkandarasi mpya unaendelea. Ni kusudio la Serikali, kukamilisha ujenzi wa Hospitali hii haraka iwezekanavyo, ili kuwaondolea wananchi usumbufu katika eneo la Vunjo. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyomngeza. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri wa *TAMISEMI,* inavyoonekana, inavyoelekea sio mradi huo tu wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Himo, ambao umejengwa chini ya kiwango. *(Makofi)*

Kama Mkuu wa Mkoa, asingekuja pale, asingeshtukiza kwenye ziara yake, jambo hilo lisingeeleweka. Lakini ukiangalia miradi mingi ya Vunjo. Kwa mfano mfereji wa Kilemapofu, barabara ya Kilemapofu kwenda Kilema Hospitali, miradi yote hii imejengwa chini ya viwango. Yule Mkandarasi wa Mfereji, *CAG* alisema ashitakiwe na mpaka leo hakushtakiwa na hatua hazikuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, je, na huyu wa Hospitali ya Himo, ni kumsimamisha tu inatosha? Ni hatua gani madhubuti za Kiserikali, zinachukuliwa dhidi ya Mkandarasi huyo na hao Makandarasi wengine kule Vunjo?

Barabara, mifereji ya maji machafu, ambayo na yenyewe iko chini ya kiwango. Unachukua hatua gani wewe Naibu Waziri? Jibu. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Haya, Hotuba sio Hotuba. Haya, tuendelee, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii anayoisema, mimi nimecheka, ni kweli hiki anachosema, wakati tulipokwenda pale tukakuta kwamba, Mkandarasi ameingia pale na akafanya kazi chini ya kiwango. Cha kwanza sisi tulichofanya pale ni kupunguza *damage* pale. Huu mradi ulikuwa 336, tumekuta wamelipa milioni 101.

Mheshimiwa Mrema, nafahamu yeye ni Mwenyekiti wa *The Local Authorities Accounts Committee* ya Bunge, unafanyaje? Unasema endelea kulipa tu kwa sababu, tumeingia Mkataba pale? Tukasema *stop,* tukasimamisha pale. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mkoa kama alivyosema, akaagiza kwamba, tusimamishe pale. Ndivyo tunavyofanya katika miradi mingine yoyote iliyoko nchini, tukikuta iko chini ya kiwango, *we stop it.* Anayekwenda Mahakamani aende, atangulie, tutakutana naye hukohuko Mahakani. Hela zilizotumika pale ni milioni 101 na haya ndio tunataka tujue, nini hatima ya hela hizi zilizotumika pale?

Mheshimiwa Spika, milioni 101 zikichukuliwa hapa Mheshimiwa, ni lazima tuulize pia kwake. Kwa hiyo, tumemwambia pale Mkurugenzi Mtendaji, tunataka wathaminishe tujue, ile *material* iliyotumika pale na shughuli iliyofanyika pale je, ina *warrant?* Kuna kitu tunachokiita *value for money,* thamani halisi ya pesa iliyotumika pale kwa hiyo, iko hivyo. Sasa amesema na miradi mingine.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro, niliutembelea zamani sana. Mimi nasema hapa kwamba, tutaweka utaratibu tutakwenda tutatembelea miradi hii ambayo umeitaja ya mifereji na ile mingine. Kama tukikuta kwamba, kuna tatizo lolote hapa, niangalie macho yangu Mheshimiwa Spika, angalia midomo yangu, *I am telling you, we shall never leave any stone unturn,* tutakwenda kushughulikia. *(Makofi)*

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, imekuwa ni kama tabia sasa, kuhusu mikataba hii inayoingiwa kati ya upande mmoja wa fedha za Serikali, na ma-*Contractor* wa

Kandarasi mbalimbali. Na utaratibu wa Mkataba ni makubaliano kati ya pande mbili na ni lazima uwe wa Kisheria na unaotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, je, inatosha tu kusimamisha Mkandarasi, wakati kwenye Mkataba kuna vipengele vingine vya kuweza kudaiwa? Pamoja na fidia? Na thamani ya fedha, kwa mfano mradi huu wa 2008/2009. Je, thamani ya fedha kwa wakati huu ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nashauri mikataba hii iangaliwe kwa umakini, tuondokane na urasimu mkubwa wa Mahakamani na muda unaopotea na fedha za walipa kodi zinapotea.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, anakubaliana na ushauri huo?

**SPIKA:** Nimekumbuka kuwa kumbe Mheshimiwa Mbatia aliwahi kuwa Mbunge wa Vunjo. Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali hilo!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la nyongeza la mheshimiwa James Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia umetukumbusha kuwa Mheshimiwa James Mbatia

aliwahi kuwa Mbunge wa Vunjo, kwa hiyo ana uzoefu mkubwa.

Naelewa pia kwamba Mheshimiwa James Mbatia ana utaalamu mkubwa kwenye masuala tunayoyazungumzia hapa na mambo mengine ya zimamoto na ajali zinazotokea barabara ya Rombo na kadhalika, nafahamu hilo.

Kwanza unachofanya, hata kwako Njombe Mheshimiwa Spika tukifika pale tukikuta mambo yanafanyika ya ajabuajabu tunasimamisha kazi, kazi ya Serikali ni kuingilia kati na kuingilia kati maana yake unastopisha unasema simamisha, halafu baada ya hapo unawaambia wafanye nini. Tulichofanya ni hicho, tuliingilia kati kwa maana ya kusimamisha na baada ya hapo tunafanya *valuation* au utafiti, tunaangalia masuala ya kisheria yote na kadhalika na tukiona kama kuna tatizo basi ndipo hapo tunapoingilia kati.

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba ushauri wa Mheshimiwa James Mbatia tunaukubali na tutauzingatia.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata na litaulizwa na Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, kwa niaba yake Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda!

**MHE. CECILIA DANIEL PARESSO:** Mheshimiwa Spika, naitwa Cecilia Paresso.

**SPIKA:** Bwana, ninyi mnafanana sana, haya Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso. (*Kicheko*)

Na. 362

**Taratibu za Uendeshaji – Mji Mdogo wa Usar – River**

**MHE. CECILIA DANIOEL PARESSO (K.n.y. MHE. JOSHUA S. NASSARI)** aliuliza:-

Pamoja na Serikali kuipa hadhi Usa- River kuwa mji mdogo, bado kumekuwa na sintofahamu nyingi kwa wananchi.

(a) Je, ni kwa nini mpaka leo Serikali inachelewesha taratibu za uendeshaji wa mji huo?

(b) Je, ni mali kiasi gani zilizokuwa zinamilikiwa na wananchi wa kijiji cha Usa-River ambazo zimehamishiwa Mamlaka ya Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo Usa River iliundwa rasmi tarehe 1 januari, 2009 chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa namba 7 ya mwaka 1982

kifungu cha 13. Mamlaka hii iliundwa baada ya kuanzishwa kwa Halmashauri mpya ya Meru mwaka 2007.

Mamlaka hii imeundwa na vitongoji tisa ambavyo vyote vina wenyeviti wake. Mamlaka pia ina wajumbe saba wanaotokana na Baraza la Madiwani wa Arumeru, kati yao, wajumbe watatu ni Madiwani wa kuchaguliwa na wanne ni Madiwani wa Viti Maalum. Mjumbe mwingine wa Baraza la Mamlaka hii ni Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tangu kuundwa kwake, Mamlaka hii imekuwa ikiendesha shughuli zake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji wa Mamlaka za Miji midogo.

Kwa mfano, mamlaka hufanya vikao mara nne kwa mwaka na pale inapobidi, vikao maalum kama kile cha kujadili Bajeti au tukio muhimu hufanyika. Kwa mantiki hii, hakuna taratibu zozote za uendeshaji wa mamlaka ya mji mdogo wa Usa River ambazo zimecheleweshwa na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya kuanza rasmi kwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Usa River, mali zote za Umma zilizokuwa zinamilikiwa na Kijiji cha Usa River, sasa zinamilikiwa na Mamlaka ya Mji Mdogo. Mali hizo ni kama ifuatavyo. Shule za Sekondari za Muungano na Lake tatu, shule za Msingi za Leganga, Muungano na Manyata, Masoko ya Usa River na Mji Mwema, Kituo cha Afya cha Usa River na Mradi wa Maji wa Usa River.

**MHE. CECILIA DANIEL PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na kwamba mamlaka ya mji wa Usa River imeanzishwa toka mwaka 2009 lakini mpaka leo Afisa wa Mamlaka ya Mji mdogo na watumishi wengine hawajateuliwa au kuajiriwa.

Je, ni lini maafisa hao wataajiriwa au kuteuliwa?

Pili, kwa kuwa, kuna matatizo makubwa ya mgawanyo wa raslimali kati ya Halmashauri na Mamlaka ya Miji Midogo iliyo ndani ya Halmashauri hizo. Je, ni lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kuzitengea Bajeti mamlaka ya miji midogo nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Paresso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, labda tuiweke vizuri dhana hii kwani ina matatizo ya kueleweka kwake. Mamlaka ya Mji ni *an integral part* ya mamlaka inayoitwa Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Ukizungumza habari ya Bajeti, Bajeti ni sehemu ya Mamlaka kubwa inayozungumzwa.

Kwa hiyo, tuelewane vizuri na Mheshimiwa Nassari anasema kwamba hakuna hii Mamlaka, Mamlaka hii ipo na Mheshimiwa Cecilia Paresso anaulizia hilo swali. Watumishi wote wanaohusika wako

pale na wengine wanakaimu nafasi zilizopo pale, hilo labda ndiyo lingekuwa swali.

Lakini naomba niseme kwamba Mamlaka hii ipo na imekuwa inafanya kazi, tumezungumza na wahusika na mimi mwenyewe napita maeneo ya Arusha najua kwamba kuna Mamlaka ya Mjji Mdogo ya Usa River na inafahamika. Nia na shabaha ya kuanzisha mamlaka ile ni kama unavyokuwa na Kibaigwa unaona inavyo *grow* na kama hukuingilia kati kwa kuweka Mamlaka ya Mji Mdogo maana yake mtafika mahali patakuwa ni ma-*squatter* tupu.

Kwa hiyo, Mamlaka ya Mji Mdogo ni kipindi cha mpito kuelekea Mamlaka ya Mji kama Korogwe na kama vile tulivyopitisha Nzega. Kwa hiyo, mambo yote ya maamuzi makubwa yanaingia katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Meru kwa maneno mengine wale Madiwani watatu wanaoingia kule. Hundi ikitoka ya Mamlaka ya Mji Mdogo ni lazima iende mpaka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru. Kwa hiyo, unaweza ukaona na kufikiri kwamba haipo hii mamlaka na kazi yake kubwa ni mambo ya usafi wa barabara na vitu ambavyo vimezungumzwa.

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu wa kusema tunagawana na inaonekana watu hawajagawa, wanagawana nini? Ile mali yote ni mali ya Halmashauri ulichosema tu ni kwamba umekubali kwamba naitambua kwamba ni Mamlaka ya Mji Mdogo wa Usa River na mali zote zilizopo pale zinakuwa ni sehemu ya Halmashauri *unless* sikumwelewa vizuri

anachozungumza anasema kuna maeneo mengine ambayo yana matatizo, lakini mahali ambapo tunatakiwa kugawana ni pale ambapo unasema kwamba hii mamlaka imeunda Halmashauri mbili kubwa. Kwa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Hai na Halmashauri ya Wilaya ya Siha, pale mtagawana mali na mtagawana watumishi na kadhalika kwa taratibu zilizopo.

Napenda niseme kwamba mimi sijaelewa vizuri anachosema lakini akinieleza vizuri nitamsaidia kwenye jambo hili ili tuondokane na hili tatizo na tunaweza tukawasaidia Wabunge wakaielewa vizuri dhana hii. Hii Mamlaka ya Mji Mdogo ni mamlaka tu ambayo ina *take care* usije ukawa na ma-*squatter* na vitu vingine vya namna ile halafu pakavurugika hujui umeme utapita wapi, maji yatapita wapi, takataka zitatolewa wapi na barabara zitapita wapi. (*Makofi*)

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Mwaka 1990 Mji wa Sengerema ulitangazwa kwenye gazeti la Serikali kuwekewa Mamlaka ya Mji Mdogo. Ilipofika tarehe 7 Mei, 2010 kwenye gazeti la Serikali Namba 133 ulirudiwa tena kutangazwa na kufanyiwa marekebisho tarehe 14 Mei, 2010 kwenye *GN Number 190* na kugawa Kata za Mji wa Sengerema kwenye Kata nne ili kupata Mamlaka ya Mji Mdogo na mpaka sasa hakuna kinachoendelea na hakuna ukaguzi wowote ambao umefanyika.

**SPIKA:** Unazungumzia suala la wapi na sisi tunazungumzia mamlaka ya Usa River, hizo *quotation* zote zinatoka wapi?

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, swali lililoulizwa la msingi la Arumerulinafanana kabisa na matatizo ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Sengerema ambao mpaka sasa hakuna kinachoendelea licha ya kwamba ilitangazwa toka mwaka 1990. Nataka kujua kauli ya Serikali hii Mamlaka ya Mji wa Sengerema utaanza lini?

**SPIKA:** Hilo siyo swali linalofanana na la msingi, unauliza kuhusu mji mwingine wakati hapa uliulizwa Mji wa Usa River.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke atauliza swali hilo.

Na. 363

**Kuboresha Zao la Alizeti**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Zao la Alizeti linastahimili ukame na linaweza kuwaongezea kipato wakulima nchini:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeza zao hilo katika Mkoa wa Kigoma?

(b) Je, Serikali imejipangaje kuwawezesha wajasiriamali kujenga viwanda vya kukamua mafuta ya Alizeti?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na makampuni binafsi kuendeleza utafiti, uzalishaji na usindikaji wa mazao ya Alizeti, Ufuta, Karanga, Michikichi, Mbegu za Pamba na Soya. Kufuatia utekelezaji huo, uzalishaji wa Alizeti uliongezeka kutoka tani 348,877 mwaka 2009/2010 hadi tani 786,902 mwaka 2010/2011. Katika Mkoa wa Kigoma zaidi ya hekta 500 za Alizeti zinalimwa katika Wilaya ya Kasulu, Kibondo na Kakonko.

Aidha, Mkoa unazalisha jumla ya tani 908 ambapo kati hizo tani 750 zinazalishwa katika Wilaya ya Kasulu. Serikali inaendelea kuongeza uzalishaji wa mazao ya Mbegu za Mafuta katika Mikoa ya Singida, Tabora, Shinyanga, Iringa, Rukwa, Katavi na Kigoma yenyewe. Kwa mfano, mwaka 2011/2012 Wakala wa Mbegu yaani *Agricultural Seed Agency* imeanza kusambaza mbegu za Alizeti kwa wakulima Mkoani Kigoma pamoja na kuandaa mawakala watakaoisaidia *ASA* kusambaza mbegu hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa uzalishaji wa Mbegu za Mafuta unaongezeka, nchi yetu bado

inaagiza takribani 60% ya mafuta ya kula kutoka nje. Uendelezaji wa mazao ya Mbegu za Mafuta unaofanywa unalenga kuaongeza uwezo wa ndani wa kuzalisha bidhaa hiyo ambayo mahitaji yake yanakadiriwa kuwa na nakisi ya tani 200,000 ya mafuta ghafi ya kula kwa sababu hiyo, Serikali inapitia upya vivutio vya sekta ya viwanda vya ndani vinavyotumia Mbegu za Mafuta.

Aidha mfuko wa Pembejeo umepanua wigo wa mikopo inayotolewa kujumuisha mashine ndogo za kukamua mafuta ambazo zinaweza kununuliwa na wakulima ama mmojammoja au kupitia katika vikundi vya uzalishaji. Hii ni fursa nzuri kwa vikundi hususani vya akina Mama kujipatia mashine za kukamua Alizeti.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa, wakulima wa Mkoa wa Kigoma hususani Wilaya za Kakonko, Kibondo na Kasulu, wakala wa Taifa Mbegu yaani *Agricultural Seed Agency* imewahamasisha kwa kupeleka mbegu ya Alizeti.

Je, Serikali sasa itawasaidiaje wakulima wa Alizeti kupata mashine za kukamua Alizeti kupitia mfuko wa pembejeo?

Pili, ili kuvutia uzalishaji wa Alizeti na mbegu nyingine za mafuta na kulinda viwanda vya ndani. Je,

Serikali itakuwa tayari kuzuia uagizaji wa mafuta ghafi kutoka nje?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Genzabuke kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, Wakala wa Mbegu yaani *Agricultural Seed Agency* tayati ameshaanza utaratibu wa kusambaza mbegu katika Mkoa mzima wa Kigoma na vikundi vingi vimeshajiandaa, vipo vikundi Kalege, Bulimanyi, Kabondo, Ruhita, Kalela, Nyachenda na kadhalika ni takribani vikundi 30.

Sasa tutakachofanya sisi ni kuvihamasisha vikundi ili viweze kupata mikopo kutoka katika mfuko wa Pembajeo. Mimi niko tayari kabisa kuvisaidia vikundi hivi na utaratibu huo utaanzia hukohuko ndani ya Wilaya zinazolima Alizeti, lakini lengo ni kuvisaidia ili viweze kupata mashine hizi ndogondogo na zinapatikana na hata Mkoani Kigoma kwenye maduka tayari mashine hizi zimeshafika.

Kuhusu kuvutia uwekezaji wa ndani hili swali nakumbuka liliulizwa na Wabunge wengi wakati Waziri wa Fedha akihitimisha hotuba yake na alisema kwamba kwa kweli kimsingi Serikali inakubaliana na kuweka ushuru ili kupunguza uingizaji wa mafuta kutoka nje ili angalau kuhamasisha uzalishaji wa mafuta ya ndani.

Lakini kama nakumbuka vizuri maelezo ya Waziri wa Fedha yalisema kwamba utaratibu huo sasa kwa sababu tupo katika makubaliano na wenzetu katika Afrika Mashariki na tupo tayari na makubaliano ya itifaki ya Ushuru wa Forodha, basi atawasiliana na wenzake katika Afrika Mashariki maana si rahisi kufika tu unazuia au unaweka ushuru mkubwa kabla hamjapatana na wenzenu katika Jumuiya. Lakini kimsingi nakumbuka Waziri wa Fedha alisema, hili limepokelewa na linafanyiwa kazi katika utaratibu huo.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba utaratibu wa upatikanaji wa mbegu ukoje? Kwa sababu wakulima wa Kibondo, Kakondo kwako Mheshimiwa Waziri, hawajaufahamu utaratibu huu. Mbegu wanazipata wapi na kwa sababu udongo wa Kibondo na Kakonko na Kasulu wote ni sawa lakini bado zao hili halijalimwa kama unavyoeleza. Utaratibu wa mbegu ukoje?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Mkosamali, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwamba ni kweli zao hili linaonekana kama ni zao jipya katika mkoa mzima wa Kigoma japokuwa mikoa mingine imepiga hatua kubwa kama Singida na Dodoma. Sasa utaratibu wa upatikanaji wa Mbegu mimi mwenyewe nimeanza na ndiyo maana nimehamasisha ASA kwamba wapeleke mbegu na waanze kutafuta mawakala na nimesema katika majibu yangu, wameanza kwenda kutafuta

mawakala watakaosaidia kueneza upatikanaji wa mbegu. Kwa hiyo, mbegu inapatikana na inazalishwa katika vituo vyetu vya utafiti, kama kituo cha Ilonga kinazalisha mbegu nzuri kabisa ambayo ukikamua 60% unapata mafuta. Sasa tutatumia utaratibu huo huo kuwahamasisha wananchi na wakala wetu atakwenda katika Mkoa ataonyesha jinsi ya kuzipata mbegu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini Mheshimiwa Elizabeth Batenga atauliza swali na kwa niaba yake Mheshimiwa Charlesl Mwijage.

Na. 364

**Ujenzi wa Bomba la Mafuta Dar es Salaam - Mwanza**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE (K.n.y. MHE. ELIZABETH N. BATENGA):-**

(a) Je, ni lini bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza litajengwa?

(b) Je, bei ya mafuta haiwezi kuwa moja kwa nchi nzima kama ilivyo kwa Soda na Bia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Aprili, 2007 Serikali kupitia Wizara ya Mipango na Uwezeshaji ilisaini mikataba ya utekelezaji *(Implementation Agreements)* miradi ya kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta ghafi *(Refinery)* na bomba la kusafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma kwa maana ya miradi miwili yaani Dar es Salaam – Mwanza na *Kigoma Pipeline* na Kampuni ya *NOIT (Noor Oil Industry Technology)* kutoka nchini Marekani . Miradi husika haijatekelezwa mpaka sasa kutokana na *NOIT* kushindwa kutekeleza mambo ya msingi yaliyomo katika mikataba. Kwa sasa Wizara inaangalia upya mpango mzima wa utekelezaji wa mradi huo maana bado ni muhimu.

(b) Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1999 Serikali iliruhusu uanzishwaji wa mfumo wa soko huria katika biashara ya bidhaa za *petrol* hapa nchini. Tofauti na hapo awali biashara hii ilikuwa chini ya usimamizi wa mfumo hodhi ambao bidhaa za *petrol* zilikuwa zinaingizwa nchini na Serikali kupitia shirika la Maendeleo ya *petrol* (*TPDC)*, kwa kipindi chote kabla ya mwaka 1999.

Soko huru katika biashara ya mafuta ya *petrol* ni vigumu kutekeleza utaratibu wa bei za bidhaa hiyo kuwa sawa nchi nzima kutokana na kila kampuni kuwa na mfumo, utaratibu na gharama za usambazaji wa mafuta. Hata hivyo *EWURA* kama mdhibiti *(Regulator)*

inaendelea kupanga bei elekezi na pia bei kikomo kwa kuzingatia gharama za ziada kama usafiri na usafirishaji wa mafuta.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mojawapo ya tatizo la ujenzi wa bomba la mafuta kwenda Kigoma na Mwanza ni hali ya uzushi kuwapo watu *speculators*. Kwa kuwa, tumeshapata gesi asilia na mahitaji ya bomba la mafuta yanahitaji *light of way,* Serikali kama ilivyojijasiria kujenga bomba la kutoka Mtwara kwa nini isianze kutengeneza njia ya kutengeneza bomba la mafuta na gesi kwenda mikoa ya Magharibi ili bomba linapopita watu waweze ku-*tap gas* na waweze kupata mafuta?

Pili, kuhusu bei moja nchi nzima tatizo letu sisi mikoa ya pembezoni hasa Magharibi ni kuwa tunanunua mafuta bei ghali na mazao yetu yanauzwa bei rahisi na tunapata *inflation*. Kwa kuwa, *EWURA* ndiye mwenye *temperate* inayopanga bei na yeye ndiye anayetoa bei kikomo, kwa nini asiweke *transport equalisation factor* kwenye bei yake ili kusudi nchi nzima tupate unafuu na watu wa magharibi tuweze kupata bei inayofaa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu maswali ya nyongeza kama yalivyoulizwa na Mheshimiwa Charles Mwijage kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwijage kwa sehemu fulani yamekaa kama ushauri na sisi kama Wizara tutazingatia ushauri huo na tutahitaji zaidi ya hapo aliposhauri ili tuweze kuboresha sekta hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** *Okay!* Sikuona swali lingine kabla, hivyo tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Moses J. Machali.

Na. 365

**Madini katika Wilaya ya Kasulu**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

(a) Je, tafiti za madini zinaonesha wilaya ya Kasulu ina aina gani ya madini hadi sasa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha vijana kuchimba madini hayo ili kukabiliana na tatizo la ajira nchini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moses J. Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, kijiolojia Wilaya ya Kasulu iko katika ukanda wa miamba ya

*Bukoban Supergroup* yenye uwezekano wa kupatikana madini aina ya shaba, *nickel* na chuma *(iron).* Hata hivyo, Wilaya ya Kasulu inayo madini ya aina nyingine ya *opal, agate, limestone* na madini ya ujenzi kama vile mawe, mchanga na changarawe. Pamoja na taarifa za kijiolojia kuonesha kuwepo kwa madini mbalimbali hasa shaba, *nickel* na chuma bado utafiti wa kina wa madini hayo haujafanyika ili kujua kama kuna mashapo ya kutosha kuweza kuanzisha mgodi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa uchimbaji wa madini unafanywa na wachimbaji wadogo wenye leseni katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kasulu. Maeneo hayo ni pamoja na Nyakachacha, Migunga, Nyenge, na Nyakitonto ambao hujishughulisha na uchimbaji wa madini ya vito *(opal).* Wachimbaji wengine wako katika maeneo ya Makere ambayo huchimba mawe na kuzalisha chokaa *(limestone).* Vilevile, madini ya ujenzi huchimbwa katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Kasulu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa uchimbaji madini hususan uchimbaji mdogo umekuwa ni chanzo kikubwa cha ajira na mapato kwa wananchi walioko vijijini. Kutokana na hilo Serikali inahamasisha wananchi ikiwa ni pamoja na vijana wa Wilaya ya Kasulu kushiriki katika shughuli za uchimbaji na biashara ya madini ili waweze kujipatia kipato na hivyo kuondoa umaskini. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge

awahamasishe vijana katika Wilaya ya Kasulu kujiunga katika vikundi vya uchimbaji madini ambavyo ni rahisi kwa Serikali kuvisaidia kiutaalam na hata vifaa.

**MHE. MOSES J. MACHALI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(I) Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba, utafiti wa kina bado haujafanywa ili kujua kuna mashapo ya kutosha na hatimaye kuweza kuhamasisha watu kuweza kuanzisha migodi mikubwa. Ningependa kujua ni lini utafiti huo wa kina utafanywa ili kusudi wananchi wa Kasulu waweze kunufaika na masuala ya ajira kupitia sekta ya madini.

(II) Kumekuwa na *contradictions* kati ya Wizara mbili katika masuala yanayohusu uchimbaji wa madini. Wizara ya Nishati na Madini ambayo imekuwa ikijihusisha na masuala ya kutoa leseni kwa wachimbaji mbalimbali wakubwa na wadogo na hasa wachimbaji wadogo.

Lakini vile vile *contradiction* iliyojitokeza kati ya Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Nishati na Madini wanapotoa leseni Wizara ya Maliasili wanakuja kuwawekea pingamizi hao watu kuingia kwenye maeneo kwa madai kwamba wanaharibu mazingira.

Ningependa kujua hii *contradiction* Serikali itaweza kuiondoa lini kwa maslahi ya wachimbaji ambao wamepewa leseni lakini wanazuiwa kuchimba madini kwa kigezo kwamba wanaharibu mazingira.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Moses J. Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo.

(1) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini kupitia wakala wa jiolojia *(GST)* tumejipanga kuandaa utaratibu wa kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali ya wachimbaji wadogo ili kuweza kujua kiwango cha mashapo ambacho kipo katika maeneo ya wachimbaji wadogo na kama yanafaa kwa ajili ya uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Spika, jana tu nimerudi kutoka ziara ya Mkoa wa Kigoma na nimetembelea maeneo yote hayo ya Kasulu na mengine ya mkoa wa Kigoma. Nimejionea katika eneo hilo analozungumza kwa mfano pale Kasulu katika eneo la Makere kuna uchimbaji wa chokaa na wachimbaji wale wanachimba kwa njia za kienyeji lakini wanatoa chokaa bora kabisa ambayo unaweza ukafikiri imetokea kiwandani.

Nimeagiza wataalam wetu waweze kuandaa taratibu za kuangalia namna tunavyoweza kuwasaidia wachimbaji hawa kufanya tafiti katika maeneo yale ya uchimbaji wa chokaa na madini mengine ili kujua kiwango cha mashapo na kuweza kupima kina cha

uwekezaji ambacho kinahitajika katika miradi hiyo ya wachimbaji wadogo.

(ii) Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge anajaribu kuuliza! Naomba unikumbushe kidogo.

**SPIKA:** Anauliza juu ya *Contradictions* kati ya Wizara ya Nishati na Madini na ile ya Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusiana na utoaji wa leseni. Sisi Wizara ya Nishati na Madini tunapotoa leseni katika *section 95* ya masharti ya leseni inaeleza wazi yeyote anayepewa leseni ni lazima apate kibali cha kuingia kufanya shughuli, kama ni kwenye eneo la hifadhi na hata kama ni kwenye eneo la kijiji ambapo wananchi wanakuwa na maeneo yao.

Kwa mfano mashamba, mwenye leseni hawezi kwenda kuingia sehemu yoyote kwa lengo la kufanya shughuli ya uchimbaji bila kupata kibali cha mamlaka ama wananchi wa eneo husika.

Kwa hiyo, kwa *case* ya Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Nishati na Madini tunafahamu hapa nchini yako maeneo ya Hifadhi ya maliasili ya nchi, na maeneo haya mengine yameonekana kuwa na madini na watu wetu wengi wamekuwa wakivamia kimya kimya kwenda kuanza shughuli za uchimbaji. Lakini kwenye eneo la Makere ambako kuna uchimbaji wa chokaa ni eneo la Maliasili la Hifadhi.

Nimewaagiza wataalam wetu wasaidie wachimbaji wadogo ili waweze kupata kibali kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, ambayo ndiye mmiliki wa eneo lile ili waweze kutoa ruhusa ili wachimbaji wadogo wadogo waweze kuchimba.

Kwa hiyo, suala la mwingiliano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Nishati na Madini linaunganishwa na *section 95* ya masharti ya leseni ambayo siyo tu kwa Maliasili, bali hata kwa wananchi wengine wo wote. Shughuli za uchimbaji lazima upate kibali ama ridhaa ya wahusika wa eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa majibu yamekuwa marefu kwa hiyo tunaendelea na Wizara inayofuata, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Michael L. Laizer anauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Mary Chatanda.

Na. 366

**Kupeleka Askari Katika Kituo cha Polisi cha Kata**

**MHE. MARY P. CHATANDA (K.n.y. MHE. MICHAEL L. LAIZER)** aliuliza:-

Kituo cha Polisi Kata ya Gilailumbwa kimejengwa na kukamilika mwaka 2007 lakini mpaka sasa bado hakijafunguliwa:-

Je, Serikali itapeleka lini askari kwenye kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael L. Lazier, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba jengo analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge ambalo lilijengwa kwa nguvu za wananchi lilikamilika mwaka 2007. Hata hivyo, yapo mapungufu ambayo yanastahili kufanyiwa kazi kabla ya kupeleka askari kwenye kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapungufu yaliyopo napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inathamini sana michango ya wananchi na Waheshimiwa Wabunge katika ujenzi wa vituo vya polisi. Naomba nimhakikishie pia Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tunalifuatilia kwa ukaribu na wahusika wote ili kituo hiki kianze kutumika.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa wananchi wamejenga jengo hili kwa asilimia kubwa, kwanini sasa Serikali isiweze kuwasaidia kukamilisha jengo hili ili kusudi liweze kuanza kutumika kutoa huduma kwa wananchi wa maeneo hayo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mary Chatanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakabiliwa na majengo ya namna hii mengi sana nchi nzima. Pamoja na hilo tunafanya jitihada kuona kwamba pamoja na majengo mengine lakini na jengo hili tutalikamilisha ili litumike.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la uhaba wa askari ni kubwa sana nchini, jambo ambalo linafanya Serikali ishindwe kuwasambaza katika majengo hayo ambayo yanaulizwa katika swali la msingi, na kwa kuwa kuna tatizo kubwa sana la ajira katika nchi yetu.

Je, ni kwanini Serikali isifanye mpango sasa wa kuwaajiri vijana ambao hawana kazi ili waweze kuchukua nafasi hizo katika hayo majengo ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi yakiwepo pia majengo ambayo yako katika jimbo la Ukonga na ambayo nimekuwa nayazungumzia kwa muda mrefu sana hususan katika maeneo ya Mvuti na Chanika? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Yaani hiyo ni kwa ajili ya askari tu, loh! Haya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Eugen Mwaiposa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa viwango vya kimataifa Tanzania bado tuna *ratio* ya ajabu ambayo haitoshelezi kwa askari kama wanavyotakiwa kulinda wananchi wetu. Tatizo hili Serikali inalitambua na pia inatambua ukosefu wa ajira wa vijana. Hata hivyo, pamoja na jitihada za kukamilisha taratibu za kuongeza askari bado hilo linategemea Bajeti tuliyonayo pamoja na vitendeakazi vingine ambavyo vitahitajika.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuajiri kwa mujibu wa Bajeti inavyoruhusu pamoja na mahitaji. Hilo litaendelea na hatimaye tunaweza kupunguza pengo kati ya mahitaji na waajiriwa wa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Na. 367

**Upatikanaji wa Vifaa Bora vya Zimamoto Jijini Dar es Salaam**

**MHE. HAMAD ALI HAMAD (K.n.y. MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA)** aliuliza:-

Ujenzi wa majengo ya ghorofa zinazofikia ishirini (20) unazidi kuongezeka na kadiri mji unavyokua na huduma zaidi zinahitajika; zaidi ya hapo inasemekana kuwa Shirika la *NSSF* nalo linampango wa kujenga jengo litakalokuwa na ghorofa zaidi ya 40:-

Je, Serikali imejipanga vipi kupata magari pamoja na vifaa bora zaidi vya zimamoto vitakavyoweza kutoa huduma hiyo kwenye majengo marefu kama hayo pale majanga ya moto yanapotokea?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kupanuka kwa mji kunaambatana na ujenzi wa majengo marefu yanayopelekea uhitaji wa huduma bora za Zimamoto na Uokoaji. Kwa kuliona hilo Wizara yangu kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inatarajia kutenga fedha kwenye b Bajeti ya mwaka wa fedha ujao wa 2013/2014 kwa ajili ya kununulia gari la kuzimia moto linalofikia majengo yenye urefu wa hadi ghorofa 37 ambao ndio urefu wa mwisho wa gari la kuzimia moto duniani kote.

Aidha, kwa mujibu wa Sheria majengo yote marefu yanatakiwa kuwa na mfumo wa kugundua na kumwaga maji yenyewe mara moto unapowaka *(fire Sprinkler System)* ili kuweza kukabiliana na moto au dalili za moto zinapojitokeza.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa kibali cha kuanza ujenzi hutolewa baada ya usanifu wa majengo kukamilika.

Je, idara ya Zimamoto inashirikishwaje ili kuona kwamba michoro ya majengo hayo inayo maeneo ya kuwezesha kutolewa huduma ya dharura wakati wa moto?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba ni sheria majengo marefu yanatakiwa kuwa na mfumo wa kugundua na kumwagilia maji yenyewe wakati wa moto?

Je, kwa haya majengo marefu yanayojengwa sasa yanao mfumo huu? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, kama ifuatavyo:-

Ni sawa na kweli kwamba Idara ya Zimamoto na Uokoaji inashiriki katika kuangalia michoro na kwa sababu hiyo inapoona kuna upungufu inaweza kupeleka marekebisho.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba majengo ambayo yanajengwa sasa kwa sababu idara inashiriki katika michoro ni dhahiri kwamba michoro

ambayo inapelekwa na kupita Idara ya Zimamoto inakuwa tayari imeishajulikana kwamba itakuwa na miundombinu inayotakiwa. Pamoja na hilo Idara ya Zimamoto na Uokoaji hufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kuhakikisha kwamba, mapungufu yote yanajadiliwa na sheria zinafuatwa ili kuhakikisha kwamba hata moto utakapotokea madhara yake yanakuwa madogo.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kumwuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mbali na huu utaalam unaozungumzwa wa majengo yajizime yenyewe lakini kuna tatizo kubwa ambapo baadhi ya majengo yanayojengwa hasa Jijini Dar es Salaam mengine hata kuyafikia pale unapotokea moto inakuwa tatizo kwa sababu hakuna barabara za haraka za kuyafikia.

Je, hili nalo Serikali inafanyaje katika kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Naomba kujibu swali la la Mheshimiwa Khalifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba moja kati ya changamoto kubwa ambazo Idara ya Zimamoto na Uokoaji inapambana nazo ni miundombinu au uwezekano wa kufikia kwenye maeneo ya majanga kutokana na utaratibu wa ujenzi

hasa katika Jiji la Dar es Salaam. Hili ni moja kati ya matatizo ambayo yanafanya mara nyingi Zimamoto wanapigwa mawe kwa kufikiri kwamba wamechelewa makusudi, lakini wanakuwa wanafanya *maneuver* ili waweze kufika huko.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili tunalifahamu na kwa sasa kitu ambacho tunafanya ni kuhakikisha maeneo mapya ya ujenzi yanazingatia mahitaji ya Zimamoto au moto unapotokea tuweze kufika kwenye maeneo husika. Aidha, katika maeneo ambayo tayari yameishajengwa tunajaribu kutazama utaratibu wa vipi tunaweza kuongeza *water hydrants* au hata kuzifufua ambazo zilikuwepo na zimeharibika kwa sababu mbalimbali. *(Makofi)*

Na. 368

**Sekondari ya Ndanda kuwa ya Wavulana tu**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA (K.n.y. MHE. MARIAM R. KASEMBE)** aliuliza:-

Sekondari ya Ndanda imekuwa shule ya wasichana na wavulana kwa Kidato cha Kwanza hadi cha Sita kwa miaka mingi sasa, lakini cha kushangaza ni kuwa shule hiyo sasa imefanywa ya Kidato cha Tano na Sita kwa wavulana tu:-

(a) Kwanini Serikali imeibadili shule hiyo kuwa ya Kidato cha Tano na cha Sita na kwa wavulana tu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kitendo hicho kimewanyima fursa vijana wa Mtwara na Lindi hasa wa kike wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne kupata masomo yao kwenye mazingira hayo bora na huduma zote za elimu?

(c) Je, kwanini Serikali isione umuhimu wa kutazama upya maamuzi hayo na kurudisha shule hiyo kuwa ya wavulana na wasichana kwa kidato cha Kwanza hadi cha Sita kama ilivyokuwa awali?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mbunge wa Masasi lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilibadili shule ya Sekondari ya Ndanda kuwa shule ya wavulana kwa Kidato cha Tano na Sita ikiwa ni mojawapo ya jitihada za Serikali za kuongeza nafasi kwa ajili ya wanafunzi wahitimu wa Kidato cha Nne wanaotokana na ongezeko la shule za Sekondari za Kutwa za Kidato cha Kwanza hadi cha Nne *(O – Level)* ambalo lilipelekea uwepo wa wanafunzi wengi waliofaulu kuingia Kidato cha Tano.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa MMES Awamu ya Kwanza, moja ya malengo yake ilikuwa ni kuanzishwa kwa shule za Sekondari za Kata na shule mbili (2) za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita *(A-Level)* katika kila Kanda. Moja kati ya shule hizo iwe ya wasichana na nyingine ya wavulana. Katika Kanda ya Kusini ambayo inajumuisha mikoa ya Lindi na Mtwara shule mbili ziliteuliwa kuwa za Kidato cha Tano na Sita ambazo ni Ndanda Sekondari kwa ajili ya wavulana na *Masasi Girls* kwa ajili ya wasichana.

Mheshimiwa Spika, shule za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita *(A- Level)* ni shule za Kitaifa ambazo zinapokea vijana wahitimu wa Kidato cha Nne waliofaulu kutoka mkoa wowote wa Tanzania. Kwa mantiki hii shule za Sekondari za Ndanda na Masasi ni shule za Serikali kwa ajili ya vijana wote wa Kitanzania yaani ni shule za Kitaifa kama zilivyo shule nyingine za Sekondari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kubadili shule ya Sekondari ya Ndanda kuwa shule ya wavulana pekee haijawanyima fursa vijana wa Mtwara hasa wasichana wa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne kwa sababu katika shule zilizopo bado kuna upungufu wa wanafunzi.

Mfano shule za Kiengei, Kilimarondo na Namakwiya hazijapata wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka huu, 2012. *(Makofi)*

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri hivi hakuna Shule ya Kidato cha Kwanza hadi cha Sita nchini cha Wasichana na Wavulana ni Ndanda tu peke yake ndio maana mliona msitishe hiyo huduma ya Wasichana?

Swali la pili, kwa kuwa shule hii ilikuwa ni ya Bweni kuwaondoa Wasichana pale ni kuwanyima fursa yao ya msingi na ni ubaguzi wa jinsia. Je, hamwoni kwamba hiyo ilikuwa ni kudididmiza elimu kwa Wasichana Wilaya Masasi na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, shule za namna hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Dustan Mkapa zipo, lakini ninachosemea hapa ni kwa Kanda ya Kusini tu, Kanda ya Mikoa ya Mtwara na Lindi ziliteuliwa shule hizo za Masasi Girl's na Ndanda ili ziwe za shule za "*A" Level* kwa ajili ya Wasichana pekee na Wavulana pekee. Lakini hata hivyo kule Lindi na Mtwara bado kuna shule inaitwa *Mtwara Girl's* bado vilevile inachukua Wasichana.

Lakini kama nilivyosema kwenye swali langu la msngi kwamba sasa hivi tuko kuboresha elimu, tunataka *quality education*, suala sio kujenga tu shule hizi na ambapo tayari nimesema kwamba hata huko Mtwara tayari kuna hizi sekondari tatu mwaka huu hazina wanafunzi. Kwa hiyo tunataka *quality education* kwamba tuanze kuboresha sasa elimu, tuanze kuongelea masuala ya vitabu, masuala ya Walimu na mambo mengine na madawati.

Lakini tumeshajenga hizi shule na ilani ya Chama cha Mapinduzi tayari ni kama hapo imetekelezeka vizuri sana. Sasa hivi tuanze kuongelea masuala ya Walimu, lakini shule tayari tumeshajenga na tayari Shule za Wasichana kule Mtwara na Lindi zipo kama nilivyosema.

Na. 369

**Shirika la NDC Kupewa Nguvu ya Kuzalisha Umeme**

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR** aliuliza:-

Uchumi wa nchi yetu unayumba kutokana na ukosefu wa umeme wa uhakika hali inayosababisha kuyumba kwa uwekezaji na mfumko mkubwa wa bei na bidhaa za ndani:-

Je, Serikali haioni kuwa, kuna ulazima wa kuliwezesha Shirika la *NDC* ili liweze kuzalisha umeme wa uhakika wa Makaa wa Mawe ambao unaweza kuuzwa hata nje ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, umeme wa uhakika ni muhimu sana kwa uchumi na unatoa mchango mkubwa katika kupunguza mfumuko wa bei wa bidhaa ya kupanda kwa gharama za maisha kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imekuwa ikilijengea uwezo Shirika la Taifa la Mendeleo *(NDC)* kila mwaka ili liweze kumudu majukumu yake. Kwa hivi sasa, *NDC* imeweza kuchangia kwa kuibua miradi mitatu ya kuzalisha umeme wa uhakika kwa kutumia makaa ya mawe na upepo kama ifuatavyo:-

(i) Tayari Shirika la *NDC* limefanikiwa kumpata mwekezaji katika mradi wa mkaa wa mawe wa Mchuchuma. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Tanzania *China International Mineral Resource Limited* ambayo imeingia ubia na Serikali kupitia *NDC. (Makofi)*

(ii) Mheshimiwa Spika, Mradi mwingine wa *South* Ngaka wa kuzalisha umeme kutokana na makaa ya mawe unatekelezwa na Kampuni ya *TANCOAL ENERGY LTD.* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya Serikali kupitia *NDC* na Kampuni ya *Intra Energy Limited.*

Mradi huo tayari umeanza uchimbaji wa makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi viwandani na unatarajiwa kuzalisha umeme kiasi cha megawati 200 mwa 2015 hadi Megawati 400 mwaka 2017/2018 na kuunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.

(iii) Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme wa Upepo unaotekelezwa na Kampuni ya *Geo Wind Power Tanzania Limited* ambayo ni ya ubia kati ya Serikali kupitia *NDC* na *TANESCO* na Kampuni ya *Power Pool East Africa Limited (PPEAL).* Kampuni ya iliyoingia ubia inategemea kuzalisha umeme kiasi cha megawati 50 ifikapo Oktoba, 2013 na kufikia megawati 300 ifikapo 2018/2019.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri yanayoleta matumaini na nitakuwa na masuala mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na jibu lake la msingi amezungumzia kwamba mradi wa Mchuchuma tayari umeshapata mwekezaji na Serikali itakuwa ina hisa kwa kupitia *NDC.*

Je, nataka kuelewa hisa hii ya Serikali imefikia angalau asilimia 50. Na kama jibu litakuwa ndio suala la pili litakufa.

Kama jibu litakuwa hapana nataka kuelewa je, Serikali haioni kama tutakuwa tuko chini ya asilimia 50 kwamba itakuwa tumekalia mkiani kwenye punda wetu wenyewe nikiwa na maana ya kwamba tutakuwa hatuna maamuzi kwenye Bodi ambazo kwamba zitakuwa zina maamuzi ya msingi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ana wasiwasi

kwamba katika uwekezaji wa *NDC* katika kupitia makaa ya mawe anakuwa na wasiwasi wa asilimia 50 kama tumefikia au hatujafikia, kama Serikali.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kutekeleza miradi hii ya kupata umeme kwa njia ya makaa ya mawe ni kwamba iko sehemu mbili.

Sehemu ya kwanza ni ule upembuzi yakinifu, usanifu wa mwanzo wa kutafuta makaa yenyewe kama yapo au hayapo. Sasa Serikali kupitia *NDC* ndiyo imeingia ubia na huyu mwekezaji wa awali ya kwanza ya kutafuta makaa yenyewe.

Lakini katika kutafuta makaa ya mawe mwanzo, huyu mwenzetu mwekezaji ameonyesha nia kwamba ana uwezo na ana fedha na hivi ninavyoongea mwekezaji huyu amewekeza dola bilioni 3 za America, amewekeza kwenye mradi huu ili iweze kupata kujua kwamba kuna makaa ama hakuna.

Katika hii awamu ya kwanza Serikali imeingia ubia wa asilimia 20 na mwekezaji amepewa asilimia 80 kwa sababu yeye ana fedha na anatafuta makaa na akishajua kwamba kuna makaa basi tunaingia tena mkataba mwingine ambao tayari tunajua kwamba asilimia 49 kwa Serikali ambapo tutakuwa tumeshajua kwamba makaa yameshapatikana na halafu kuna utaratibu mpya unaanza. Kwa sasa hivi Serikali imeingia ubia kwa sababu yule anayewekeza anachukua asilimia 80 na Serikali inachukua asilimia 20 baada ya makaa kugunduliwa asilimia 49 itakuwa ni hisa ya Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umeisha na leo tuna shughuli nyingi. Naomba niwatambue baadhi ya wageni tulionao humu ndani. Kwanza kabisa kuna Mheshimiwa Dkt. Nderakindo Perpetua Kessy, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki, sijui yuko wapi, ahsante karibu sana. (*Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao kwanza ni Kaimu Katibu Mkuu Bwana Selestine Jesimba. Ahsante sana. Kuna Kamishna wa Elimu Professa Stella Balalusesa. Ahsante sana nadhani nimetamka vizuri jina lako. Halafu tuna Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo na Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wakaguzi Wakuu wa Shule za Kanda, Wilaya na Wadau wa Elimu Nchini. Hawa ni wengi naomba msimame kwa pamoja kokote mliko. Ahsante sana tunawashukuru sana. (*Makofi)*

Halafu tuna familia ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi familia ya Mheshimiwa sijui inaongozwa na mama maana yake hawajasema. Iko wapi familia yake. Bila shaka inaongozwa na mke wake mpendwa na watoto wake. Ahsante sana. (*Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge kuna wageni 24 wa Mheshimiwa Betty Machangu ambao ni Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Mandaka kilichopo

Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na Wakufunzi wao wanne.

Naomba wasimame hapo walipo Walimu na Wakufunzi. Ahsante sana Walimu nategemea mtafanya kazi nzuri. Lakini inaongozwa na Bibi Leila Hoza, sasa hawakuniambia Leila Hoza ni nani? (*Makofi)*

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa David Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, ambao ni wazee kutoka Kata ya Chang'ombe Dodoma. Naomba wazee hao wote wasimame pale walipo. Wako wapi? Nadhani wamekosa nafasi watapata nafasi baadaye jioni.

Tuna wageni 26 wa Mheshimiwa Faith Mitambo ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Abbas Abdallah Matulilo. Naomba Waheshimiwa Madiwani wasimame walipo. Ahsante sana tunawashukuruni karibuni sana. Liwale ni mbali lakini mmefanikiwa kuja. Ahsante sana. (*Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Stephen Ngonyani maarufu kwa Professa Majimarefu ambao ni Madiwani 24 na Wenyeviti 15 kutoka Halmashauri ya Korogwe wakiongozwa na Mheshimiwa Sadik Yusuph Kalaghe. Hawa nao Waheshimiwa wasimame wote walipo. Ahsante sana karibuni sana. Mbunge wenu alikuwa anaumwa lakini sasa hajambo ndiyo maana mmekuja. Ahsante sana karibuni sana. (*Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Susan Lyimo ambao ni viongozi wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) wakiongozwa na Mheshimiwa Germima Salari. Naomba hawa Waheshimiwa wasimame hapa. Ahsante sana karibuni sana, Mheshimiwa Mbunge wenu anafanya kazi vizuri. (*Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Cecilia Paresso, ambao ni Bwana Peter Tahani na Fanuel Richard. Hawa ni wawakilishi wa vikundi vya wakulima toka Karatu. Wasimame walipo. Ahsante wako pale nashukuru karibuni sana wakulima, ahsante sana. (*Makofi)*

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ambao ni familia yake ikiongozwa na mke wake mpendwa Bayuni Kigwangalla. Wako wapi hao. Ahsante karibuni sana lakini sijawaona. (*Makofi)*

Halafu tuna wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo hawa ni wanafunzi 80 pamoja na Walimu wao kutoka Chuo cha *VETA Dodoma.* Hawa wapo karibu na sisi hapa wako wapi wanafunzi wa *VETA.* Ahsante sana karibuni sana nyie majirani zetu.

Tunao wanafunzi 60 pamoja na Walimu wao kutoka Shule ya Msingi Chang'ombe. Naomba hawa wanafunzi na Walimu wasimame. Ahsante sana Walimu na wanafunzi.

Tuna wageni 20 kutoka kikundi cha LISHE (Usalama wa Chakula na Haki za Watoto) wakiongozwa na Bi. Edna Kamaleki. Hawa watoto wa LISHE wako wapi. Nafikiri watapatikana baadaye wamekosa nafasi humu ndani.

Waheshimiwa matangazo ya kazi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 mchana kutakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Mussa Zungu yeye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa 7.15 watakuwa na kikao katika ukumbi Namba 219.

Mheshimiwa Susan Lyimo, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake wa Bunge (TWPG) anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa Umoja wa Wanawake wa Bunge wote (*Executive Committee)* hapa kuwa leo watakuwa na kikao chao saa 7.15 katika Ofisi ya *TWPG* ghorofa ya 2 Utawala. Hii ni Kamati Tendaji sio Wanawake wote katika Ofisi yenu mtakuwa na kikao.

Halafu, Ofisi yangu inatangaza kwamba tunawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kuna mwaliko wa futari iliyoandaliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu leo tarehe 13 Agosti, 2012 nyumbani kwake kuanzia saa 12.30. Waheshimiwa Wabunge wote mnakumbushwa leo kuna futari ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mulugo naona haikuletwa mapema anao wageni wake, familia ya Mheshimiwa Mulugo naomba wasimame hapo walipo. Ahsante sana. (*Makofi)*

Halafu wako Madiwani 29 kutoka Bagamoyo na wenyewe wako wapi? Aaah !! Ahsanteni. Kumbe karibu nisiwatangaze haiukuandikwa vizuri. Nashukuru. Hawa ni Madiwani wa Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Karibuni sana nashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge nimepewa pia taarifa hapa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hatakuwa ndani ya Bunge kwa sababu amesafiri kwenda Kondoa atakuwa hayupo kuanzia tarehe 12 mpaka 13 Agosti. Anasema wakati ambapo hayupo atakayekaimu nafasi ya Shughuli za Serikali Bungeni atakuwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

**UCHAGUZI MDOGO WA MBUNGE WA BUNGE LA AFRIKA**

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa Spika, kama nilivyowatangazia tarehe 6 Agosti, 2012 leo tarehe 13 Agosti, 2012 baada ya kipindi cha maswali na kama *Order Paper* ya leo inavyoonyesha.

Mheshimiwa Spika, kutakuwa na Uchaguzi Mdogo kujaza nafasi moja ya kundi "C" Wabunge Wanaume Tanzania Bara, ilioachwa wazi na Mheshimiwa Stephen Julius Masele, aliyekuwa mwakilishi katika Bunge la Afrika baada ya kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

Kutokana na uteuzi huo nafasi yake katika Bunge la Afrika imebaki kuwa wazi. Hivyo Bunge linatakiwa kuchagua Mjumbe mwingine kujaza nafasi hiyo.

Wabunge waliojitokeza kuchukua fomu walikuwa Wabunge wawili, ambao ni Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla na Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda. (*Makofi)*

Siku ya kurudisha fomu *nomination day* ilikuwa ni siku ya Ijumaa tarehe 10 Agosti, 2012 saa kumi jioni ambapo wagombea wote walirudisha fomu kwa wakati uliopangwa.

Kwa mujibu wa kifungu cha 9 (5) cha Kanuni za Bunge kila mgombea atatakiwa afike mbele ya

Wabunge na kujieleza kwa lugha ya kiingereza na kuulizwa maswali, kujibu na kuomba kura. Baada ya wagombea kujieleza, karatasi za kura zitatolewa ambapo kila Mbunge atapewa karatasi moja ya kupigia kura na atatakiwa kupiga kura katika jina la mgombea mmoja. Hiyo ndiyo taarifa ya Uchaguzi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunao Uchaguzi wa Waheshimiwa wawili na kwa utaratibu wetu majina yao yamepangwa *in alphabetical order* ninapenda Mheshimiwa Said Mohammed Mtanda atoke nje. Akirudi tutampa dakika 5 ajieleze au dakika 5 ni nyingi ni dakika 5 au dakika 3?

**WABUNGE FULANI:** Dakika 5.

**SPIKA:** *Order please!* Kwa kuwa mnawafahamu wote ninawapa dakika 3, kwa kuwa siyo wageni kwetu. Lakini pia tutawauliza maswali yasiyozidi matatu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Said Mohammed Mtanda atoke nje na tutamwita Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla aje ajieleze. Dkt. Kigwangalla unakaribishwa kujieleza kwa muda usiozidi dakika tatu (3) *and you are going to use English language given 3 minutes to explain yourselves and then there will be three questions from Members of the Parliament.*

**HON. DR. HAMIS A. KIGWANGALLA:** Thank you Honourable Speaker, Honourable Heads of Government Business in the House, Honorable, Heads of Opposition in the House and Fellow Honorable

Members of Parliament. *Asalaam Aleykum, Tumsifu Yesu Kristo.*

Honourable Speaker, standing before you here today is my Humble self going by the name Hamis Kigwangalla, Member of Parliament from Nzega. I am greatly privileged to have this opportunity to contest for the post of Member of Parliament in the Pan African Parliament. I feel greatly humbled that I have been part of noble House for the past two years and I feel greatly privileged to receive your advice, to have leant from you, to have been coached and menitored by all of you fellow Members of Parliament.

I believe I am ready and capable to save the interest of our nation, to represent the interest of our nation and the Pan African Parliament successfully . I believe I have tools due to my education, experience, skills and the teachings that I have received from you for the past two years.

I am one of the few Tanzanians who are privileged to have world class qualifications in the number of, Three minutes?

**HONOURABLE SPEAKER:** Three minutes and not much.

**HON. DR. HAMIS A. KIGWANGALLA**: Honourable Speaker, Honorable Heads of Government Business in the House, Honorable Head of opposition and fellow Members of Parliament I beg for your votes please trust

me I am capable and with my knowledge, skills and experience I am ready to save you. Thank you very much and God Bless you all.

**HONOURABLE SPEAKER:** Any questions? Oh! only three ok Honorable Zitto.

**HON. KABWE ZUBERI ZITTO:** Honourable Kigwangalla, on the third of August our foreign Minister will be leading a delegation to Mzuzu in Malawi to discuss the border disputes between Tanzania and Malawi. If your elected as a Member of Pan African and the foreign Minister ask you for an advice what will be the best option to solve our boarder dispute in Malawi.

**HON. DR. HAMIS A. KIGWANGALLA**: Thank you Honourable Kabwe Zitto for your question in a democratic country we consider the fact that the Pan African Parliament is actually founded on the strong foundation of democracy, piece and stability. I believe the same values are also being uphold by our constitution. What I believe is we need to solve all conflicts democratically, in a transparent manner and uphold Good Governance so that the African people as Africans we can live in piece and harmony as brothers and sisters of this wonderful continent.

**HONOURABLE SPEAKER:** The second question will come from the Minister of Energy and Minerals.

**HON. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Honourable candidate, the Pan African Parliament is based in South Africa and at the moment there is a debate going on within the ANC of South Africa on whether to nationalize all the mines or not. What is your opinion on nationalizing of Tanzanian mines including other African mines?

**HON. DR. HAMIS A. KIGWANGALLA**: Thank you Honourable Minister Professor Muhongo honestly speaking I believe in solving conflicts democratically, I believe on earning what is deservedly ours following and upholding the rule of Law and Good Governance in our country. I wouldn't be proposing that we actually confiscate all mines as what my good friend Julius Malema was proposing in his country but I would rather actually propose for a democratic process whereby we will negotiate with the mining companies to give more to our country because we deserve more.

**HONOURABLE SPEAKER:** Third question will come from Honourable Saada Mkuya Salum.

**HON. SAADA MKUYA SALUM:** Honourable candidate when you were explaining on yourself you mentioned that you are one of the few Tanzanians who have qualifications to the Pan African. But why do you consider yourself as so special to be in that Pan African Parliament.

**HON. DR. HAMIS A. KIGWANGALLA**: In the first place I will say I hold a Medicine Degree from University of Dar es salaam, a Masters of Public Health from University of Caroline, Institute in Sweden, a masters of Business Administration from Institute of Technology also in Sweden and I am Currently pursuing my Doctorate Degree in Public Health Specializing in Health Economic from the University of Cape Town. Furthermore I had an opportunity to serve in a number of Bodies and Committee, Local and International I have a wealthy of experience and I am ready to serve this country and our beloved continent more succefully and in a right way. Therefore I consider my selves highly qualified for the job to serve as a Pan African Parliament Member.

**HONOURABLE SPEAKER:** Thank you this was the last question. Can you say something for the voters, the last word?

**HON. DR. HAMIS A. KIGWANGALLA**: Honourable Speaker, Honourable head of opposition in the House and colleagues, brothers and sisters, mothers, fathers and uncles in the House I beg for your votes please trust me I am a changed men, I am a better Member of Parliament and will represent the interest of our country in a fruitful manner thank you very much and God Bless you all.

**HONOURABLE SPEAKER:** Honourable Said Mohammed Mtanda you have three minutes to

explain yourself and address this August Assembly, then there will be three questions, if any for you.

**HON. SAID M. MTANDA:** Your Excellence Madam Speaker, your Excellency Prime Minister, Honorable Deputy leaders of opposition, Honourable Members of this Assembly it is a great honor for me to stand before you so as to express myself and request for your support. To vote for me as to represent Tanzania in Pan African Parliament.

Honourable Speaker, my name is Said Mohammed Mtanda elected Member of the Parliament representing Mchinga Constuency which is in Lindi Region. I have been educated at University of Dar es salaam where I pursued Degree in Political Science and Public Administration as well as History I am a teacher by profession, Iam proud to day but one among my student is also among this Assembly Honorable Joshua Nassari.

I also recently graduated with the post graduate Diploma in Management of Foreign Relations which gave me enough experience and knowledge on issues related to protocol, diplomacy, conflict resolution and conflict management.

I have Leadership Certificate from United States of America which gives me enough courage that I am a good leader whom could represent Tanzania everywhere with confidence, before joining this

Assembly I worked with various organization including Soba Tanzania, teaching in various school and also as a personal assistant to Secretary General of Chama cha Mapinduzi (CCM).

Honourable Speaker, Pan African Parliament is a platform where African Countries meet and discuss challenges which affects Africa in order to bring about sustainable Development in Africa. I am here humbly to request Members of this Assembly to vote for me for sure I shall represent this country well. Thank you very much and I request for your vote.

**HONOURABLE SPEAKER:** Members of Parliament will ask you three questions if any. The First question will be from Honorable Khalifa.

**HON. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Honourable candidate you have just mentioned that you are intending to join the Pan African Parliament in Geopolitics there is so called Arab Spring. Can you mention two countries in Africa which face such a strategy.

**HON. SAID M. MTANDA:** I beg your pardon.

**HON. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** In the Geopolitics or the World Politics there is what is called Arab Springs which made some countries in the World

almost to follow down. Can you mention two countries in Africa which face such a strategy?

**HON. SAID M. MTANDA:** We have Tunisia and Libya.

**HONOURABLE SPEAKER:** The third question please, Professor Muhongo

**HON. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Honourable candidate, Africa's population is about 14% of the world's population. Economically Africa is accounting 2% of the Worlds GDP. When you take the OECD and Brits countries are accounting for the 80% of the Worlds GDP what is your personal strategy for Economic Development of the African continent.

**HON. SAID M. MTANDA:** Pan African Parliament is a platform whereby African meets and discuss challenges in Africa. So as part of that Parliament I am sure we shall discuss on the strategies on how to improve Economic situation in Africa this is not a question of being alone thank you and I beg for you vote.

**HONOURABLE SPEAKER:** Another question be asked by Honourable Leticia Nyerere.

**HON. LETICIA M. NYERERE:** Honourable candidate could you please tell us why are you contesting for the position and what are your objectives.

**HON. SAID M. MTANDA:** I am contesting for this post because it is vacant we need a representative to fill the vacant. But also I am confident that once you vote and elect me to became a member of Pan African Parliament I shall try to use my knowledge to represent this country.

**HONOURABLE SPEAKER:** Honourable Mtanda give us your last word.

**HON. SAID M. MTANDA:** My fellow Members of this Assembly you should be believe that I have confidence, I am a reliable person, who can be trusted to represent this country. I request you to vote for me being sure that the interest of Tanzania in this Assembly is going to be preserved. Thank you very much.

**HON.SPEAKER:** Thank you very much you can take your seat. The Clerk of National Assembly. May we have your attention please.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie muda huu ili Wabunge waliopo ndani waweze kuhesabiwa.

*(Hapa Kengele ilipigwa ili Wabunge waingie Ukumbini na kuhesabiwa tayari kupiga kura)*

**MHE. STEPHEN JULIUS MASELE:** Taarifa!

**SPIKA:** Taarifa lazima ihusiane na Uchaguzi!

**MHE. STEPHEN JULIUS MASELE:**Inahusu Uchaguzi Mheshimiwa Spika**.**

**SPIKA:** Atoe maelezo kwanza Msimamizi wa Uchaguzi.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa Wabunge tutagawa Karatasi za Kura ambazo zitakuwa na mfano wa namna hii. Ina majina mawili jina la kwanza ni Mheshimiwa Hamis Andrea Kigwangalla na jina la pili ni la Mheshimiwa Said Mohammed Mtanda.

Karatasi hii inatolewa kwa mujibu wa kifungu cha kumi cha kanuni za Uchaguzi wa Bunge la Afrika nyongeza ya (5) unachotakiwa kufanya ni kuweka alama ya tiki kwenye jina moja tu ukiweka alama mbili karatasi yako ya kura itakuwa imeharibika. Kila mpiga kura atapewa karatsi moja tu ya kupigia kura, ukishapiga kura utaikunja tutazungusha masanduku ya kura hapohapo ulipo utatumbukiza karatasi yako ya kura na itakuwa ndiyo mwisho wa kupiga kura.

Baada ya hapo atakayepata kura nyingi zaidi atahesabiwa kuwa ni mshindi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Stephen Masele.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI NA NISHATI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wagombea hawa wanachukua nafasi yangu nilitaka kuwatakia kila la heri wote wameonyesha uwezo mkubwa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ukisikia mtu anapoteza wakati ndiyo huyo!(*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa tunaomba tupewe idai ya Wabunge na mpaka sasa hivi waliopo ndani ni Wabunge 210, kwa hiyo karatasi za kura zigawiwe.

Waheshimiwa Wabunge mnapopiga kura muwe wastaarabu, ninyi wote mmesoma habari ya kuambizana ni sehemu ya kutokuendelea. Watu wasioendelea wanaambizana niandike wapi.(*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge pokeeni karatasi tuandike na tuweke katika boksi ya kura. Tutumie muda mfupi na wanaokusanya kura wawe karibu kwa sababu kupiga kura ni kazi rahisi.

Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu, tunapopiga kura hakuna sababu ya kuongea. Kuna mtu hajapata karatasi ya kura? Naomba mtulie hapo

mlipo watakuja kukusanya karatasi hapo kwenye nafasi zenu.

Tungependa Mheshimiwa Mtanda atoe mtu wa kwenda kusimamia kura zake.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ninamteua Eng. Masauni.

**SPIKA:** Hata wewe mwenyewe unaweza kwenda siyo lazima utaje mtu.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, basi nitakwenda mwenyewe. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Haya, Dkt. Kigwangwala.

**MHE. HAMISI A. KIGWANGWALLA:** Mheshimiwa Spika, nitakwenda mwenyewe.

**SPIKA:** Haya, ahsanteni sana.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kupiga kura nimeingia sasa hivi.

**SPIKA:** Sawa, huyu anaongezeka anakuwa Mbunge wa 111. Naomba mpeni karatasi ya kupiga kura. Mheshimiwa Jafo kuna nini?

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, na mimi niliingia katika rekodi ya mwanzo sikuweza kuhesabiwa nilitoa taarifa kwa Katibu anayekusanya.

**SPIKA:** Kwa hiyo hujapiga kura?

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, nimeshapiga kura tayari.

**SPIKA:** Hukuhesabiwa?

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Rekodi ya kwanza sikuhesabiwa.

**SPIKA:** Umehesabiwa.

Waheshimiwa Wabunge, je, tumekusanya kura zote? Mheshimiwa Dkt. Kigwangwala na Mheshimiwa Said Mtanda naomba sogeeni mbele, pamoja na sekretariati ya Bunge mtakwenda huko *Speakers Lounge* mkaendelee na shughuli.

Tunaendelea na shughuli zingine, Katibu tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2012/2013 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati

ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusiana na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa mwenye afya njema.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia fursa hii kuwapongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, kwa kuiongoza nchi yetu vema na kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniteua tena kuongoza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Naahidi kwamba nitajitahidi kwa uwezo wangu wote, kuendelea kufanikisha malengo ya Wizara pamoja na yale ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Bagamoyo kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za

kimaendeleo. Hili linathibitishwa kwa ujio wa Madiwani wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo hapa Bungeni wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Shukuru Mbato na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Hashim Makida.

Nawashukuru sana Madiwani hawa na ninawaahidi wananchi wa Jimbo langu la Bagamoyo kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa na kwa uwezo wangu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe Spika na Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge, kwa uendeshaji bora wa shughuli za Bunge. Tunaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwawezesha na kuwaongoza.

Mheshimiwa Spika, napenda kwa namna ya pekee kumshukuru Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Sekta ya Elimu. Kamati hii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta Mbunge, imeichambua na kuijadili kwa kina bajeti ya Wizara yangu.

Kamati pia imetembelea miradi mbalimbali na kufanya mikutano na wanafunzi na viongozi wa wanafunzi ili kuelewa maendeleo na changamoto zilizopo katika sekta hii.

Ushauri na maelekezo ya Kamati hii yameiwezesha Wizara kukamilisha bajeti yake kwa muda muafaka. Aidha, ushauri, maoni na maelekezo ya Kamati yamechangia katika kuimarisha Sekta ya Elimu katika ngazi zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na majanga, pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini. Aidha, kwa namna ya pekee, ninachukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Watanzania wote kutokana na ajali ya meli ya *MV. Skagit* iliyotokea tarehe 18 Julai, 2012.

Vilevile, napenda kuchukua fursa hii kutoa salamu za pole kwa Serikali ya Kenya na wananchi wa Kenya kutokana na ajali ya basi iliyotokea tarehe 10 Agosti, na kupoteza maisha ya raia 12 wa Kenya na wengine kujeruhiwa. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi. Aidha, wale waliopata maumivu na bado wanaendelea kujiuguza, ninawaombea, Mungu awajalie nafuu ya haraka ili waweze kurudi katika shughuli zao na kuendelea na ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, niungane na wenzangu waliotangulia katika kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya, Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Mei, 2012. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mussa Zungu

Azzan, Mbunge wa Ilala, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge.

Nawapongeza pia Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge waliochaguliwa kuchukua nafasi zilizoachwa wazi. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Bunge lako Tukufu kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki. Natarajia kwamba wote walioteuliwa na kuchaguliwa watatumia nafasi hizo kwa manufaa ya Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe; Katibu Mkuu Mstaafu, Profesa Hamisi Omari Dihenga; Kaimu Katibu Mkuu Ndugu Selestine Muhochi Gesimba pamoja na aliyekuwa Kaimu Kamishna wa Elimu Bibi Marystella Maufi Wassena, pamoja na Kamishna wa Elimu Profesa Eustela; Wakurugenzi, Viongozi wa Wakala, Mashirika, Mabaraza, Taasisi, Tume na Vyuo Vikuu vilivyo chini ya Wizara; Viongozi katika ngazi mbalimbali na watumishi wote, kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na maandalizi ya Bajeti hii.

Aidha, shukurani zangu ziwaendee viongozi wa vyama vya wafanyakazi, vyama vya wanataaluma, wanafunzi, na wadau wa maendeleo kwa ushirikiano wao katika kuiendeleza Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri waliotangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Katavi, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu na Mbunge wa Jimbo la Bunda; na Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Waziri wa Fedha na Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa ujumla katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na Matumizi na mwelekeo wa uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013. Naomba kuwashukuru waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja za Mawaziri waliotangulia. Maoni ya Waheshimiwa Wabunge hao yamesaidia kuboresha mipango ya Serikali katika Sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 ni mwaka ambao Serikali itafanya Sensa ya Watu na Makazi. Kutokana na umuhimu wake Wizara yangu imetoa maelekezo kwa Wakuu wa Taasisi za kielimu katika ngazi zote, kurekebisha mihula na likizo zao ili kuwezesha wanafunzi na wanachuo kuhesabiwa pamoja na familia zao, na hivyo kazi ya Sensa kufanyika kwa ufanisi. Aidha, kwa kuwa sehemu ya nguvukazi inayoshiriki katika kuhesabu watu inatokana na walimu, Wizara imehakikisha kuwa ratiba hiyo haiathiri masomo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kufanya mapitio katika maeneo yafuatayo: Utekelezaji wa Ilani

ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, majukumu ya Wizara ya Kisera na ya kiutendaji, Utekelezaji wa Mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya CCM YA mwaka 2010 na utekelezaji wake; Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Sekta ya Elimu ilielekezwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 85(a):- Kuhusu Elimu ya Awali:-

(i) kuhakikisha kuwa kila Shule ya Msingi ina darasa la Elimu ya Awali lenye madawati yanayolingana na hali ya watoto wa elimu hiyo;

(ii) kujenga vyoo kwa ajili ya watoto wa Elimu ya Awali ili wasiingiliane na wale wa shule za msingi; na

(iii) kuandaa walimu wengi wa Elimu ya Awali na kuwapanga katika shule zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi, Serikali ilitoa mwongozo unaoelekeza kila Shule ya Msingi kuwa na darasa la Elimu ya Awali. Aidha, uandikishaji wa wanafunzi katika madarasa ya Elimu ya Awali umeongezeka kutoka wanafunzi 925,465 mwaka 2010 hadi 1,034,729 mwaka 2012. Kiwango cha uandikishaji kwa sasa ni asilimia 41.8, na uandikishaji wa rika lengwa (miaka 5-6) ni asilimia 39.9.

Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa Elimu ya Awali inapata rasilimali stahiki kama inavyoelekezwa katika MMEM II, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Elimu, imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika madarasa ya Elimu ya Awali kwa kuongeza idadi ya vyoo kwa ajili ya wanafunzi kutoka 934 mwaka 2010 hadi kufikia vyoo 1,097 mwaka 2012.

Aidha, idadi ya walimu wenye taaluma ya kufundisha Elimu ya Awali iliongezeka kutoka walimu 2,961 mwaka 2010 hadi 3,095 mwaka 2012; na walimu wote wanaohitimu mafunzo ya Cheti wanapatiwa mafunzo ya ufundishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(b): Elimu ya Msingi. Ilani imeelekeza kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya Pili (MMEM II: 2007 – 2011) na kuandaa na kutekeleza Awamu ya Tatu (MMEM III).

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II) kwa kutoa Ruzuku ya Uendeshaji wa Shule, ambapo wastani wa Shilingi 6,025 zilitolewa kulinganisha na lengo la Shilingi 10,000 kwa kila mwanafunzi wa Elimu ya Msingi. Aidha, MMEM II

umefanyiwa mapitio ili kuwezesha maandalizi ya MMEM III.

Katika utekelezaji wa mpango huu, idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika Darasa la Kwanza iliongezeka kutoka 1,356,574 mwaka 2010 hadi 1,404,998 mwaka 2012.

Aidha, watoto wa jinsi zote wanapata fursa ya kuandikishwa katika Elimu ya Msingi; idadi ya Shule za Msingi nchini imeongezeka kutoka 15,816 mwaka 2010 hadi 16,331 mwaka 2012; kiwango cha ufaulu kimeongezeka kutoka asilimia 53.5 mwaka 2010 hadi asilimia 58.3 mwaka 2011.

Idadi ya walimu wa Shule za Msingi imeongezeka kutoka walimu 175,449 mwaka 2011 hadi kufikia 180,987 mwaka 2012 na uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi umeimarika kutoka kwa mwalimu 1:48 mwaka 2011 hadi 1:46 mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(c): Kuhusu Elimu ya Sekondari. Ilani imeelekeza kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili (MMES II: 2010 - 2014), kuandaa na kutekeleza Awamu ya Tatu (MMES III).

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010, iliahidi kutekeleza azma ya kuwa na angalau shule moja ya ya Kidato cha 5 na 6 kwa kila Tarafa. Ili

kutekeleza azma hii, Wizara ilifanya ufuatiliaji na uchambuzi wa mahitaji ya shule zinazostahili kuanza kupokea wanafunzi wa Kidato cha 5 mwaka 2012 katika Mikoa yote ili kubaini miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kukidhi vigezo vya uanzishwaji wa Kidato cha 5.

Aidha, Wizara iliandaa Miongozo ya ujenzi wa miundombinu ya shule na udhibiti wa ubora wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuisambaza kwa wadau na iliongeza idadi ya Shule za Sekondari zenye Kidato cha 5 na 6 kutoka 205 mwaka 2010 hadi 207 mwaka 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya ufuatiliaji na tathmini katika shule 264 (shule 2 kila Halmashauri) ili kubaini gharama halisi ya kujenga au kukarabati shule hizo ili zifikie kiwango bora (*functional schools*). Miongozo ya ujenzi imeshaandaliwa na kutumwa katika Halmashauri kwa lengo la kuanza mchakato wa kupata wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa ufaulu unaongezeka katika ngazi zote za Elimu ya Sekondari, Wizara ilitoa mafunzo kwa walimu 3,042 kwa ajili kuimarisha ufundishaji na kujifunza kwa masomo ya Sayansi, Hisabati na English na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 210. Aidha, Wizara ilisambaza jumla ya vitabu 1,520,000 na nakala 60,000 za Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo ya Sayansi katika shule 1,500 pamoja na nakala 15,000 za *DVD* za miongozo ya walimu ya kufundishia Sayansi kwa vitendo katika shule za Serikali na zisizo za Serikali. Vilevile, ilitoa mafunzo ya

wawezeshaji 60 wa kitaifa na 336 wa mikoa katika masomo ya Sayansi na Hisabati.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(d): Elimu ya Ualimu. Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Ualimu *(Teacher Development Management Strategy – TDMS) katika utoaji wa mafunzo ya Ualimu.*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010, Wizara ilidahili jumla ya wanachuo 37,698 katika ngazi ya Cheti na Stashahada. Hili ni ongezeko la asilimia 2.9 ukilinganisha na idadi ya wanachuo 36,648 waliodahiliwa mwaka 2010/2011 ambapo, walimu 292 kati ya hawa ni wa fani ya Elimu ya Michezo. Aidha, walimu 2,052 walipatiwa mafunzo kazini ili kuinua sifa na ubora wa ufundishaji kupitia programu ya Mafunzo ya Walimu Kazini kwa Elimu ya Msingi (MWAKEM) ngazi ya shule, na Wakufunzi 120 walihudhuria mafunzo ya kufundisha na kujifunza kwa kutumia TEHAMA; na Wakufunzi 573 walijengewa uwezo wa kufundisha masomo ya Sayansi, *English* na TEHAMA kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Wakuu wa Vyuo vya Ualimu 34 vya Serikali walipatiwa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Ualimu kwa ufanisi. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mafunzo haya ulifanyika katika vyuo vya ualimu 18, kati ya vyuo 34 vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(e): Elimu ya Juu. Kusimamia kwa ukamilifu Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza lengo hilo, Wizara ilifanikiwa kuongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya Elimu ya Juu kutoka wanafunzi 139,638 (wanawake 49,959) mwaka 2010/2011 hadi wanafunzi 166,484 (wanawake 60,592) mwaka 2011/2012. Hili ni ongezeko la asilimia 19. Aidha, idadi ya wanafunzi madaktari wa binadamu, meno na tiba ya mifugo iliongezeka kutoka 1,750 mwaka 2010/2011 hadi 1,900 mwaka 2011/2012.

Mafunzo ya madaktari wa binadamu, meno na tiba ya mifugo yanatolewa katika vyuo vifuatavyo: Chuo Kikuu cha 12 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013 Afya na Sayansi Shirikishi - Muhimbili, Chuo Kikuu cha Dodoma, *Hubert Kairuki Memorial University, Kilimanjaro Christian Medical College, Weil Bugando University College of Health, International Medical and Technological University* na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Idadi ya wanafunzi waliopata mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imeongezeka kutoka wanafunzi 91,568 mwaka 2010/2011 hadi wanafunzi 93,176, mwaka 2011/2012.

Aidha, Vyuo Vikuu vitatu (3) vilianzishwa ambavyo ni: *Eckenford Tanga University, Jomo Kenyatta University of Agriculture na University of Bagamoyo;* na Vyuo Vikuu vishiriki vitatu (3) vilianzishwa ambavyo ni: *Jordan University College; St. Francis University College*

*of Health and Allied Sciences; na St Joseph College of Engineering and Technology.* Jumla ya programu 81 za ngazi ya Shahada ziliidhinishwa kufundishwa nchini katika mwaka 2011/2012.

Vile vile, mpango wa kuainisha na kuweka viwango vya programu za masomo ya biashara ulianza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(f): Mafunzo ya Ufundi. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya hali halisi ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini kwa ajili ya maandalizi ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi imekamilika. 13 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013

Ibara 85(g): Elimu ya Watu Wazima yenye Manufaa:-

(i) Kuandaa na kutekeleza mpango kabambe wa Elimu ya Watu wazima yenye manufaa nchini kote;

(ii) Kuimarisha Mipango ya Elimu ya kujiendeleza ikiwa ni pamoja na Elimu Masafa na Ana kwa Ana;

(iii) Kuimarisha utoaji wa elimu nje ya mfumo rasmi kupitia mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Waliokosa (MEMKWA) kwa kushirikiana na wadau wengine;

(iv) Kuinua ubora wa Elimu ya Watu Wazima kupitia Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA); na

(v) Kuimarisha uwezo wa watendaji katika usimamizi na menejimenti ya programu za elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza utoaji wa Elimu ya Watu Wazima yenye manufaa, Wizara ilifanikiwa kuandaa kitabu cha Mazoezi cha Mwanakisomo, Kiongozi cha Mwalimu cha Kufundishia, Kiongozi cha Msimamizi na Filamu ya Mpango wa 'Ndiyo Ninaweza' ya kufundishia stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

Aidha, Wizara iliweza kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika mpango huu na kufanya ufuatiliaji katika vituo ambavyo mpango huu utatekelezwa; kuandaa rasimu ya Sera na Mwongozo wa utekelezaji wa programu za Elimu ya Sekondari kwa njia ya Ana kwa Ana; kuandikisha wanafunzi 76,867 ili kupata Elimu ya Msingi katika vituo chini ya mpango huu na kuandikisha wanakisomo 907,771 katika mpango wa MUKEJA; kufanya uchambuzi wa mahitaji ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia na kusambaza vitabu 450 katika Halmashauri 147 ambazo ni Dodoma, Kinondoni, Ilala, Temeke, Mkuranga, Kisarawe na Bagamoyo; na kutoa mafunzo ya usimamizi na uratibu wa vituo vya MUKEJA kwa Maafisa wa Wizara 10, Mikoa 10,

Halmashauri 20 na walimu wanaofundisha katika vituo 95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hali ya sekta ya elimu nchini. Majukumu ya Wizara. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekabidhiwa majukumu ya kuweka viwango vya ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi za Elimu ya Awali na Msingi; Elimu ya Sekondari; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya ya Mfumo rasmi; Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Elimu ya Ualimu; Elimu ya Juu, Usajili wa Shule, na Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu pamoja na Taasisi na Mabaraza yaliyo chini yake.

Wizara, pia ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa utoaji wa elimu kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini, pamoja na kufanya mapitio, kuandaa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sera, Mipango, Sheria na kanuni za elimu zilizopo, kulingana na mabadiliko ya dhima na dira ya Serikali; na kuandaa mikakati ya utekelezaji wake. Aidha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ndiye msimamizi mkuu wa masuala ya taaluma katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inatekeleza mipango mbalimbali ili kuinua ubora wa elimu itolewayo. Mipango hiyo ni pamoja na: Mpango wa Maendeleo 15 *Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013* ya Elimu ya Msingi (MMEM); Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES); Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu (TDMS); na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU). Katika kutekeleza

mipango hiyo, Wizara imepata mafanikio mbalimbali na kukabiliwa na changamoto kadhaa.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2010 hadi 2012, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imepata mafanikio yafuatayo:-

(a) Uandikishaji wa wanafunzi katika madarasa ya Elimu ya Awali uliongezeka kutoka wanafunzi 925,465 mwaka 2010 hadi 1,034,729 mwaka 2012 na idadi ya wanafunzi walioandikishwa Darasa la Kwanza iliongezeka kutoka 1,356,574 mwaka 2010 hadi 1,404,998 mwaka 2012;

(b) Idadi ya Shule za Msingi nchini iliongezeka kutoka 15,816 mwaka 2010 hadi 16,331 mwaka 2012;

(c) Kuimarika kwa uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika Shule za Msingi kwa asilimia 11 kutoka uwiano wa 1:51 mwaka 2010 hadi 1:46 mwaka 2012;

(d) Kiwango cha ufaulu katika ngazi ya Elimu ya Msingi kiliongezeka kutoka asilimia 53.5 mwaka 2010 hadi asilimia 58.3 mwaka 2011, na idadi ya walimu wa Shule za Msingi iliongezeka kutoka 165,856 mwaka 2010 hadi 180,987 mwaka 2012;

(e) Uandikishaji wa wanafunzi wa Kidato cha I - IV uliongezeka kutoka 1,566,685 (wasichana 699,951) mwaka 2010 16 *Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/13* kufikia wanafunzi 1,802,810 (wasichana 847,849) mwaka 2012; na uandikishaji wa wanafunzi wa Kidato cha 5-6 uliongezeka kutoka 72,014 (wasichana

28,577) mwaka 2010 kufikia 81,462 (wasichana 25,950) mwaka 2012;

(f) Uandikishaji wa wanafunzi katika Kidato 1-6 uliongezeka kutoka 1,638,699 (wasichana 728,528) mwaka 2010 kufikia 1,884,272 (wasichana 873,798) mwaka 2012; idadi ya walimu wa Shule za Sekondari iliongezeka kutoka 40,517 (shule za Serikali 30,252) mwaka 2010 kufikia walimu 65,086 (shule za Serikali 51,469) mwaka 2012;

(g) Udahili katika Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinavyotoa elimu na mafunzo ya ufundi stadi uliongezeka kutoka 102,217 (wanawake 50,190) mwaka 2010 hadi 121,348 (wanawake 56,849) mwaka 2011, ambalo ni ongezeko la asilimia 27; Vyuo vya Elimu ya Ufundi (*Technical Education and Training*) vilivyosajiliwa viliongezeka kutoka 224 mwaka 2010 hadi kufikia Vyuo 260 mwaka 2012;

(h) Udahili wa wanachuo katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali uliongezeka kutoka wanachuo 36,648 (wanawake 16,597) mwaka 2010 hadi 43,258 (wanawake 18,898) mwaka 2012;

(i) Wakufunzi 573 walipewa mafunzo kazini ya ufundishaji bora wa masomo ya Sayansi, Hisabati na *English* kwa vitendo, na walimu 3,323 walipewa mafunzo kazini kuhusu mbinu shirikishi katika kufundisha na kujifunza masomo ya Sayansi na Hisabati;

(j) Washiriki wa Programu za Elimu ya Watu Wazima na 17 *Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013* Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ilikuwa kama ifuatavyo: Elimu Masafa na Ana kwa Ana 49,533 (2009) hadi 62,533 (2011), MUKEJA 924,893 (2010) hadi 907,771 (2012); MEMKWA 72,799 (2010) hadi 76,867 (2012);

(k) Idadi ya Vyuo Vikuu iliongezeka kutoka 34 mwaka 2010 hadi 46 mwaka 2012; na udahili wa wanafunzi wa Vyuo Vikuu uliongezeka kutoka wanafunzi 139,638 (wanawake 87,778) mwaka 2010/2011 hadi kufikia 166,484 (wanawake 60,592) mwaka 2011/2012; *(Makofi)*

(l) Idadi ya wanafunzi waliopatiwa mikopo kwa ajili ya Elimu ya Juu iliongezeka kutoka 91,568 mwaka 2010/2011 hadi kufikia 93,176 Mwaka 2011/2012; Aidha, Wizara ilianza mfumo wa kupokea maombi ya mikopo kwa njia ya mtandao (*Online Loan Application System – OLAS*); na

(m) Ilitoa udhamini kwa mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa wahadhiri 634 wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, Changamoto.Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Sekta ya Elimu bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Kuwepo haja ya kuendelea kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote za elimu na mafunzo;

(b) Kuimarisha na kuongeza idadi ya samani, miundombinu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vikiwemo vifaa vya wenye ulemavu;

(c) Kuongeza kiwango cha ufaulu hususan katika masomo ya 18 *Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013* Hisabati, Sayansi, na English katika Shule za Msingi na Sekondari;

(d) Kupata vyanzo mbadala vya kugharimia Elimu ya Juu na kuimarisha urejeshwaji wa mikopo;

(e) Kukidhi mahitaji ya rasilimaliwatu katika ngazi zote za elimu na mafunzo;

(f) Kuimarisha usimamizi na uendeshaji katika ngazi zote za elimu na mafunzo;

(g) Kupunguza idadi ya watu wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK); na

(h) Kuongeza mafundi wa ngazi ya kati kwa kutoa fursa za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa wanafunzi wa aina zote, wakiwemo wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012 na makadirio ya mwaka 2012/2013. Naomba niendelee kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kisha nitoe mwelekeo wa Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Mapato ya Mwaka 2011/2012. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilipanga kukusanya maduhuli ya Serikali yenye thamani ya Shilingi 121,766,401,334.

Bajeti ya maduhuli ya Idara ilikuwa Shilingi 4,138,947,000, na ya Taasisi ilikuwa Shilingi 117,627,454,334. Hadi tarehe 30 Juni, 2012, jumla ya Shilingi 95,142,715,493 zilikuwa zimekusanywa, ambazo ni asilimia 78.14 ya makadirio. Kati ya hizo, Shilingi 5,119,639,163 zilikusanywa na Idara; na Shilingi 90,023,076,330 zilikusanywa na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Mwaka 2011/2012.Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilitengewa jumla ya Shilingi 659,296,862,000. Kati ya hizo, Shilingi 523,778,766,000 zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 135,518,096,000 zilikuwa ni za Miradi ya maendeleo.

Aidha, Wizara iliongezewa Shilingi 91,722,783,264 kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu, posho za nyumba za wahadhiri na mishahara ya wafanyakazi, na kufanya bajeti ya Wizara kufikia Sh. 751,019,645,264. Kati ya hizo, Shilingi 614,886,069,517 ni za bajeti ya matumizi ya kawaida na Shilingi 136,133,575,747 ni za bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

Hadi tarehe 30 Juni, 2012, jumla ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara yalikuwa Shilingi 594,449,397,517 ambayo ni asilimia 96.68 ya makadirio, na Matumizi ya Maendeleo yalikuwa Shilingi 93,043,293,557 ambayo ni asilimia 68.35 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya jumla kuhusu matumizi ya fedha zilizopokelewa, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012. Ofisi ya Kamishna wa Elimu, Idara na Vitengo vya Wizara. Ofisi ya Kamishna waElimu ina majukumu ya kuweka na kudhibiti viwango vya ubora wa elimu na utoaji wa elimu katika ngazi za Awali; Msingi; Sekondari; Mafunzo ya Ualimu; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; pamoja na Ukuzaji Mitaala, Uendeshaji Mitihani, Huduma za Maktaba na Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu.

Ofisi hii inajumuisha vitengo vya Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari, Elimu Maalumu, Elimu kwa Redio, Usajili wa Shule, Kitengo cha Ithibati ya Vifaa vya Elimu pamoja na Masuala Mtambuka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Ofisi ya Kamishna wa Elimu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilihamasisha Menejimenti ya Wizara na Wafanyakazi wengine na wanafunzi kuhusu utoaji wa elimu ya VVU na UKIMWI katika sehemu za kazi kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kufanya vikao vya wadau kuhusu elimu rika katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Tanga,

(ii) Kutoa mafunzo ya ushauri na unasihi kwa walimu 105 wa Ushauri na Unasihi wa Shule za Sekondari katika mkoa wa Tanga,

(iii) Kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo wa kufundisha 22 *Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013* stadi za maisha, Elimu ya Afya ya Uzazi na UKIMWI na kutoa huduma za unasihi shuleni kwa walimu 120 wa Shule za Msingi za Wilaya za Muheza na Handeni,

(iv) kuendesha mkutano wa wadau mbalimbali wanaojihusisha na masuala ya VVU na UKIMWI shuleni kwa kuhusisha wajumbe 50 kutoka Serikalini (WEMU, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na OWM-TAMISEMI), mashirika yasiyo ya kiserikali, *TACAIDS,* Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Tumaini, *UNICEF* na *UNESCO;*

(v) Kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa waelimishaji rika 200 kutoka katika vyuo vya Elimu vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuhusu utoaji wa huduma rafiki vyuoni, na usimamizi wa elimu rika vyuoni kwa ushirikiano na Shirika la UMATI;

(vi) Kupitia Mpango Mkakati wa Elimu ya UKIMWI katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo vya Ufundi; na

(vii) Kufanya mkutano wa wadau 50 wanaojihusisha na elimu ya Stadi za Maisha kutoka wizara na asasi mbalimbali, ambapo viashiria vya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Elimu ya Stadi za Maisha shuleni katika ngazi zote za Elimu viliandaliwa;

(b) Iliwezesha jumla ya Wanafunzi 410 wenye ulemavu wa aina mbalimbali kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2012 ambapo:- wasioona walikuwa 187 (wasichana 84); viziwi 125 (wasichana 60); wenye ulemavu wa akili 13 (msichana 01); na Wenye ulemavu wa Viungo 85 (wasichana 44);

(c) Iliandaa mwongozo wa utoaji wa huduma za kielimu kwa watoto wenye ulemavu wa ngozi na uoni hafifu;

(d) Ilihariri, kutafsiri na kuthamanisha ‘Mkakati wa Elimu Jumuishi’;

(e) Iliendesha mafunzo kuhusu Elimu Jumuishi kwa ajili ya Maafisa Elimu, na uelimishaji rika kwa ajili ya walimu na wanafunzi wenye ulemavu kutoka Halmashauri saba (7) za Magu, Makete, Mtwara, Bagamoyo, Hai, Siha na Temeke zilizo chini ya mradi wa *UNICEF;*

(f) Ilihuisha kivunge (*toolkit*) cha Elimu Jumuishi;

(g) Ilitafsiri taarifa ya utafiti unaohusu 'Ubora wa Elimu katika Nchi 15 za Kusini mwa Afrika' katika lugha ya Kiswahili;

(h) Ilitayarisha na kutangaza vipindi 350 vya Shule za Msingi na 26 vya mbinu za ufundishaji kupitia *TBC* Taifa;

(i) ilikamilisha 'Mpango Mkakati wa Maji, Afya na Usafi wa Mazingira' na kutoa mafunzo elekezi kwa wadau 72 wa ngazi ya Mkoa na Wilaya zote za Mkoa wa Rukwa na Wilaya ya Chunya, pamoja na walimu wakuu wa shule 8 za Sumbawanga;

(j) Iliendesha mafunzo kuhusu masuala ya 'Mabadiliko ya Tabianchi' kwa watumishi wa elimu kwenye ngazi ya Halmashauri katika mikoa ya Morogoro na Pwani pamoja na watumishi wa Wizara;

(k) Lisajili jumla ya shule 254. Kati ya hizo, 169 ni za sekondari (za Serikali – 77); shule 2 ni za Awali na 83 za Awali na Msingi. Aidha, ilisajili Vyuo vya Ualimu 7 visivyo vya Serikali;

(l) Ilizifutia usajili Shule za Sekondari mbili (2) ambazo ni 24 *Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2012/2013 Biafra Secondary School*' ya Dar es Salaam na '*Dodoma Central Secondary School*' ya Dodoma kutokana na mgogoro katika umiliki na usajili wa shule hizo;

(m) Ilitoa jumla ya nyaraka 19, zikiwemo:-

(i) Waraka Na. 14 wa mwaka 2011 unaokataza kusajili katika kidato cha 1 wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika;

(ii) Waraka Na. 1 wa mwaka 2012 unaoagiza urejeshwaji wa ada za mitihani ya Kidato cha 2;

(iii) Waraka Na. 16 wa mwaka 2011 unaozungumzia wastani wa ufaulu kwa mwanafunzi wa Kidato cha 2 na unaomruhu mwanafunzi kukariri mara moja tu;

(n) Iliridhia maombi 120 ya kujenga shule na kuthibitisha wenye shule na meneja 102; na

(o) Ilitoa leseni 266 za kufundisha, kati ya maombi 283 yaliyopokelewa.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Msingi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Kitengo cha Elimu ya Msingi, iliendelea kutekeleza '*Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi*' Awamu ya I - II (MMEM I - II) kwa ufanisi. Mojawapo ya malengo ya MMEM I - II ni kutoa Elimu ya Awali na Msingi kwa watoto wote wenye umri

wa kwenda shule. Uandikishaji katika Elimu ya Msingi ulishuka kutoka wanafunzi 8,363,386 mwaka 2010/2011 hadi 8,247,172 mwaka 2011/2012 kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 1. Kushuka kwa uandikishaji katika Elimu ya Msingi ni ishara kwamba malimbikizo ya watoto wa rika lengwa la kwenda shule yamekwisha. Aidha, idadi ya shule zote za msingi nchini iliongezeka kutoka 16,001 mwaka 2010/2011 kufikia shule 16,331 mwaka 2011/2012; hili ni ongezeko la asilimia 2.1.

Mheshimiwa Spika, Wizara, kupitia Kitengo cha Elimu ya Msingi, ilitekeleza yafuatayo katika Elimu ya Msingi: -

(a) Iliandaa 'Mwongozo wa Ufundishaji wa Elimu ya Awali' na kutoa semina elekezi juu ya mwongozo huu kwa watendaji wakuu wa Wilaya 36.

(b) Ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji wa Elimu ya Awali na Msingi katika mikoa 10 ambayo ni Kagera, Morogoro, Mara, Tanga, Mbeya, Pwani, Rukwa, Tabora, Shinyanga na Singida, ili kuhakikisha kuwa watoto wote wa rika lengwa wanaandikishwa katika Elimu ya Awali na Msingi na wanahudhuria masomo hadi kuhitimu.

(c) Ilifanya tathmini ya MMEM II katika mikoa sita ambayo ni Tanga, Pwani, Mtwara, Kigoma, Shinyanga na Manyara kwa kuwashirikisha wataalamu elekezi. Matokeo ya tathmini hiyo yatatumika katika kuandaa andiko la MMEM III.

(d) Iliratibu ‘Mpango wa Lishe Shuleni’ na kutoa mafunzo ya uendeshaji wa mpango huo kwa watendaji 194 katika Halmashauri za Chamwino na Longido. Aidha, mchakato wa kuanzisha mpango huu kitaifa unaendelea, ambapo Makala ya Mpango (*Concept Paper*) imewasilishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hatua zaidi.

(e) Iliandaa Mtihani wa Taifa wa Darasa la Nne na wa Ufundi Stadi wa mwaka 2011. Matokeo ya Mtihani wa Darasa la Nne yanaonesha kwamba ufaulu umepanda kutoka asilimia 53.52 mwaka 2010 hadi asilimia 58.28 mwaka 2011.

(f) Iliratibu uanzishwaji na uendeshaji wa Mradi wa Utoaji wa Elimu ya Msingi kwa kutumia TEHAMA (*TZ 21$^{st}$ Century Basic Education Programme*) mkoani Mtwara.

(g) Iliratibu uandaaji wa Sera Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (*Integrated Early Childhood Development Policy – IECDP).*

(h) Iitekeleza Mradi wa Elimu kwa Teknolojia (*Bridge IT*) unaolenga katika kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika ujifunzaji na ufundishaji wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Stadi za Maisha katika Shule za Msingi. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri 17 za Mikoa 7 ya mradi. Jumla ya shule 150 zinanufaika na mradi huu. Ufundishaji huu hutumia video kupitia Televisheni na hivyo kurahisisha ujifunzaji na ufundishaji kwa mwalimu na mwanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sekondari. Kitengo cha Elimu ya Sekondari kina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu katika ngazi ya Elimu ya Sekondari ambayo kimsingi ni kiungo kati ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Juu. Aidha, kitengo cha Elimu ya Sekondari kinasimamia utoaji bora wa elimu kwa usawa kwa Kidato 1–6, kuweka viwango, na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu ya sekondari itolewayo nchini.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sekondari hutolewa katika ngazi ya kawaida (*O-level)* ambayo huchukua miaka minne, na ngazi ya juu (*A-level*) ambayo ni ya miaka miwili. Katika mwaka 2011/2012, idadi ya shule zote za Sekondari nchini iliongezeka kutoka 4,367 mwaka 2010/2011 na kufikia 4,528 mwaka 2011/2012. Kati ya shule hizo, 3,508 ni za Serikali na 1,020 ni shule zisizo za Serikali. Aidha, shule za Sekondari zinazochukua wanafunzi wenye ulemavu ziliongezeka kutoka 35 hadi kufikia 39.

Jumla ya wanafunzi walioko katika shule zote za Sekondari nchini iliongezeka kutoka wanafunzi 1,789,547 (1,515,671 katika shule za Serikali) mwaka 2011 hadi 1,884,272 (1,602,752 katika shule za Serikali). Wanafunzi wa Kidato cha I hadi IV ni 1,802,810 (wasichana 847,849), na wanafunzi wa Kidato cha 5 na 6 ni 81,462 (wasichana 25,950). Idadi ya wanafunzi wa kike waliopo katika shule za Sekondari iliongezeka kutoka 802,554 mwaka 2010/2011 hadi 873,799 mwaka 2011/2012. Kuongezeka kwa wanafunzi wa kike ni kielelezo cha kuhamasika kwa wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike.

Idadi ya walimu walioko katika shule zote za Sekondari iliongezeka kutoka 52,146 (39,934 shule za Serikali) mwaka 2010/2011 hadi 65,025 (51,458 shule za Serikali) mwaka 2011/2012. Ongezeko la wanafunzi na walimu katika shule za Sekondari linatokana na mafanikio ya utekelezaji wa *Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) Awamu ya I – II* (MMES I-II) uliowezesha kujengwa kwa shule za Sekondari nyingi zaidi, na hivyo kuongeza fursa za elimu katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zinazotokana na ugatuaji wa uendeshaji wa shule za Sekondari, huduma kwa walimu na wanafunzi zinafanyika kwa mafanikio zaidi baada ya ugatuaji. Aidha, Wizara yangu inaendelea kuwa na dhamana ya Sekta ya Elimu, yenye wajibu wa kuweka viwango vya elimu bora kwa nchi yetu na kusimamia upatikanaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu, kupitia kitengo cha Elimu ya Sekondari, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu 3,042 wa Sayansi, Hisabati na English na 210 wa TEHAMA.

(b) Ilinunua kompyuta 210 na seti 42 za Televisheni kwa ajili ya Shule za Sekondari 21 zilizoteuliwa kuwekewa maabara moja ya TEHAMA kila moja.

(c) Ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya matokeo ya mafunzo kazini kwa walimu wa Shule za Sekondari katika ufundishaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati katika mikoa yote 21 ya Tanzania Bara, kwa ushirikiano na Idara ya Ukaguzi wa Shule.

(d) Iliwezesha kutolewa ruzuku ya uendeshaji ya shilingi bilioni 6.3 kwa ajili ya Halmashauri zote na kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya Ruzuku hiyo. Aidha, ilitoa mafunzo kwa Maafisa Elimu 21, Maafisa Taaluma 21 wa Mikoa, Maafisa Elimu Sekondari 132, Maafisa Taaluma 132 wa Halmashauri na Wakuu wa shule 2,437.

(e) Iligharimia mafunzo ya kuwajengea uwezo wahasibu 3, wakaguzi wa ndani 3 na waratibu wa MMES 4.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ualimu. Idara ya Elimu ya Ualimu inasimamia utoaji wa mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada.

Aidha, Idara huandaa na kupitia miongozo na viwango vya Elimu ya Ualimu, na kufuatilia uendeshaji na utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya Elimu ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada hutolewa katika Vyuo vya Ualimu 34 vya Serikali na 82 visivyo vya Serikali vyenye uwezo wa kudahili jumla ya wanachuo 47,898 kwa wakati mmoja. Aidha, idadi ya wanachuo katika Vyuo vya Ualimu iliongezeka kutoka 37,698 (wa kike 17,313) katika mwaka wa masomo 2011, hadi 43,258 (wa kike 18,898) katika mwaka wa masomo 2012. Idadi

hii inajumuisha walimu 188 waliohitimu mafunzo ya Elimu Maalum.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuinua ubora wa utoaji wa elimu nchini, wizara yangu kwa ushirikiano na Serikali ya Uswidi kupitia shirika lake la maendeleo la Sida, iliendelea kutekeleza mradi wa kufundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na English kwa kutumia TEHAMA katika shule 21 kwenye Halmashauri 9.

Aidha Vyuo 7 vya Ualimu vya Serikali viliteuliwa kulea (*mentor*) shule hizi kwa kutoa mafunzo kwa walimu kuhusu matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza, pamoja na mafunzo ya matengenezo madogomadogo ya vifaa vya TEHAMA. Mradi huu, ambao ni wa majaribio, utadumu kwa muda wa miaka 2 kuanzia Julai, 2011 hadi Juni, 2013.

Katika mwaka 2011/2012, utekelezaji wa mradi huu ulihusisha kubaini na kuandaa maudhui ya masomo katika hali ya kielektroniki, kugawa vifaa vya TEHAMA (kompyuta pakato *(laptop*) 5; projekta 2 na skrini 2) kwa kila shule; kuwajengea uwezo wa kufundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na *English* kwa kutumia TEHAMA walimu 210, na kuwaelekeza walimu 21 namna ya kufanya matengenezo madogo-madogo ya vifaa vya TEHAMA. Ili kuimarisha utekelezaji wa mradi huu, moduli 3 zimeandaliwa kwa ajili ya mafunzo ya matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia, ambazo ni: ‘Mafunzo ya Msingi ya Kutumia Vifaa vya TEHAMA Kufundishia’; ‘Mafunzo ya Jinsi ya Kutumia TEHAMA Kufundishia (*pedagogy*)’ na ‘Mafunzo ya Matengenezo ya Vifaa vya TEHAMA’. Aidha, maandiko

ya ‘Mwongozo wa Kutathmini Maudhui ya Masomo Yaliyoandaliwa Ki-elektroniki’ na ‘Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini’ yaliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba kumbukumbu za watumishi zinatunzwa ipasavyo Wizara imeandaa mfumo wa kielektroniki utakaotumika katika kutunza kumbukumbu za watumishi, wanachuo na mali za vyuo katika Vyuo vya Ualimu (*Teacher Education Staff and Students Inventory System – TESSIS*). Aidha, wakufunzi 34 (mkufunzi mmoja kutoka katika kila chuo cha Serikali) walipewa mafunzo ya kuwawezesha kutekeleza matumizi ya mfumo huu mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Idara ya Elimu ya Ualimu, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliendesha mafunzo ya ualimu kwa wanachuo 25,677 wa ngazi ya Cheti, na 13,416 wa ngazi ya Stashahada.

(b) Iliendesha mafunzo kazini kwa ajili ya walimu 2,052 katika ngazi ya shule katika Halmashauri saba za majaribio ambazo ni: Magu, Makete, Mtwara, Bagamoyo, Hai, Siha na Temeke, kupitia ‘Mkakati wa Mafunzo ya Walimu Kazini Elimu ya Msingi’ (MWAKEM) ngazi ya shule.

(c) Iliendesha mafunzo kuhusu ufundishaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati na English kwa kutumia TEHAMA, kwa wakufunzi 72, walimu wa Shule za Sekondari 210 na waratibu 8 wa ngazi ya kitaifa.

(d) Ilitoa mafunzo kuhusu matumizi ya ‘*Moodle*’ katika kufundisha na kujifunza kwa wakufunzi 204 wa vyuo vya Ualimu. *Moodle* ni mfumo ambao huwawezesha wanafunzi na wakufunzi kupata taarifa za kielimu kutoka kwenye mtandao kwa wakati wao (*Online Learning Management System*). Mfumo huu hutumika kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia intaneti.

(e) Ilisimamia na kuimarisha ufundishaji wa michezo katika Vyuo vya Ualimu 12 vya Serikali kwa kutoa Mafunzo ya Elimu ya Afya kwa wakufunzi 30 wanaofundisha Elimu kwa Michezo katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali.

(f) Iliendelea kuratibu utoaji wa mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti (Michezo) katika vyuo vya ualimu 12, kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la *Liike* la Finland.

(g) Ilitoa mafunzo ya ‘Usimamizi na Uendeshaji Fanisi wa Mtaala’ kwa Wakuu wa Vyuo vya Ualimu 34 vya Serikali ili kuimarisha uwezo wao katika usimamizi wa mafunzo ya ualimu.

(h) Iligharimia sehemu ya mafunzo kwa ajili ya wakufunzi 109 (Shahada ya Kwanza – 22, Uzamili -85 na uUzamivu - 2) katika vyuo vikuu mbalimbali.

(i) Ilifanikiwa kukarabati miundombinu ya Vyuo vya Ualimu vya Kitangali, Bustani na shule ya Msingi ya

Mazoezi Buhemba iliyo chini ya Chuo cha Ualimu Tarime.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Moja ya majukumu ya Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ni kuleta msukumo katika juhudi za Serikali za kukabiliana na ongezeko la watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Aidha, idara ina wajibu wa kutoa fursa ya kujiendeleza kielimu nje ya mfumo rasmi wa shule miongoni mwa vijana na watu wazima, na kusimamia vituo vya magazeti ya elimu katika Kanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliandaa na kusambaza nakala 10,500 za magazeti matano (5) katika Kanda za kisomo za Kusini (Songea), Magharibi (Tabora), Ziwa (Mwanza), Kaskazini (Moshi) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya).

(b) Ilifanya ufuatiliaji wa mpango wa ‘Ndiyo Ninaweza’ wa kufuta ujinga wa kutojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) katika Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ambayo ni kati ya Halmashauri 9 zilizo chini ya mpango huo.

(c) Ilifanya maandalizi ya awali ya utafiti kuhusu kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu katika Halmashauri za mikoa 19 nchini kwa kushirikiana na *UNESCO.*

(d) Iliratibu uandaaji wa mfumo unaoainisha sifa na viwango vya wahitimu wa Mipango ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi *(EWW na ENMRA).*

(e) Ilikamilisha maandalizi ya 'Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi' ambao uliidhinishwa na Serikali kwa utekelezaji kupitia Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu.

(f) Ilikamilisha maandalizi ya 'Mpango Mkakati wa Elimu juu ya Haki za Binadamu' ambao uliidhinishwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji kupitia Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu.

(g) Iliandaa vifaa vya kutolea mafunzo ya walimu wa mpango wa 'Ndiyo Ninaweza' ambavyo ni kadi za maneno, kadi za maendeleo ya mwanakisomo na kitabu cha mazoezi ya ziada.

(h) Ilikusanya takwimu za awali za vituo vya utoaji wa *EWW-ENMRA* na kuandaa zana za kukusanyia taarifa, na kuunda timu ya kitaalamu ya kufanikisha kazi ya kufanya utafiti wa maendeleo ya kisomo nchini.

(i) Iliandaa hadidu za rejea pamoja na zana za kukusanyia taarifa kwa ajili ya tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Elimu kwa Wote, kwa kushirikiana na *UNESCO.*

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya

Ufundi Stadi ina majukumu ya kubuni, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Aidha, Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, huhakikisha kuwa elimu na mafunzo yanayotolewa inazingatia ubora kulingana na mahitaji ya soko la ushindani, na kutolewa kwa walengwa wenye sifa stahiki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Iliratibu utoaji wa mafunzo ngazi ya pili kuhusu *Competence- Based Education and Training (CBET) Best Practices* kwa maofisa 30 kutoka Wizara na Taasisi zinazoshiriki katika mradi wa *Education for Employment* na mafunzo ngazi ya pili kuhusu Tathmini ya Soko la Ajira. Aidha, ilifanikisha uendeshaji wa Kongamano la kitaifa la wadau kuhusu namna ya kujirekebisha kulingana na mabadiliko yanayotokea duniani. *(Makofi)*

(b) Ilikamilisha ripoti ya uchambuzi wa hali halisi ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini ikiwa ni hatua za mwanzo za maandalizi ya ‘Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi’ (MMEU).

(c) Iliimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kuendesha vikao viwili

vya kiutendaji na viwili katika ngazi ya Mawaziri wa Wizara zinazoshiriki katika Mradi wa *Education for Employment (EFE)* vilivyofanyika Agosti na Novemba 2011 ili kuimarisha utekelezaji wa mradi wa *'EFE'.* Aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano iliwasilisha kwa Serikali ya Canada, ombi la kuwa na awamu ya pili ya mradi wa *EFE.*

(d) Iliandaa rasimu ya mpango wa uanzishaji wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya wilaya unaojumuisha ujenzi wa vyuo vipya na kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii katika kutoa mafunzo ya ufundi stadi.

(e) Iliratibu ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi katika mikoa ya Lindi, Manyara, Pwani na Kituo cha TEHAMA cha Dar es Salaam.

(f) Iliendelea na ujenzi wa Chuo cha Wilaya cha Makete ambacho kimekamilika kwa asilimia 98.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu. Idara ya Elimu ya Juu ina majukumu ya kusimamia na kutathmini sera, sheria, taratibu na miongozo ya utoaji wa Elimu ya Juu. Aidha, Idara ya Elimu ya Juu, kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mamlaka ya Elimu Tanzania na Vyuo vya Elimu ya Juu, inahakikisha kuwa elimu inayotolewa inazingatia ubora kulingana na mahitaji ya soko la ushindani, na inawafikia walengwa wenye sifa stahiki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Elimu ya Juu ilitolewa katika vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki 46 (vya Serikali 14). Kazi za msingi zinazofanywa na Vyuo Vikuu ni kufundisha na kufanya utafiti unaolenga katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini, na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na umma kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udahili katika Vyuo vya Elimu ya Juu uliongezeka kutoka wanafunzi 139,638 (wa kike 49,959) mwaka 2010/2011, hadi 166,484 (wa kike 60,592) mwaka 2011/2012 kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 4. Ongezeko hili ni matokeo ya mafanikio ya utekelezaji wa MMES I – II iliyoongeza uandikishaji katika shule za sekondari zilizojengwa chini ya mpango huu, na kuajiri walimu wa kutosha waliowawezesha wanafunzi wengi zaidi kufanya vizuri katika mitihani ya Elimu ya Sekondari ya Kawaida na kuchaguliwa kuendelea na Elimu ya Sekondari ya Juu; na kisha kuhitimu wakiwa na sifa za kujiunga na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara, kupitia Idara ya Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iligharimia mafunzo ya madaktari wanafunzi 1,900 kwa kutoa fedha ya posho ya vitabu na viandikia, mahitaji maalum ya vitivo na ada.

(b) Ilidhamini wanafunzi 47 raia wa Uganda katika Vyuo Vikuu vya Tanzania kama ifuatavyo: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (26); Chuo Kikuu cha Afya na

Sayansi Shirikishi Muhimbili (11), na Chuo Kikuu Ardhi (10). Aidha, ilidhamini Watanzania 37 wanaosoma katika Vyuo Vikuu mbalimbali nchini Msumbiji na Uganda chini ya utaratibu wa kubadilishana wanafunzi kati ya Tanzania na Uganda; na Tanzania na Msumbiji.

(c) Ilidhamini wanafunzi watano (5) raia wa China katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam kwa ajili ya kozi ya Kiswahili ya mwaka mmoja chini ya Mkataba wa Ushirikiano kati ya Tanzania na China.

(d) Iligharimia mahitaji maalumu kwa ajili ya wanafunzi 24 katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu ya Ushirika na Biashara Moshi katika maeneo yafuatayo:-

Mafuta ya ngozi kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi; vifaa kwa ajili ya wasioona; shimesikio (*hearing aids*) kwa wenye ulemavu wa kusikia, na visaidizi kwa wenye ulemavu wa viungo.

(e) Ilitoa elimu kwa umma kuhusu dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi kupitia maonesho ya Taasisi za Elimu ya Juu.

(f) Iliratibu udhamini wa wanafunzi 161 uliofanywa na nchi mbalimbali ambapo wanafunzi 156 walichaguliwa kama ifuatavyo:- Algeria (61), China (72), Cuba (4), Korea ya Kusini (1), Urusi (9), Uingereza (4) na Sebia (5).

(g) Iligharimia mafunzo ya Wahadhiri 31 walioko Ujerumani chini ya uratibu wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kupitia mpango wa *DAAD.*

(h) Ilifanya utafiti wa gharama halisi za kugharimia Elimu ya Juu na kutoa rasimu ya kwanza ya taarifa ambayo ilipitiwa na jukwaa la kudhibiti ubora wa elimu ya juu na maoni yao kuwasilishwa kwa mtaalamu mwelekezi ambaye anaendelea kuyajumuisha katika ripoti yake ya mwisho.

(i) Ilifanya utafiti kuhusu njia mbadala ya kugharimia Elimu ya Juu. Rasimu ya kwanza ya ripoti iliwasilishwa mwezi Aprili, 2012.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Shule. Idara ya Ukaguzi wa Shule ina majukumu ya kuhakikisha kuwa sera, sheria, kanuni na viwango vya utoaji elimu vilivyowekwa vinatekelezwa kwa ufanisi katika ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, vitengo vya elimu maalum, vituo vya ufundi stadi, Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya Mfumo Rasmi, na Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Idara ya Ukaguzi wa Shule, ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) ilifanya ukaguzi katika asasi 6,228 kati ya 20,045 zilizolengwa.

(b) Iliendesha Mtihani wa Kidato cha 2 wa mwaka 2011, ambapo jumla ya watahiniwa 418,974 (Wasichana 193,331) walifanya mtihaniambapo watahiniwa 190,259 (asilimia 45.4) walifaulu. Kati ya hao, wasichana walikuwa 77,388, ambayo ni asilimia 40 ya watahiniwa wote.

(c) Iliandaa rasimu ya andiko kuhusu mchakato wa kuifanya Idara ya Ukaguzi kuwa wakala ili kuongeza ufanisi katika kudhibiti ubora wa utoaji wa elimu. Rasimu hiyo ilisambazwa kwa wadau ili kupata maoni.

(d) Ilifanya tathmini ya kiwango cha ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha 2 katika mwaka 2011 ambapo ufaulu ulionekana kuwa wa kiwango cha chini katika masomo ya Sayansi kama ifuatavyo: Basic Mathematics (12.5%); Physics (27.4%), Chemistry (34.0%) na Biology (36.1%).

Mheshimiwa Spika, Sera na Mipango. Idara ya Sera na Mipango ina majukumu ya kutoa utaalamu na huduma katika uandaaji, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo, na uratibu wa maandalizi ya ‘Mpango Mkakati wa Muda wa Kati wa Wizara’, na ‘Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Fedha’ pamoja na uandaaji wa Mpango wa Utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Idara ya Sera na Mipango, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilikamilisha ukusanyaji na uchambuzi wa maoni ya wadau mbalimbali wakiwemo waheshimiwa wabunge kuhusu rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo na kuanza kuandaa mkakati wa utekelezaji wake.

(b) Iliendesha mafunzo ya uingizaji data katika hazinadata (*database*) kwa maafisa wa elimu 40, wakiwemo Maafisa Taaluma wa Mikoa na Halmashauri, na Maafisa Vifaa na Takwimu. Aidha, ununuzi wa seti za kompyuta kwa ajili ya Halmashauri 40 ulifanyika.

(c) Ilitoa mafunzo ya 'Wawezeshaji wa Wawezeshaji' (*Trainers of Trainers – TOT*) 20, Maafisa Elimu wa Mikoa 21, Maafisa Elimu Taaluma wa Mikoa 21, Maafisa Elimu wa Sekondari kutoka Halmashauri 132 na Waingiza data wa Halmashauri 132 kuhusu usimikaji na matumizi ya mfumo wa kuingiza taarifa za wanafunzi wa Kidato cha 4 kwenye Fomu za Uchaguzi (*Selection Forms - SEL Forms*).

Aidha, ilifanya usimikaji wa mfumo wa uchaguzi wa wanafunzi wa Kidato cha 5 kwa kila Halmashauri. Matumizi ya mfumo huu yamepunguza gharama za uendeshaji kwa kuwa na idadi ya washiriki wachache zaidi kwa asilimia 27.7 na siku za kazi chache zaidi kwa asilimia 17.1.

(d) Iliratibu mkutano wa pamoja wa mapitio ya Sekta ya Elimu kwa mwaka, 2011.

(e) Ilifanya mapitio ya michoro pamoja na miongozo ya ujenzi na ukarabati wa shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

(f) Ilisanifu na kusimamia ujenzi wa shule mpya ya bweni ya Sekondari ya Miono yenye Kidato cha 5 na 6, mchepuo wa Sayansi, itakayokuwa na uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 800, wakiwemo wasichana 400.

(g) Ilifanya tathmini ya hali halisi ya shule za Sekondari 264 (Shule 2 kila Halmashauri) ili kubaini mahitaji ya ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu, na kuandaa hati za zabuni kwa ajili ya kazi hiyo.

(h) Ilifanya mapitio ya 'Mpango Mkakati wa Muda wa Kati' – 2010/2011 – 2012/2013 wa Wizara ili uendane na 'Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano'wa 2011/2012 – 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu. Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu inasimamia masuala ya utawala, ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi pamoja na sheria, kanuni na taratibu za utumishi. Aidha, inaratibu 'Programu ya Kuboresha Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma'.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliajiri watumishi 224, iliidhinisha vibali vya ajira za watalaam wa kigeni 362; iliratibu upandishaji vyeo kwa watumishi 441 na kuthibitisha kazini watumishi 41.

(b) Ilitayarisha muundo wa Utumishi wa Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu na kuuwasilisha katika Baraza Kuu la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma ambalo liliidhinisha muundo unatekelezwa kwa sasa.

(c) Ilianza kutumia mfumo wa kielektroniki wa LAWSON kwa ajili ya kuhifadhi na kuimarisha taarifa za kiutumishi.

(d) Ilikamilisha Mpango wa Urithishaji wa Madaraka (*Succession Plan*) katika ngazi ya makao makuu ya Wizara (Idara na Vitengo), na kuuwasilisha Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara ianaendelea na zoezi hili katika taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Mawasiliano ya Serikali. Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kina majukumu ya kuratibu na kuandaa utoaji wa habari za Sekta ya Elimu kwa wananchi kupitia kwenye vyombo vya habari. Aidha, kinashirikiana na wadau wengine wa Sekta ya Elimu katika kuhamasisha wananchi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) ilitoa taarifa za maendeleo ya Sekta ya Elimu kwa umma kupitia redio, televisheni na magazeti, pamoja na mikutano 10 ya waandishi wa habari na watendaji wakuu wa Wizara.

(b) ilitoa ufafanuzi wa maswali 19 yalioulizwa na wadau kupitia tovuti ya wananchi *(www.wananchi.go.tz)*.

(c) Iliandaa na kutangaza vipindi 6 vya redio na 19 vya televisheni.

(d) iliandaa na kuchapisha makala 6 kwenye magazeti.

(e) Iliratibu ushiriki wa Wizara katika maadhimisho ya miaka 50 ya uhuru.

(f) Ilichapa na kusambaza nakala 1,500 za jarida la *Ed. -SDP.*

Mheshimiwa Spika, Wakala, Taasisi na Mabaraza ya Wizara. Wakala, Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yana wajibu wa kusimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini. Mwaka 2010/2011, kila Wakala, Baraza na Taasisi zilitekeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ina jukumu la kutoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na elimu ya kujiendeleza nje ya mfumo rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi kwa kutumia mtaala wa *Competence-Based Education & Training (CBET)* kwa wanafunzi 89 wa Cheti, 272 wa Stashahada, na 88 wa Shahada.

(b) Iliandaa mitaala ya masomo ya kufundishia (*Pedagogical Content Knowledge Subjects*) masomo ya Elimu ya Sekondari na kufanya mapitio ya hatua ya kwanza ya mitaala ya masomo mengine.

(c) Ilifanya tathmini na kuainisha maeneo yanayohitaji mafunzo.

(d) Ilichapisha nakala 500 za *Journal of Adult Education* No. 19 na nyingine 500 za *Studies in Adult Education No. 67.*

(e) Ilifunga mtambo mdogo wa kuunganisha mtandao (*Cyber roam server*) katika ofisi za makao makuu ya Taasisi kwa ajili ya kuunganisha makao makuu ya Taasisi na vituo vitano katika mtandao wa mawasiliano ya kompyuta ili kuinua ubora wa utoaji wa Elimu Masafa.

(f) Iliratibu mkutano wa 46 wa Elimu Masafa katika nchi za *SADC* uliofanyika Dar es Salaam – Tanzania.

(g) Iliandaa ‘Rasimu ya Mtaala wa Hatua ya III’ (Kidato cha 5&6) ambayo ilihusisha masomo 11 yanayotoa fursa ya kuwepo kwa tahasusi (*combinations*) 8. Mtaala huo uliandikwa kwa kuzingatia ufundishaji wa kisasa unaolenga katika kumpa mwanafunzi ujuzi badala ya nadharia tu.

(h) Ilifanikisha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi kutoka 49,533 mwaka 2010/2011 hadi 69,533 mwaka 2011/2012 kutokana na kuhamasika kwa jamii (watoto, vijana na watu wazima wakiwemo wafanyabiashara, wakulima na wafanyakazi waliomaliza darasa la saba) juu ya umuhimu wa kujiendeleza kupitia mfumo wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana.

(i) Iliratibu mafunzo ya *Diploma* ya Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii kwa njia ya Elimu Masafa kwa wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Kazi hiyo ya uratibu inafanyika kwanza kwa majaribio, ambapo washiriki 34 walijiunga kutoka vyuo vya maendeleo ya wananchi katika Awamu ya Kwanza. Hii ilifanyika kwa kushirikiana na taasisi za *Karibu Tanzania Association (KTA)* na; *Karibu Sweden Association (KSA)*. Aidha, Moduli 22 zimekwishaandikwa na kuanza kutumika. Mafunzo ya Ana kwa Ana yalifanyika mara 4, na washiriki walipewa semina elekezi juu ya kutumia mtandao katika kujifunza.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania. Taasisi ya Elimu Tanzania ina majukumu ya kubuni na kuandaa mitaala na mihtasari ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu Maalum.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilifanya mapitio ya mitaala ili kuinua ubora wa elimu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, ambapo:-

(i) Iliandaa andiko la utafiti kuhusu tathmini ya mitaala ya elimu ya awali na msingi.

(ii) Ilikamilisha uainishaji wa upungufu katika maudhui ya mihtasari ya elimu ya awali na msingi na kuingiza marekebisho yake.

(iii) Ilisanifu mihtasari 20 ya mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti na 28 ya Stashahada.

(iv) Iliandaa zana za utafiti kuhusu mahitaji na maudhui ya mihtasari ya masomo ya kilimo na biashara.

(v) Iliendesha mikutano kumi (10) ya paneli za masomo ya Elimu ya Awali, Jiografia, *History,* Kiswahili, *English, Physics, Chemistry, Biology, Mathematics* na *Theatre Arts* kwa ajili ya shule na vyuo vya ualimu.

(b) Iliendesha warsha ya wadau kuhusu matumizi ya maandiko yanayohusu mitaala kwa shule na Vyuo vya Ualimu.

(c) Ilianzisha mafunzo ya Stashahada ya Uzamili katika Usanifu na Ukuzaji Mitaala kwa njia ya masafa kwa washiriki 48 kutoka ndani na nje ya nchi.

(d) Ilifanya upembuzi yakinifu wa kujenga kituo cha mafunzo ya mitaala na utafiti wa maendeleo ya kielimu.

(e) Ilifanya utafiti kuhusu sababu zinazowafanya watoto kumaliza Darasa la VII na kujiunga na Kidato cha I bila kuwa na stadi za Kusoma na Kuandika na Kuhesabu (KKK). Utafiti huu ulifanyika katika mikoa saba (Mwanza, Mbeya, Ruvuma, Shinyanga, Lindi, Tabora na Mtwara).

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania. Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ina jukumu la kutoa na kusambaza huduma za maktaba nchini. Aidha, ina jukumu la kuanzisha, kuendesha, kuongoza, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma kuanzia ngazi za Vijiji, Wilaya hadi Mikoa, na kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliwezesha kupatikana kwa jumla ya vitabu 93,914. Kati ya hivyo, 523 vilipatikana kwa mujibu wa sheria Na. 6 ya mwaka 1975, inayomtaka kila mchapishaji kuwasilisha Maktaba Kuu, nakala mbili (2) za kila kitabu anachokichapisha; vitabu 90,708

vilipatikana kwa njia ya msaada, na 942 vilinunuliwa na hivyo kufanya idadi ya vitabu vyote katika Maktaba nchini kufikia 1,184,957.

(b) Ilitoa ushauri kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa maktaba katika shule 101, vyuo 29 na Halmashauri za wilaya 11.

(c) Ilishirikiana na Halmashauri za wilaya nne ambazo ni Ruangwa, Chunya, Masasi pamoja na Kibaha katika kuanzisha Maktaba za Umma.

(d) Iliwezesha udahili wa wanafunzi 990 wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka, ambapo ngazi ya Cheti walikuwa 390, Stashahada 450 na wa mafunzo ya awali 150.

(e) Ilianza awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 60.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu. Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu una majukumu makuu manne:-

Kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti katika masuala yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu; na kuandaa na kusambaza makala na vitabu mbalimbali vya uongozi na uendeshaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa wanachuo 561 kati ya wanachuo 600 waliolengwa, na hivyo kutekeleza lengo kwa asilimia 93.5. Wanachuo hao ambao walitoka katika Idara mbalimbali za elimu, walikuwa ni Walimu Wakuu, Waratibu Elimu Kata, Maafisa Elimu ngazi ya Wilaya, walimu wa Shule za Awali, Msingi na Sekondari, wafanyakazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali *(NGOs)* na mameneja na wamiliki wa shule zisizo za serikali.

(b) Iliandaa zana za kufundishia na kutoa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa elimu kwa wawezeshaji wa wawezeshaji kwa ajili ya mafunzo ya Waratibu Elimu Kata.

(c) Ilitoa mafunzo ya uongozi kwa washiriki 100 (Maafisa Elimu Taaluma 50 na Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu 50) kwa ushirikiano na shirika la Kimataifa la Japan *(JICA).*

(d) Ilitoa mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa elimu kwa Maafisa Elimu 130 ngazi ya mikoa na wilaya.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya *UNESCO.* Tume ya Taifa ya *UNESCO* ina majukumu ya kutekeleza programu za *UNESCO* nchini kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara, kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO,* ilitekeleza yafuatayo: -

(a) iliratibu ushiriki wa Serikali katika kikao cha 35 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* uliofanyika Paris.

(b) Iliratibu uanzishwaji wa kikundi cha Wanawake katika Sayansi Tanzania (*STI4W Reference Group*), ili kuweka mkakati wa kuongeza ushiriki wa wanawake katika Sayansi.

(c) Ilisimamia uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Utafiti na Uhifadhi wa Nyaraka za Masuala ya Jinsia kilichopo Tengeru, Arusha.

(d) Iliratibu ushiriki wa vijana katika utekelezaji wa programu za *UNESCO,* kupitia Dawati la Vijana la Tume ya Taifa ya *UNESCO.*

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania. Baraza la Mitihani la Tanzania lina jukumu la kutekeleza sera ya mitihani kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978.

Aidha, Baraza lina jukumu la kuendesha mitihani ya kuhitimu Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada na mtihani wa Maarifa, na kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na bodi za nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka, 2011/2012, Wizara, kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka, 2011 kwa watahiniwa 983,545.

(b) Iliendesha Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2011 kwa watahiniwa 441,426, Mtihani wa Maarifa mwaka 2011 kwa watahiniwa 23,585, Mtihani wa Kidato cha Sita mwaka, 2012 kwa watahiniwa 55,591 na mitihani ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada kwa watahiniwa 21,145.

(c) Ilitoa mafunzo ya matumizi ya katarasi za *Optical Mark Reader (OMR)* katika kujibu Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, kwa Maafisa Elimu na Maafisa Taaluma wa Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara na Waratibu wa Elimu Kata.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Maendeleo Dakawa. Kituo cha Maendeleo Dakawa kina majukumu ya kutunza na kuhifadhi majengo, vifaa na miundombinu iliyokabidhiwa na Chama cha *African National Congress (ANC)* cha Afrika ya Kusini kwa ajili ya kulinda Historia ya Ukombozi wa Kusini mwa Afrika.

Baada ya Serikali ya Tanzania kukabidhiwa Kituo cha Maendeleo Dakawa kutoka kwa Wapigania Uhuru wa *ANC,* Wizara yangu imekusudia kukiendeleza kituo hiki na kukitumia katika kutoa Elimu ya Sayansi na Ufundi kupitia Taasisi zilizopo na zitakazoainishwa hapo baadaye ili kiwe ‘Kitovu cha utoaji wa Elimu ya Sayansi

na Teknolojia' (*Centre of Excellence for Science and Technology*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Kituo cha Maendeleo Dakawa, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilisimamia taasisi zilizomo katika kituo kwa ufanisi kwa kutoa mafunzo na huduma.

(b) Ilianzisha kozi ya TEHAMA kwa ajili ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari na wanachuo wa Ualimu na Ufundi wa Mitambo ya Kilimo (*Agro-mechanics*) katika chuo cha *VETA* kilichoko kituoni. Aidha zaidi ya ekari 50 za mashamba ya kituo yalitumika kwa ajili ya Mafunzo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania. Mamlaka ya Elimu Tanzania ina majukumu ya kutafuta na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharimia maendeleo ya Sekta ya Elimu nchini ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wadau wa elimu kuchangia kwa hiari katika miradi ya elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilifadhili uaandaaji wa Kiongozi cha Kufundishia masomo ya Sayansi katika shule za Sekondari.

(b) Ilizindua harambee ya ujenzi wa mabweni ya wasichana, ambapo jumla ya shilingi milioni 105 zikiwa ni fedha taslimu na ahadi zilizopokelewa.

(c) Ilifadhili jumla ya miradi 101 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 ambapo miradi miwili yenye thamani ya shillingi milioni 200 ni ya shule za Msingi; 92 yenye thamani ya shilingi milioni 695.9 ni ya shule za Sekondari; na miradi 7 yenye thamani ya shilingi milioni 804.1 ni kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu, Ufundi na Vyuo Vikuu.

(d) Ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi 65 kati ya 70 iliyopangwa, ili kuthibitisha ukamilifu na ubora wa miradi iliyofadhiliwa.

(e) Ilitoa mafunzo mbalimbali kwa wafanyakazi 11 ili kuwajengea uwezo na weledi katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina majukumu makuu ya kusimamia ubora wa elimu ya juu, kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa Vyuo Vikuu, na kuidhinisha programu zinazofundishwa, ili zikidhi maendeleo ya Taifa na soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitathmini ubora wa programu 81 za masomo ya Vyuo Vikuu na vyuo vikuu vishiriki nchini kwa lengo la kuziidhinisha.

(b) Iliendesha warsha 7 za kuwajengea viongozi uwezo wa uongozi, kwa kushirikiana na taasisi ya

*Carnegie Corporation of New York* ambapo jumla ya viongozi 106 wa Vyuo Vikuu vya Tanzania walihudhuria. Kati ya hao, viongozi watatu kutoka *State University of Zanzibar (SUZA), Nelson Mandela African Institute of Science and Technology* (NMAIST) na *Hubert Kairuki Memorial University* (HKMU) walitembelea Vyuo Vikuu vya nje kwa lengo la kujifunza mbinu mbalimbali za uongozi na maendeleo ya Vyuo Vikuu.

(c) Ilikamilisha andiko la Mfumo wa Sifa Linganifu za Elimu ya Juu (*University Qualifications Framework*) kwa kushirikiana na *The Netherlands Initiative for Capacity development in Higher Education (NICHE).*

(d) Ilikamilisha rasimu ya kwanza ya ‘Mfumo wa Kitaifa wa Sifa Linganifu’ (*National Qualifications Framework)* na maandalizi ya kanuni za mfumo huo na kuipeleka kwa wadau kwa ajili ya maoni na mapendekezo zaidi.

(e) Ilifanya tathmini ya kitalaamu katika vyuo 16. Kati ya vyuo hivyo, vitatu (3) ni vipya ambavyo ni *St. Joseph University in Tanzania*, *St. Augustine University of Tanzania* – vituo vya Bukoba na Songea na *Stella Maris University College - Mtwara*.

Aidha, vyuo vingine ni *St. John University - Dodoma*, *St. John University* – kituo cha *St. Marks Dar es Salaam,* Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara-Moshi, Chuo Kikuu Kishiriki cha Sebastian Kolowa - Lushoto, *Nelson Mandela African Institute of Science and Technology*- Arusha, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya, Chuo Kikuu cha Arusha,

vituo vya Mbeya na Musoma, Chuo Kikuu cha African United Tanzania, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ualimu na Falsafa cha Don-Bosco Moshi, Skuli Kuu ya Stadi za Afya ya Zanzibar (*Zanzibar School of Health*), Chuo Kikuu cha Bagamoyo, na Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Kampala – Dar es Salaam.

(f) Iliratibu na kutathmini 'Mradi wa Majaribio ya Kudhibiti Ubora wa Programu za Vyuo Vikuu' 5 vinavyotekeleza mradi huu chini ya *Inter University Council for East Africa (IUCEA).* Aidha, ilifanya warsha ya kubadilishana uzoefu uliotokana na utekelezaji wa mradi huu kwa vyuo 26 ili viweze kuanza kutekeleza miongozo ya udhibiti wa ubora kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika vyuo vya mradi huo katika vyuo vitano (5).

(g) Ilichapisha nakala 20,000 za kitabu cha 'Mwongozo wa Udahili' na vipeperushi mbalimbali vinavyoelimisha umma juu ya majukumu ya Tume na kuwaelekeza waombaji jinsi ya kuomba kudahiliwa katika vyuo vya Elimu ya Juu nchini.

(h) I liratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi wapatao 45,598 wa mwaka wa masomo 2011/2012.

(i) Iligharimia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 25, na ya muda mrefu kwa wafanyakazi wanne (4) katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu *(Ph.D.),* ili kukabiliana na changamoto za maendeleo ya Elimu ya Juu kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

(j) Ilikamilisha machapisho ya miongozo mbalimbali ya ubora wa elimu yakiwemo:-

*(i) University Qualifications Framework* (UQF).

*(ii) Tanzania University Level Education - Credit Accumulation and Transfer General Guidelines.*

*(iii) Tanzania University Level Education - Minimum Guidelines for the Harmonisation of Awards Offered in Tanzania.*

*(iv) Tanzania University Level Education - Minimum Standards for Postgraduate Training.*

*(iv) Tanzania University Level Education - Minimum Guidelines and Norms for Governance Units.*

*(v) Tanzania University Level Education - Employment, Staff Performance Review and Career Development Minimum Guidelines*.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lina majukumu ya kusimamia na kuratibu mitaala, ubora wa mafunzo, mitihani, tuzo, usajili na ithibati za Vyuo vya Elimu ya Ufundi vya umma na binafsi nchini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa ithibati kwa vyuo 36 ambapo, vyuo 23 vilipata ithibati kamili na vinne (4) vilipata ithibati ya muda. Aidha, vyuo 9 vilipata Ithibati Andalizi (*Accreditation Candidacy*).

(b) Ilisajili vyuo 55 ambapo, Vyuo 16 vilipata usajili kamili, 36 vilipata usajili wa muda na vitatu (3) vilipata idhini ya kuendelea na matayarisho ya usajili (*Preparatory Registration*).

(c) Ilibaini na kutoa usajili kwa walimu 274, ambapo walimu 129 walipata usajili kamili na 145 walipata usajili wa muda.

(d)Iliidhinisha mitaala 61 ya programu za mafunzo, na kuratibu uendeshaji wa mitihani katika vyuo 30.

(e) Ilifanya ufuatiliaji katika vyuo 10 kwa lengo la kuvielekeza jinsi ya kuimarisha taaluma kwa kutumia vigezo na viwango vya ubora vilivyowekwa na Baraza.

(f) Iliratibu udahili wa wanafunzi wa Shahada na Stashahada katika vyuo 18.

(g) Ilifanya ufuatiliaji katika vyuo 10 ili kuhakiki utekelezaji wa masharti ya ithibati.

(h) Ilitoa mafunzo kwa walimu katika vyuo 16 juu ya kufundisha kwa kutumia mitaala mipya.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ina majukumu ya kutoa mikopo kwa

wanafunzi raia wa Tanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa mikopo kwa ajili ya chakula, malazi, vitabu na viandikia kwa wanafunzi 93,176 wakiwemo wahadhiri 256 wanaosomea Shahada za Uzamili na Uzamivu nchini, na kufanikisha urejeshwaji wa mikopo kutoka kwa wadaiwa 69,143 ambao muda wa kuilipa mikopo yao ulikuwa umefika.

(b) Ilitoa elimu kwa umma kuhusu uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu kupitia programu za redio, televisheni, magazeti, maonesho ya Elimu ya Juu na sherehe za miaka 50 ya uhuru.

(c) Ilisogeza huduma za utoaji wa mikopo karibu na wananchi kwa kuimarisha uendeshaji wa Ofisi ya Kanda ya Dodoma na kufanya maandalizi ya kuanzisha Ofisi za Kanda za Bodi huko Zanzibar.

(d) Iliimarisha uendeshaji wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa wanafunzi wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ina majukumu ya kuratibu, kudhibiti, kugharimia, kutoa na kukuza elimu na mafunzo ya ufundi stadi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, ilitekeleza yafuatayo:

(a) Ilikamilisha andiko la 'Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Ufundi Stadi wa Miaka Mitano' ambao ulipitishwa na Bodi ya Elimu na Mafunzo ya ufundi Stadi.

(b) Ilifanikisha ujenzi wa Kituo cha Makete kwa asilimia 75% ambapo Mheshimiwa Makamu wa Rais aliweka jiwe la msingi.

(c) Iliwajengea uwezo wakufunzi 60 na watumishi waendeshaji 24 katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

(d) Ilitekeleza awamu ya majaribio ya mpango wa mafunzo ya ufundi viwandani uitwao *Skills Development Enhancement Programme (SDEP)* katika makampuni ya: *A to Z Textile Mills Ltd*. – Arusha; *ALAF Ltd. – Dar es Salaam*; *Chemi & Cotex Ind. Ltd. Dar es Salaam*, *TANESCO – Dar es Salaam; Movenpick Royal Palm Hotel – Dar es Salaam*; *Tanga Cement Ltd. – Tanga*; *TPC Ltd. - Moshi*; *Alliance One Tobacco – Morogoro*; *21st Century Textile Mills* – Morogoro, na baadaye kuanza kutekelezwa nchi nzima baada ya kuonyesha mafanikio makubwa na kukubalika na waajiri.

(e) Iliimarisha Vyuo vya Ufundi Stadi baada ya mkakati wa ukarabati wa vyuo husika katika awamu ya kwanza kupitishwa na Menejimenti ya Mamlaka.

(f) Ilianzisha mafunzo ya hoteli na utalii katika '*Chuo cha VETA cha Hoteli na Utalii*' kilichopo Njiro – Arusha, ambapo idadi ya waliojiunga katika ngazi ya Stashahada ni wanafunzi 41.

(g) Ilianzisha mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo vipya ambapo: wanafunzi 76 walidahiliwa katika Chuo cha Lindi, wanafunzi 56 Chuo cha Pwani, wanafunzi 150 Chuo cha TEHAMA Kipawa na wanafunzi 80 Chuo cha Manyara.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili jumla ya wanachuo 15,641 ambapo wanafunzi 13,267 ni wa Shahada ya Kwanza na 2,374 ni wa Shahada za Uzamili na Uzamivu;

(b) Iliendelea kushirikiana na washirika wa maendeleo wafuatao katika nyanja za mafunzo, utafiti na ujenzi wa miundombinu: Sida - Serikali ya Kifalme ya Uswidi, *NORAD* - Serikali ya Norway, Benki ya Dunia,

*Goldman Sachs* na mashirika mengine kama *Mc Arthur Foundation;*

(c) Ilikamilisha maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya kufundishia kwa ushirikiano na Benki ya Dunia na kuanza rasmi ujenzi Februari 2012;

(d) Iliendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza katika Taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tawi la Zanzibar, eneo la Buyu;

(e) Ilianzisha Shahada za Kwanza za *B.Sc in Textile Engineering*, na *B.Sc. in Textile Design and Technology;*

(f) Iligharimia mafunzo ya wahadhiri 90 kupitia mradi wa Benki ya Dunia;

(g) Iliadhimisha miaka 50 ya kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo tuzo mbalimbali zilitolewa kwa baadhi ya wanachuo wa zamani wakiwemo Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Yoweri Kaguta Museveni, Jaji Mstaafu Julie Manning, Chief Patrick Kunambi na Makamu Mkuu wa Chuo wa Kwanza - Prof. Cranford Pratt;

(h) Ilifanya utafiti katika maeneo yafuatayo:-

(i) Athari za mabadiliko ya tabianchi na tahafifu nchini Tanzania kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu vya Sokoine na Ardhi;

(ii) Sayansi ya Bahari (*Marine Science*);

(iii) Nishati Endelevu (*Renewable Energy*);

(iv) Uimarishaji wa lugha za Tanzania (*Empowering the languages of Tanzania*); na

(i)Ilitoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kiwango cha tetemeko la ardhi katika bwawa la Kihansi (Seismicity Level around Kihansi Dam);

(ii) Mradi wa umeme kwenye mto Rusumo (Regional Rusumo Falls Haydroelectric and Multipurpose Project);

(iii) Mradi wa kuvuna magadi kutoka ziwa Natron *(The hydrology hydrodymnamics and chemistry of Lake Natron, and its ecological functions and related issues);*

(iv) Tathmini ya mpango wa Angaza Zaidi *(Mid-term Evaluation of Angaza Zaidi Programme)* kwa kushirikiana na *AMREF;* na

(j) Ilichangisha shilingi bilioni 1.07 kwa ajili ya Kituo cha Wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam. Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo hiki kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili wanafunzi wapya 161 wa masomo ya Sayansi na 1,007 wa masomo ya Sanaa na Sayansi ya Jamii, na kufanya jumla ya wanafunzi wote waliodahiliwa kwa mwaka wa masomo 2011/2012 kuwa 1,168.

(b) Iligharimia mafunzo ya wahadhiri 38 katika Shahada za Uzamili na 61 katika Shahada za Uzamivu ndani na nje ya nchi. Aidha, wahadhiri 23 wamemaliza mafunzo (Shahada ya Uzamivu - 4, Shahada za Uzamili - 17 na Stashahada - 2).

(c) Iliajiri wafanyakazi 44 (walimu 23 na waendeshaji 21).

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, ambacho ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, ilitekeleza yafuatayo:

(a) ilidahili wanafunzi 780, kati yao 184 ni wa fani ya Sayansi.

(b) Ilikamilisha upanuzi wa jengo la maktaba ya Chuo lililokabidhiwa rasmi tarehe 28 Januari 2012. Aidha, kiliendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara, kilikarabati vyumba vya madarasa pamoja na ofisi za wafanyakazi.

(c) Iligharimia masomo ya wahadhiri 33 (21 ngazi ya Uzamili na 12 ngazi ya uzamivu).

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za kilimo, mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara, kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili jumla ya wanafunzi 7,228 (Shahada ya Kwanza 6,828, Shahada za Uzamili na Uzamivu 400).

b) Ilikamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250 kwa wakati moja.

(c) Ilianzisha Shahada sita za uzamili na Stashahada moja.

(d) Ilijenga bwawa la uvunaji maji ya mvua kwa kukinga maji katika mteremko, kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

(e) Iliendeleza miradi 130 ya utafiti kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kama ifuatavyo:-

(i) Programu ya kuimarisha maisha ya watu kupitia mabadiliko ya kilimo na maliasili (*Programme for Agriculturre and Natural Resources Transformation for Improved livelihood*).

(ii) Kuimarisha ubunifu katika maliasili na mlolongo wa thamani ya mazao ili kuwainua wakulima wadogowadogo (*Enhancing pro-poor Innovation in Natural Resources and Agricultural Value Chains*).

(iii) Kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi (*Climate change Impacts, Adaptation and Mitigation*).

(iv) Kuimarisha upimaji, utoaji taarifa na kuhakiki misitu Tanzania kwa njia ya teknolojia ya hali ya juu ihusuyo ung'amuzi na utambuzi kwa mbali *(Monitoring, Reporting, and verification of Forests in Tanzania through use of Advanced Remote Sensing Technologies – MRV).*

(v) Utafutaji wa mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yenye ikolojia tofauti katika milima ya Uluguru – Morogoro, ili kuimarisha uwezo wa jamii zilizo katika nyanda za juu za milima ya Uluguru katika kukabiliana na mabadiliko hayo, kupitia shughuli fungamani na endelevu za kijamii.

(vi) Iliandaa na kurusha programu kumi (10) za ushauri wa kitaalamu nchini kupitia Redio Ulanga, Redio Boma - Hai, Redio Kilosa na Redio Ruangwa, sambamba na vipindi vya televisheni kupitia televisheni za Masasi, Mpwapwa na Tanga. Utaalamu huo ulihusu ukulima wa kisasa wa migomba, unenepeshaji wa ng'ombe wa asili, malisho ya ng'ombe wa maziwa, ufugaji wa samaki mabwawani, ufugaji wa nyuki kwa njia za kisasa, kilimo cha umwagiliaji, kilimo bora cha nyanya, mihogo na bidhaa zake, ufugaji bora wa kuku wa asili, na uhifadhi wa mazingira kwa njia za asili. Vipindi hivi hurushwa pia na Televisheni ya Chuo *(SUATV).*

(vii) Matumizi bora ya udongo na maji katika kilimo, uzalishaji wa mbegu bora za maharage, mpunga, na mazao mengine, na matumizi ya teknolojia za baiolojia katika kuzalisha mbegu bora za ndizi na matunda mengine.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara cha Moshi. Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara ambacho ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kina majukumu ya kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za ushirika, maendeleo ya jamii, biashara, oganaizesheni, ujasiriamali na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara, kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Elimu ya Biashara Moshi, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) iliongeza udahili kutoka wanafunzi 3,638 (wanawake 1,482) mwaka 2010/2011 hadi 4,211 mwaka 2011/2012 (wanawake ni 1,869). Aidha, ilianzisha programu mpya za cheti katika kituo cha Mwanza, Stashahada katika Kampasi ya Kizumbi - Shinyanga na programu mbili mpya za Shahada ya Kwanza na programu za Shahada ya Uzamili na Uzamivu katika Kampasi ya Moshi.

(b) Iliendelea kuwagharimia wahadhiri 23 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu.

(c) Iliratibu uandaaji wa maandiko mawili (2) ya miradi ya utafiti kwa ajili ya ufadhili toka nje na kupitia mpango wake wa *Small Scale Competitive Research Grant* ambapo utafiti katika maeneo matano ulifadhiliwa na Chuo. Aidha, ilichapisha Jarida la 'Ushirika na Biashara' (*Journal of Co-operative and Business Studies-JCBS*) na Jarida maalum kwa ajili ya mfululizo wa taarifa za utafiti (*Research Report Series*).

(d) Ilishirikiana na vyuo vya Makerere, Zambia na Malawi kwa ufadhili wa Fredskorpset-FK, Norges Vel, Norway ili kuwezesha ubadilishanaji uzoefu miongoni mwa watafiti wachanga (*Young Research Fellowships*).

(e) Ilifanya kazi mbalimbali za ushauri kwa kushirikiana na vyuo na mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi, kama ifuatavyo:-

(i) Tathmini ya Miradi 11 chini ya '*JPI-Coop AFRICA Challenge Fund*' katika wilaya za Masasi na Mtwara;

(ii) Uanzishaji na usajili wa vyama vya ushirika katika mipango teule iliyo chini ya 'Mradi wa Wazalishaji na Wauzaji Wadogo-wadogo wa Malawi' (*Development and Registration of Co-operatives on selected Schemes covered by the smallholders Crop Production and Marketing Project* (*SCPMP*).

(iii) Tafiti wa *Vertical Integration on Financial Market* chini ya udhamini wa Kituo cha Ushirika cha Uswidi (*Swedish Cooperative Centre - SCC*).

(iv) Uanzishaji na usajili wa vyama vya ushirika katika mipango teule iliyo chini ya 'Mradi wa Wazalishaji na Wauzaji Wadodo wadogo wa Malawi' chini ya udhamini wa *MASDAR (UK)* na *UK Coop College.*

(v) Utoaji wa mafunzo ya Wakufunzi wa Ushirika wa Wilaya yaliyofanyika Afrika ya Kusini chini ya udhamini wa Serikali ya Afrika ya Kusini.

(f) Iliimarisha mipango ya uenezi wa elimu nje ya Chuo ili kuchochea ari ya maendeleo katika jamii kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Ilifanya maonesho mbalimbali ya ushirika ili kueneza elimu ya ushirika kwa jamii;

(ii) Ilitoa mafunzo ya elimu ya ushirika kwa wadau ambapo jumla ya washiriki 5,509 (wanawake 1,946) walihudhuria;

(iii) Iliendesha kozi maalum za muda mfupi katika maeneo ya utunzaji wa vitabu vya uhasibu, ujasiriamali na menejimenti bora ya ushirika. Aidha, kilitoa elimu ya ushirika kwa wadau mbalimbali kupitia vipindi vya redio;

(iv) Iliendesha semina na warsha mbalimbali kwa ajili ya wafanyakazi na wanafunzi kwa kushirikisha wataalamu kutoka nje ya Chuo na asasi zinazoshughulika na masuala mtambuka. Aidha, majarida na vifaa mbalimbali vya kujikinga (*protective gear*) vilinunuliwa katika kutekeleza sera za UKIMWI; na

(v) Ilijenga na kukarabati majengo ya Chuo kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kina majukumu ya kutoa Elimu ya Juu kwa njia ya Masafa na Ana kwa Ana; kutafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kueneza maarifa kupitia vituo vyake vilivyopo mikoani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliongeza udahili wa wanafunzi wa Shahada ya Kwanza kutoka 2,358 mwaka 2010/2011 hadi kufikia 3,749 mwaka 2011/2012 ambayo ni asilimia 94.6 ya lengo la wanafunzi 3,961 kwa mwaka.

(b)Ililifanikisha udahili wa wanafunzi wa Shahada za Uzamili na Uzamivu hadi kufikia wanafunzi 2,079 ambayo ni asilimia 81.9 ya lengo la wanafunzi 2,538 kwa mwaka.

(c) Ilijenga viwanja vya michezo katika eneo la makao makuu ya chuo huko Bungo – Kibaha.

(d) Ilifanya utafiti katika maeneo yafuatayo:-

(i) Usalama wa matumizi ya TEHAMA (*ICT Security*);

(ii) Matumizi ya Simu za Mikononi katika masomo;

(iii) Matumizi ya matingatinga katika kusafisha majitaka (*Constructed Wetlands*) pamoja na mabwawa ya majitaka (*Waste Stabilization Ponds*).

(iv) Namna ya kuongeza ufanisi wa kukusanya na kuzitupa au kuzihifadhi taka mbalimbali mijini.

(v) Matumizi ya ardhi na maji ya Ziwa Victoria.

(e) Iliandaa mitaala kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ualimu kwa njia ya masafa na Ana-kwa-Ana kwa nchi za *SADC,* kwa ngazi ya Stashahada na Shahada.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Ardhi. Chuo Kikuu Ardhi kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika nyanja mbalimbali zikiwemo za maeneo ya ardhi, nyumba, mazingira na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Chuo Kikuu Ardhi ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilikamilisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa: jengo la mihadhara, ofisi za wahadhiri, jengo la hosteli na nyumba ya Makamu Mkuu wa Chuo.

(b) Iliimarisha seva (*server*) ya Chuo na miundombinu ya habari na mawasiliano na kukamilisha maandalizi kwa ajili ya kuunganisha Chuo na mkongo wa taifa wa habari na mawasiliano.

(c) Mheshimiwa Spika, Chuo kilifanya utafiti katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mikakati asilia na fanisi itakayowezesha nchi yetu kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika usalama wa chakula na afya ya wakulima wadogowadogo nchini Tanzania (*Effective Indigenous Adaptation Strategies on Impact of Climate Change Variability on Food Security and Health of Subsistance Farmers in Tanzania*).

(ii) Matumizi ya teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya kuimarisha usalama wa chakula katika maeneo yenye ukame; kwa kutumia uchunguzi kifani wa Wilaya ya Bahi – Dodoma (*Utilisation of Potential Rain Water Harvesting Technology for Improving Food Security in Dry Areas, the Case of Bahi District in Dodoma*).

(iii) Njia rasmi na zisizo rasmi za upatikanaji wa nyumba za gharama nafuu, kwa kutumia uchunguzi

kifani wa Dar es Salaam - Tanzania (*Formal and Informal Practices for Affordable Urban Housing, the Case Study of Dar es Salaam – Tanzania*).

(d) Ilifanya makadirio ya thamani ya uharibifu wa mali uliotokana na milipuko ya mabomu ya Gongo la Mboto, Dar es Salaam, na kutafuta maeneo mengine ya kuwahamishia wahanga wa milipuko hiyo (*Valuation of damaged properties caused by Gongo la Mboto blast in Dar es Salaam and surveying of new areas for resettling the bomb blasts victims*).

(e) Iliandaa Mpango Mkuu (*Master Plan*) wa kuwatafutia mahali pengine pa kuishi wahanga wa mafuriko yaliyotokea Wilaya ya Kilosa.

(f) Iliandaa taarifa ya Hali ya Majiji chini ya 'Mtandao wa Majiji Tanzania' kwa ajili ya majiji 9 ya Ilala, Kinondoni, Temeke*, DSM City Council,* Zanzibar, Arusha, Mbeya na Mwanza (*The state of the Cities Report under the Tanzania Cities Network - TACINE) for nine cities of Ilala, Kinondoni, Temeke, DSM City Council, Zanzibar, Arusha, Mbeya and Mwanza).*

(g) Iliandaa 'Mpango Mkuu wa Mtumiaji wa Ardhi kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Asha Rose Migiro' iliyoko Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro (*'Landuser Masterplan for the Dr. Asha Rose Migiro Secondary School' located in Mwanga District in Kilimanjaro Region*).

(h) Ilisimamia ujenzi wa nyumba za maaskari Bukoba, Musoma na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kina majukumu ya kufundisha, kutafiti, kutibu na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya tiba na afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2011/2012, Wizara, kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili wanafunzi 429 wa Shahada ya Kwanza, ambayo ni ziada ya asilimia 7 ya wanafunzi wote (400) waliokusudiwa kudahiliwa. Aidha, wanafunzi 245 kati ya 250 (Asilimia 98) waliokusudiwa walidahiliwa kwa Shahada za Uzamili na Uzamivu.

(b) Ilifanya utafiti wa dawa ya malaria ya ALU (Dawa Mseto) katika maeneo ya Nagaga – Masasi Mkoani Mtwara, na Mlandizi mkoani Pwani. Katika utafiti huu iligundulika kwamba uwezo wa dawa ya *ALU* kutibu malaria katika maeneo yote (Nagaga na Mlandizi) ulikuwa zaidi ya asilimia 95. Kwa sasa, Chuo kinaendelea kufanya utafiti ili kujua muda ambao dawa *(ALU)* inatumia kuua vimelea vya malaria *(Malaria Parasites).*

(c) Iliratibu utafiti wa TaMoVac (*Tanzania & Mozambique HIV Vaccine Programme-01*) ambapo washiriki 120 (60 kutoka Dar es Salaam, na 60 kutoka Mbeya) wamepatikana na wako katika hatua mbali mbali za kuendelea na utafiti. Matokeo ya awali yanatarajiwa kutolewa mnamo mwisho wa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Mzumbe. Chuo Kikuu Mzumbe kina majukumu ya kutafuta, kukuza, kuhifadhi na kueneza maarifa na stadi za menejimenti kwa njia ya mafunzo, utafiti na huduma za kiufundi na kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara , kupitia Chuo Kikuu Mzumbe ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliweka samani katika hosteli ya wanafunzi wa kike iliyopewa jina la 'Hosteli ya Mama Maria Nyerere', ambapo wanafunzi 400 wamepewa nafasi za malazi hapo.

(b) Ilikamilisha na kuanza kuyatumia madarasa matatu yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 160 kila moja.

(c) Ilichimba kisima cha maji ambapo inaendelea na utaratibu wa kukiunganisha kwenye mfumo wa maji.

(d) Ilikamilisha utafiti katika maeneo 16 na taarifa zake kuchapishwa. Aidha, kazi za ushauri zilitolewa kwa taasisi 26 na taarifa za ushauri kukubalika na wateja.

(e) Ilichapisha vitabu 26 na vitini 3, na kutoa makala 76 katika majarida mbalimbali, ambapo makala 28 kati ya hizo, zilichapishwa katika majarida ya kimataifa.

(f) Iliajiri wahadhiri 8 na wafanyakazi waendeshaji 6.

(g) Iliwezesha wahadhiri 14 kujiunga na masomo ya uzamivu na wengine 12 walijiunga na masomo ya uzamili. Aidha, wahadhiri 42 walirejea kutoka masomoni. Kati ya hao 6 walikuwa wamehitimu na kufaulu masomo ya uzamivu na 36 masomo ya uzamili.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma. Chuo Kikuu cha Dodoma kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara, kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilikamilisha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa barabara za ndani ambapo kilomita 30 za barabara zilijengwa.

(b) Ilianza ujenzi wa maabara katika vyuo vya Sayansi za Asili na Sayansi za Ardhi.

(c) Iliendelea kutekeleza mpango wa upatikanaji wa maji safi na salama na kuondosha majitaka, kwa kuweka miundombinu husika.

(d) Ilidahili wanafunzi wapya 3,700 wa Shahada ya Kwanza na 412 wa Shahada za Uzamili.

(e)Ilitoa ushauri juu ya kufanya utafiti katika maeneo yanayohusu kilimo, ardhi na matumizi ya rasilimali maji ya Ziwa Victoria.

(f) Ilifanya ukaguzi wa kitaaluma ili kuhuisha mitaala inayotumika katika kufundisha.

(g) Iliendeleza jitihada za kuinua ubora wa maktaba katika kila Chuo (*College*).

(h) Iliendelea kuimarisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

(i) Iliendeleza jitihada za kukuza mahusiano na vyuo vikuu na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kina majukumu ya kuendesha mafunzo katika fani za Sayansi za Jamii kwa kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada; kutoa mafunzo ya uongozi; kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara, kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili wanafunzi wapya 279 wa programu ya Cheti, 534 wa Stashahada na 307 wa Shahada ya Kwanza, na kufanya jumla ya wanafunzi waliodahiliwa kuwa 1,120 (wanawake 686).

(b) Iligharimia mafunzo ya wanataaluma 11 (9 Shahada ya Uzamivu, 2 Shahada ya Uzamili).

(c) Iligharimia mafunzo ya wafanyakazi waendeshaji wawili (Shahada ya Uzamili -1, Shahada ya Kwanza -1).

(d) Ilianza ujenzi wa hostel moja eneo la kivukoni na kukamilisha ujenzi wa jengo moja lenye ghorofa nne eneo la Bububu - Zanzibar, likiwa na madarasa 19 na ofisi za wafanyakazi, na kuanza kutumika rasmi tarehe 09 Januari 2012 kwa kuanza kuendesha programu ya Cheti katika Kazi za Vijana.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi Arusha. Chuo cha Ufundi Arusha kina majukumu ya kutoa elimu na mafunzo ya ufundi katika fani za magari, ujenzi, mitambo, umeme, barabara, sayansi na teknolojia ya maabara, eletroniki na mawasiliano ya anga; kwa kiwango cha Cheti na Stashahada.

Aidha, Chuo hufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo yake ya taaluma na kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia Chuo cha Ufundi Arusha ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili jumla ya wanafunzi 480 wa mwaka wa kwanza (ngazi ya cheti na Stashahada 454 na ngazi ya Shahada - 26).

(b) Iliendesha mafunzo ya wiki 10 kwa wanafunzi waliomaliza mafunzo ya *VETA* ili kuwawezesha kujiunga na mafunzo ya ufundi sanifu.

(c) Ilianzisha programu mbili za ufundi sanifu (NTAs 4-6) katika Ujenzi na Umwagiliaji na Umeme wa Magari na Elektroniki.

(d) Iliajiri wanataaluma 38 na wafanyakazi waendeshaji 11. Mchakato wa kuajiri wanataaluma 11 na wafanyakazi waendeshaji 7 unatekelezwa na Sekretarieti ya ajira.

(e) Illiendesha kozi ya awali ya kujiunga na Chuo kwa wanafunzi wa kike, kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu Tanzania *(TEA),* ambapo jumla ya wanafunzi 68 walijiunga na Chuo.

(f) Iligharimia mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 17 na Mfanyakazi mwendeshaji 1, na mafunzo ya muda mfupi kwa wanataaluma 25.

(g) Ilifanya upanuzi wa ukumbi mmoja na darasa moja ili kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

(h) Ilimalizia ukarabati wa bweni na. 2 la wavulana.

(i) Ilikamilisha hati ya makubaliano na maelewano na *VETA* kuhusu matumizi ya ardhi yenye ukubwa wa ekari 150 iliyoko Oljoro. Ilikamilisha upimaji wa vyanzo

vya maji kutoka chini ya ardhi kwa kushirikiana na 'Ofisi ya Kanda ya Maji ya Bonde la Pangani'.

Aidha, ilikamilisha upimaji ramani na kuanza kusanifu skimu ya umwagiliaji na mashamba-darasa katika eneo hilo kwa kushirikiana na Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Kaskazini.

(j) Iliendelea na ujenzi wa jengo la Uhandisi Umwagiliaji, ambapo:-

(i) Slabu ya ghorofa ya tatu imekamilika, na

(ii) Ujenzi wa nguzo kwa ajili ya kumwaga zege la slabu kwenye ghorofa ya nne unaendelea;

(k) Ilifunga viti na meza 312 zisizohamishika katika madarasa sita (6);

(l) Iliendeleza mikakati ya mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI *(HIV/AIDS)* kwa wanajumuiya ya Chuo, kwa kuadhimisha 'Siku ya Afya *ATC'* mwaka 2011;

(m) Iliendeleza ushirikiano na nchi wahisani, mashirika ya Kimataifa na Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundi vilivyo nchini na vya kimataifa kama ifuatavyo:-

(i) Ushirikiano na Vyuo vya Ufundi barani Afrika chini ya uratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA);*

(ii) Ushirikiano na Chuo cha Camosun cha nchini Kanada kupitia mradi wa *Education for Employment (EFE),* ambapo; wanataaluma tisa (9) walipata mafunzo ya muda mfupi nchini Kanada;

(iii) Ubunifu wa mitaala miwili kwa ushirikiano na wataalamu wa Chuo cha Camosun kama ifuatavyo: Teknolojia ya Uchongaji Mawe na Usonara ambao umeshaidhinishwa na *NACTE* ili kuanza kutumika katika mwaka wa masomo 2012/13; na Teknolojia ya Magari na Mitambo Mikubwa ambao uko katika hatua ya kuhakikiwa na kupelekewa *NACTE* kwa uhakiki; na

(iv) Kutoa mafunzo ya mbinu za kisasa za ufundishaji/ ukufunzi kwa wanataaluma 25 Chuoni;

(n) Ilishiriki katika mradi wa *Technical Education and Labour Market Support Programme* (TELMS) unaofadhiliwa na Serikali ya Italia ambapo:

(i) Wanafunzi wa kike 182 walipata ufadhili wa Sh. 180,000.00 kila mmoja ikiwa ni mchango wa ada ya mwaka.

(ii) Wanafunzi wa kike 6 waliofaulu vizuri zaidi walipewa zawadi za kompyuta pakato (*Laptops*).

(iii) Maadhimisho ya siku ya uhamasishaji wa wanafunzi wa kike ili wajiunge na masomo ya sayansi na teknolojia;

(iv) Wakufunzi walitembelea baadhi ya mikoa ili kuhamasisha wanafunzi wa kike kujiunga na masomo ya sayansi na teknolojia;

(v) Jengo la mahusiano na viwanda liliimarishwa, na kompyuta 12 zilinunuliwa kwa ajili ya kazi hiyo.

(o) Iliendesha mafunzo ya Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji kwa vitendo kwa kushirikiana na wataalamu wa Japani.

Mheshimiwa Spika, Malengo na Bajeti ya Mwaka 2012/2013. Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mipango na bajeti ya elimu ya mwaka 2011/2012, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Kamishna wa Elimu. Katika mwaka 2012/2013, Ofisi ya Kamishna itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa Nyaraka na Miongozo ya Elimu ili kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo, Sheria ya Elimu na Kanuni za Uendeshaji wa Elimu nchini.

(b) Kuratibu shughuli za Taasisi za kitaaluma zilizo chini ya Ofisi ya Kamishna.

(c) Kuratibu shughuli zote za masuala mtambuka (Elimu ya Mazingira, Elimu ya UKIMWI, Jinsia, na Huduma za Ushauri na Unasihi) katika ngazi zote za utoaji wa Elimu na Mafunzo.

(d) Kusajili shule na vyuo vya ualimu na kutoa leseni za kufundisha.

(e) Kufanya uchaguzi wa wanafunzi wenye ulemavu waliofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka 2012 kwa ajili ya kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2013.

(f) Kuinua ubora wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kununua na kusambaza vifaa maalumu vya kufundishia na kujifunzia pamoja na visaidizi kwa watoto wenye ulemavu.

(g) Kufanya utafiti kuhusu shughuli za mradi wa III wa *SACMEQ.*

(h) Kuandaa na kutangaza vipindi 600 vya redio kwa masomo ya Shule za Msingi na vipindi 52 kuhusu mbinu za ufundishaji.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Msingi. Mwaka 2012/2013 Wizara, kupitia Kitengo cha Elimu ya Msingi itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uandikishaji, uendeshaji, upatikanaji na matumizi ya vifaa sahihi vya kufundishia na kujifunzia pamoja na miundombinu rafiki ya shule katika Elimu ya Awali na Msingi.

(b) Kuratibu upangaji wa walimu wapya wa ngazi ya Cheti katika Halmashauri kwa kushirikiana na TAMISEMI.

(c) Kufuatilia uendeshaji wa Mtihani wa Taifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi na kuandaa Mtihani wa Taifa wa Darasa la IV na Ufundi Stadi.

(d) Kuratibu mitihani ya watoto wanaojiunga na Shule ya Msingi ya Arusha inayofundisha kwa lugha ya Kiingereza (*Arusha School*) na kusimamia uchaguzi wao.

(e) Kuandaa na kusambaza vyeti 1,023,000 vya kuhitimu Elimu ya Msingi.

(f) Kukamilisha Andiko la MMEM III, kulisambaza kwa wadau, na kuratibu utekelezaji wake.

(g) Kuchapa na kusambaza miongozo 6 ya Elimu ya Awali, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto.

(h) Kuratibu 'Mpango wa Lishe Shuleni' na kukamilisha 'Mpango wa Kitaifa wa Lishe Shuleni'.

(i) Kuratibu majaribio ya mwongozo wa ufundishaji wa somo la Sayansi kwa vitendo ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo katika Shule za Msingi.

(j) Kutoa mwongozo wa kuimarisha stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu (KKK).

(k) Kutoa mafunzo elekezi ya kisera kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya kuhusu miongozo mbalimbali ya Elimu ya Awali na MMEM III.

(l) Kutoa mafunzo elekezi kwa wasimamizi na waendeshaji wakuu wa Elimu ya Awali na Msingi ngazi ya Mkoa, Wilaya na Kata kuhusu uendeshaji wa Elimu ya Awali.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sekondari. Katika mwaka 2012/13, Wizara, kupitia Kitengo cha Elimu ya Sekondari itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya tathmini ya hali halisi ya miundombinu katika Shule 528 za Sekondari ili kubaini gharama halisi ya ukarabati na ujenzi mpya.

(b) Kutoa mafunzo ya Awamu ya III kwa walimu 2,766 wa masomo ya Hisabati na Sayansi, na walimu 2,640 wa masomo ya lugha.

(c) Kutoa mafunzo ya usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya shule kwa watendaji 264 wa Halmashauri.

(d) Kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya ruzuku katika Halmashauri na shule kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI.

(e) Kuendelea kuwajengea uwezo maafisa 16 wanaosimamia shughuli za MMES.

(f) Kuratibu zoezi la uchaguzi wa wanafunzi watakaoingia Kidato cha 1 na cha 5.

(g) Kufanya tathmini ya matokeo ya Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Sekondari ya Kidato cha 4 na 6.

(h) Kuendesha mafunzo ya walimu wa sayansi kuhusu matumizi ya vivunge vya sayansi (*Macro Science-Kits*) kwa shule 180 chini ya mradi wa *UNESCO.*

(i) Kutoa mafunzo kwa walimu 945 kuhusu kuingiza stadi za TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

(j) Kutengeneza nakala 460,500 za vyeti vya wahitimu wa Kidato cha 4 na 6.

(k) Kupanga walimu wapya wa ngazi ya stashahada na shahada katika Halmashauri kwa kushirikiana na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ualimu. Katika mwaka 2012/2013, Wizara, kupitia Idara ya Elimu ya Ualimu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili jumla ya wanachuo 11,545 wakiwemo 5,770 wa ngazi ya Cheti na 5,775 wa Stashahada, na kufanya jumla ya wanachuo wote katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali kuwa 26,800. Kati ya hao, 180 watasomea namna ya kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum.

(b) Kuendesha mafunzo ya ‘Waelimisha Walimu’ (*Teacher Educators*) kwa wakufunzi 580 wa Vyuo vya Ualimu vya Serikali ili kuwajengea uwezo wa kuendesha mafunzo ya ualimu kwa ufanisi.

(c) Kuanzisha Bodi ya Kitaalamu ya Walimu (*Tanzania Teachers Professional Board*) ili kusimamia na kuratibu taaluma ya ualimu.

(d) Kuendelea kusimamia na kuimarisha michezo katika vyuo 12 vya Ualimu vya Serikali kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la LIIKE la Finland.

(e) Kutoa mafunzo kwa wakufunzi 180 ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA kama mbinu ya kufundishia na kujifunzia.

(f) Kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Mafunzo ya Walimu Kazini – Elimu ya Msingi (MWAKEM), kitaifa.

(g) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu 420 wa Shule za Msingi na Sekondari, pamoja na wakufunzi wanaofundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na English.

(h) Kuanza kutumia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* katika kudhibiti ubora wa elimu ya ualimu.

(i) Kulipia sehemu ya gharama za masomo kwa watumishi 250 wanaosoma Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na 35 wanaosoma Shahada za Uzamili katika vyuo vikuu mbalimbali.

(j) Kuingiza na kutunza kumbukumbu za watumishi, wanachuo na mali za Vyuo vya Ualimu katika mfumo wa kielektroniki (*Teacher Education Staff and Students Inventory System – TESSIS*).

(k) Kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati na English katika shule 21 za mradi kwa kutumia TEHAMA.

(l) Kufanya ufuatiliaji, tathmini na mapitio kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Menejimenti ya Maendeleo ya Walimu.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Katika mwaka 2012/13, Wizara kupitia Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi itafanya yafuatayo:-

(a) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Elimu kwa Wote *(EWO)* kwa kushirikiana na wadau wa elimu.

(b) Kufanya utafiti ili kujua kama maarifa na stadi walizopata walengwa wa programu za Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi *(EWW/ENMRA)* zimewawezesha kushiriki katika shughuli za maendeleo kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni.

(c) Kuzindua 'Mpango Mkakati wa Elimu kuhusu Haki za Binadamu'.

(d) Kufanya ufuatiliaji wa programu za EWW/ENMRA, MEMKWA, MUKEJA, Mambo Elimu na Ndiyo Ninaweza.

(e) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya vijana na watu wazima wenye mahitaji maalumu.

(f) Kuchapa na kusambaza nakala 21,000 za Magazeti Vijijini katika vituo 7 vya kanda ambavyo ni kanda ya Ziwa (Mwanza), Kaskazini (Moshi), Kusini (Songea), Magharibi (Tabora), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kati (Dodoma) na Mashariki (Morogoro).

(g) Kuzindua na kutekeleza Mpango wa 'Ndiyo Ninaweza' katika Halmashauri 9 za majaribio.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Juu. Katika mwaka 2012/13, Wizara kupitia Idara ya Elimu ya Juu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kugharimia mafunzo ya wanafunzi 1,900 (Madaktari wa Binadamu, Meno na Tiba ya Mifugo) kwenye vyuo vikuu vya ndani.

(b) Kudhamini wanafunzi 30 raia wa Uganda wanaosoma kwenye vyuo vikuu hapa nchini na watanzania 87 wanaosoma Msumbiji chini ya utaratibu wa kubadilishana wanafunzi baina ya Tanzania na Uganda, na Tanzania na Msumbiji.

(c) Kuendelea kutekeleza mkataba wa ushirikiano kati ya Tanzania na China kwa kudhamini wanafunzi 10 raia wa China katika vyuo vikuu nchini.

(d) Kuendelea kuelimisha umma kuhusu dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi, kupitia vyombo vya habari na Maonesho ya Taasisi za Elimu ya Juu.

(e) Kugharimia mahitaji maalum ya wanafunzi 100 wenye ulemavu katika vyuo vikuu nchini.

(f) Kudhamini mafunzo ya Shahada za Uzamili kwa wanataaluma 80 katika vyuo vikuu vya Umma.

(g) Kudhamini mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa wahadhiri 41 kupitia mpango wa *DAAD.*

(h) Kuratibu uteuzi wa wanafunzi 190 kwa ajili ya nafasi zinazotolewa na nchi rafiki ambazo ni Algeria, China, Cuba, Urusi, Uingereza, Korea ya Kusini, Uturuki, Misri, India na Sebia.

(i) Kuendelea kutekeleza mradi wa 'Sayansi na Teknolojia katika Elimu ya Juu' hasa katika ujenzi wa kumbi za mihadhara katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam; maabara katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam; na miundombinu ya maji safi na majitaka katika Chuo Kikuu Ardhi.

Aidha, Wizara itaendelea kujenga uwezo wa wanataaluma kwa kuwapa mafunzo wanataaluma 156 katika ngazi ya Uzamili na 142 katika ngazi ya Uzamivu.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara, kupitia Idara ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuratibu ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vinne (4) vya mikoa mipya na vinne (04) vya wilaya.

(b) Kuratibu zoezi la uimarishaji wa vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze pia kutumika katika utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi.

(c) Kuwahamasisha wanafunzi wa kike na wenye ulemavu katika Shule za Sekondari ili wajiunge na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi baada ya kuhitimu Elimu ya Sekondari.

(d) Kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

(e) Kuendelea kuhuisha Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

(f) Kukamilisha ‘Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya ufundi Stadi’ (MMEU).

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Shule. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Idara ya Ukaguzi wa Shule, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kukagua asasi 10,528 za elimu na kutoa ushauri wa kitaaluma na kitaalamu.

(b) kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa shule katika Halmashauri 50 na Kanda 5 za Ukaguzi.

(c) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi 100 wa shule katika masomo ya Sayansi, Hisabati na TEHAMA.

(d) Kuongeza ufanisi katika usimamizi wa elimu kwa kutoa mafunzo kabilishi kwa Walimu Wakuu, Waratibu Elimu Kata na Maafisa Elimu wa Wilaya.

(e) Kukamilisha Andiko kuhusu kuanza kwa mchakato wa kuifanya Idara ya Ukaguzi wa Shule kuwa wakala; na

(f) Kuimarisha mfumo wa mawasiliano na utunzaji wa taarifa za ukaguzi wa shule kwa kutoa mafunzo kabilishi kwa Maafisa Elimu wa Halmashauri na Wakaguzi wa Shule juu ya *Inspectorate Management Information System (IMIS).*

Mheshimiwa Spika, Sera na Mipango. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Idara ya Sera na Mipango, itatekeleza yafuatayo:-

(a) kukamilisha Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na mikakati ya utekelezaji wake.

(b) kutoa semina elekezi kwa wadau mbalimbali juu ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo iliyohuishwa.

(c) kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na usimamizi wa takwimu na taarifa za elimu katika Halmashauri.

(d) kuratibu Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Sekta ya Elimu wa mwaka 2012 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu.

(e) kutoa maelekezo ya kitaalamu kuhusu ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika shule na vyuo vya ualimu.

Mheshimiwa Spika, tengeo la bajeti ya Wizara katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutegemea zaidi fedha za Wahisani. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina uhitaji mkubwa wa kukarabati idadi kubwa ya Vyuo vya Ualimu nchini pamoja na taasisi zingine zinazoendeshwa na Wizara, ambazo majengo yake ni ya muda mrefu. Uzoefu unaonesha kwamba Wizara imekuwa ikipata fedha za maendeleo kwa kiasi kikubwa kutoka kwa wahisani. Mfano kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imepangiwa Sh.bilioni 92 ambazo Sh. bilioni 18 zinatoka katika vyanzo vya ndani na Sh. bilioni 74 zinatoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba Serikali iwezeshe Wizara kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu nchini ikiwemo kukarabati vyuo vya Ualimu kwa kutenga fedha zaidi kutekeleza jukumu hili kutoka vyanzo vya ndani vya nchi.

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo vya ndani vya Wizara. Kamati haikuridhika na kiasi cha mapato kinachokusanywa na Wizara kutoka katika baadhi ya Taasisi za Wizara ikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kimekusanya Sh. bilioni 9.6 kati ya Sh. bilioni 19.8 zilizokuwa zimekadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hal ikadhalika Chuo Kikuu cha Dodoma hakikuwa na makusanyo yoyote kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kwamba ni vyema Serikali kuangalia upya utaratibu wa ukusanyaji mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato nchini ili kuweza kukusanya fedha zitakazosaidia kutoa huduma nchini ikiwemo utoaji elimu bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Kuhudumia Walimu nchini (*Teachers Service Delivery System). M*oja ya mambo yanayosababisha Walimu kutohudumiwa ipasavyo, ni mfumo uliopo wa kuhudumia Walimu. Walimu wanahudumiwa na vyombo zaidi ya kimoja na kusababisha adha nyingi ikiwemo urasimu katika kupanda madaraja, kujiendeleza kimasomo, utekelezaji wa malipo ya haki zao mbalimbali kama

mishahara, fedha za likizo na hata ulipaji wa madeni. Kamati inasisitiza kwamba Serikali iangalie upya Mfumo wa Kuhudumia Walimu haraka iwezekanavyo ili kukabiliana na adha zinazowakabili Walimu nchini.

Mheshimiwa Spika, malipo ya madeni ya Walimu nchini. Pamoja na juhudi kubwa za Serikali kulipa madeni ya Walimu nchini ya takribani Sh. bilioni 52 (Mwaka 2009-2012). Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Taarifa za malipo ya madeni hayo yaliyofanyika ziwekwe wazi kwa Walimu kupitia Halmashauri zao ili kuweza kufuatilia uhalali wa taarifa za malipo hayo;

(ii) Taarifa za madai ambayo yamekataliwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ulipaji pia, ziwafikie wahusika mapema iwezekanavyo ili waweze kukidhi vigezo vinavyohitajika kwa malipo;

(iii) Fedha za utekelezaji wa malipo ya madeni ya Walimu ambazo bado hazijatumika, ziwekwe wazi ili zitumike kulipa madeni hayo mapema iwezekanavyo vigezo vya malipo vitakapokamilika. Hatua hii itapunguza manung'uniko kwa Walimu kuhusu zoezi zima la ulipaji wa Madeni ya Walimu nchini; na

(iv) Watendaji watakaobainika kwa namna moja au nyingine kuhujumu malipo ya madeni ya Walimu wachukuliwe hatua za kisheria mapema iwezekanvyo ikiwemo katika Halmashauri za Wilaya ya Chamwino, Morogoro na Same.

Mheshimiwa Spika, posho kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Uzoefu unaonyesha kwamba idadi kubwa ya wahitimu katika taaluma ya Ualimu wanaopangiwa vituo vya kazi pembezoni mwa nchi hawaripoti katika vituo hivyo tayari kwa kuanza kazi. Hali kadhalika kumekuwepo na idadi kubwa ya Walimu wanaojiendeleza kimasomo, ili kupata nafasi ya kufundisha shule zilizopo mijini. Hali hii inasababisha shule nyingi hasa za vijijini kuwa na Walimu wachache ambao wanafundisha vipindi zaidi ya idadi ya vipidi vinavyokubalika. Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo mchakato wa kutoa posho ya mazingira magumu kwa Walimu ili kuwafanya Walimu hao wabaki katika mazingira hayo na kuipenda taaluma yao (*Retaintion Scheme*).

(ii) Serikali kupitia Halmashauri husika kutoa motisha kwa Walimu wanaofanya kazi katika muda wa ziada ikiwemo Walimu wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vyuo vya VETA nchini. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kujenga chuo kimoja cha *VETA* katika kila Wilaya, Kamati inashauri hatua hiyo ya Serikali ipewe nguvu ya kutosha ili kuongeza idadi ya vyuo hivyo nchini vitakavyowahudumia idadi kubwa zaidi ya wahitimu wa Elimu ya Msingi na Sekondari ambao hawakubahatika kuendelea na masomo. Hatua hii itawawezesha wahitimu hao, kujiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuongeza mafunzo ya VETA kwa kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Katika baadhi ya maeneo nchini kuna vyuo vya maendeleo ya wananchi *Folk Development Colleges* (*FDC*) ambavyo inapendekezwa kwamba Serikali ikiviboresha, vinaweza kutumika kutoa mafunzo zaidi ya ufundi stadi kwa kiwango cha vyuo vya *VETA*. Kamati inashauri Serikali iviboreshe vyuo vya maendeleo ya wananchi ili viweze kutoa mafunzo ya ufundi. Aidha Serikali itoe taarifa kuhusu hatua za awali zilizochukuliwa kuhusu utekelezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za rada. Pamoja na pongezi kwa Serikali kuwezesha urejeshwaji wa fedha za rada takribani Sh. bilioni 70, Kamati inashauri kwamba matumizi ya fedha hizo yafanyike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Bodi za Shule kusimamia utoaji elimu ya sekondari nchini. Bodi za shule za Sekondari nchini ni vyombo muhimu sana katika kushauri na kusimamia utoaji wa elimu katika shule husika. Uzoefu unaonesha kwamba mfumo wa uteuzi wa bodi hizo hufanyika kwa Mkuu wa Shule kupendekeza majina ya wanachama wa bodi hizo, hali inayosababisha mashaka katika kusimamia utoaji wa elimu katika shule hizo. Kamati inasisitiza kwamba uteuzi wa bodi za shule uundiwe utaratibu maalumu na wa wazi ili kupata bodi madhubuti katika kushauri na kusimamia utoaji wa elimu katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, sera ya uchangiaji elimu nchini. Kwa muda mrefu sasa kumekuwepo na mgongano katika utekelezaji wa Sera ya uchangiaji elimu hususan katika utoaji elimu ya Msingi na Sekondari nchini. Mgongano huu unasababisha baadhi ya wazazi/walezi kutochangia utoaji wa elimu kwa watoto wao, kutokana na kauli mbalimbali zinazotolewa na Serikali. Hali hii inasababisha baadhi ya shule zikiwemo shule Sekondari za Kata na Shule za Msingi zilizoko maeneo ya vijijini kukosa fedha za kuendesha shughuli mbalimbali katika maeneo yao. Kamati inashauri kwamba ni vyema Sekali kutoa muongozo mahususi wa utekelezaji wa sera ya uchangiaji elimu ili kuwezesha shule hizo kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ugatuaji wa utoaji wa elimu nchini. Pamoja na juhudi za Serikali kupeleka utoaji wa huduma ikiwemo elimu karibu na wananchi, uliotekelezwa katika dhana ya ugatuaji, hatua hii bado inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo upungufu wa rasilimali hususani rasilimali watu na fedha kwani uwezo wa Halmashauri nchini kuchangia utoaji wa huduma ikimo huduma za elimu, afya na maji ni mdogo. Kamati inashauri kwamba Serikali izipe uwezo zaidi Halmashauri kumudu utoaji wa huduma mbalimbali ikiwemo utoaji wa elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, kodi zinazotozwa kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vinavyomilikiwa na watu na Taasisi binafsi nchini. Watu na taasisi binafsi nchini zimekuwa zikichangia juhudi za Serikali za kutoa elimu ya msingi, sekondari na vyuo kwa kuzingatia miongozo ya utoaji wa elimu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Ufundi. Pamoja na mambo mengine Taasisi hizi zinakabiliwa na changamoto ya utozwaji kodi mbalimbali ikiwemo kodi ya ardhi, majengo, mapato, kodi ya kuajiri Mwalimu/mfanyakazi asiye raia wa Tanzania pamoja na kukidhi masharti ya utoaji wa huduma ya usafiri kwa wanafunzi, hali inayosababisha uendeshaji wa shughuli hizo kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba Serikali ipitie upya utaratibu wa kodi zinazotozwa kwa Taasisi hizi ili kuzisaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa utoaji wa elimu nchini. Ili kusimamia viwango vya elimu inayotolewa nchini sambamba na ongezeko la taasisi mbalimbali za idadi ya takribani 20,000 zinazotoa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo, Kamati inasisitiza kwamba Serikali iimarishe Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza jukumu la ukaguzi wa elimu ziongezwe, zitengewe akaunti maalumu na zitumike kwa kuzingatia kusudi hilo. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Idara ya Ukaguzi wa Elimu iwe Taasisi inayojitegemea ili ifanye kazi yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Pamoja na juhudi kubwa ya Serikali ya kutenga Sh. bilioni 326 kuhudumia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati imebaini kwamba utaratibu unaotumika kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu haukidhi mahitaji ya wanafunzi hususan waliotoka

katika familia zenye kipato duni. Hivyo Kamati inaendelea kufanyia kazi jambo hili hususan *Means Testing* na itatoa ushauri wake kwa Serikali kazi itakapokamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa madai ya Walimu nchini. Hivi karibuni kumekuwepo na mgomo wa Walimu nchini uliotangazwa na Chama cha Walimu Tanzania, kuishinikiza Serikali kuongeza viwango vya mishahara ya Walimu pamoja na kulipa posho za kufundishia kwa Walimu. Kamati inasisitiza kwamba Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na Serikali waendeleze majadiliano kwa kufuata Sheria za Kazi. Halikadhalika, Serikali ihakikishe kwamba vyombo vya majadiliano nchini vinafanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Vyuo Vikuu nchini "*Tanzania Commission for Universities – TCU.*" Pamoja na pongezi kwa taasisi hii kuzindua vitabu mbalimbali vinavyotoa miongozo ya udhibiti wa utoaji wa mafundisho ya elimu ya juu nchini, Kamati inasisitiza kwamba elimu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya *TCU* iendelee kutolewa kwa umma kupitia vyombo vya habari, ili kuwawezesha wananchi na wadau wa elimu kuitumia kikamilifu taasisi hii muhimu katika utoaji elimu ya juu nchini.

Mheshimiwa Spika, usimamishaji masomo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini. Kamati inasikitishwa na hali ya kukosa masomo kwa baadhi ya wanafunzi wanaojihusisha na vitendo vya migomo katika taasisi mbalimbali nchini, ikiwemo IMTU, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma na *MUHAS*.

Kamati inasisitiza kwamba Serikali ikamilishe utaratibu wa kuwarudisha masomoni wanafunzi ambao wamesimamishwa masomo hayo mapema iwezekanavyo. Aidha, Kamati inatumia nafasi hii kuwaonya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini kutojihusisha na vitendo vya migomo isiyokuwa ya lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Nakushukuru wewe binafsi kwa kushirikiana na Kamati yangu kila tunapohitaji ushauri wako na pia kwa kunipa nafsi hii kuwasilisha taarifa ya Kamati yangu. Aidha, namshukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Mheshimiwa Dkt. Shukuru J. Kawambwa, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Philipho A. Mulugo na Watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu, Ndugu Selestine Gesimba kwa kushirikiana na Kamati.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa kushirikiana nami katika kuiongoza vyema Kamati. Kwa namna ya pekee, nawashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati kwa busara na umakini katika kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu na makadirio ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwa kuuthamini ushirikiano huo, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dkt. Maua A.

Daftari, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Saidi R. Bwanamdogo, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Lameck O. Airo, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Ali J. Haji, Mheshimiwa Anna MeryStella J. Mallack na Mheshimiwa Antony G. Mbassa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangala, Mheshimiwa Nyambari C. Nyangwine, Mheshimiwa Rashidi A. Omari, Mheshimiwa Said S. Suleimani, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Faki H. Makame, Mheshimiwa Highness S. Kiwia, na Mimi Martha M. Mlata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, wakiwemo Makatibu wa Kamati hii Ndugu Stella Mlambo na Ndugu Happiness Ndallu, chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kutusaidia kuokoa muda. Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hiyo. Mheshimiwa Susan A. Lyimo. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99, Kanuni ndogo ya (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007, napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika**,** kabla ya kuwasilisha maoni hayo, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya njema na hivyo kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kama Waziri mtarajiwa wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, ninamshukuru sana Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Napenda kumhakikishia kuwa nitatekeleza wajibu wangu kwa juhudi na bidii kubwa ili kukidhi matarajio ya Watanzania ya kuona mageuzi makubwa katika sekta ya elimu yanatokea na

kuwanufaisha wanachi wote. Aidha, nawapongeza sana viongozi na makamanda wote wa CHADEMA kwa kazi kubwa wanayoifanya bila kuchoka ya kuwahamasisha Watanzania kushiriki kikamilifu katika michakato ya kisiasa kupitia operesheni za *M4C* ambazo zimewafungua macho wananchi na sasa uelewa wao kuhusu masuala mbalimbali ya nchi yao uko juu sana. Tunapenda kuwahakikishia wananchi wote kwamba bado kitambo kidogo tu tutaifikia ile nchi ya ahadi, hivyo wasichoke na waongeze juhudi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, namshukuru sana marehemu baba yangu mzazi, Mzee Lyimo, kwa kunipatia elimu, bila ubaguzi na ndio imenifanya niweze kusimama hapa leo hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na mume wangu mpenzi Bonaventure Ngowi na watoto wetu Charlene, Dennis na Aidan, kwa upendo wao kwangu na uvumilivu wao kwa kipindi kirefu ninapokuwa mbali nao kwa shughuli za kichama na kibunge. Aidha, nawashukuru kwa namna ya pekee mama zangu wapendwa Maria Lyimo na Atanasia Seiya, kwa ushauri na sala zao kwangu ambavyo vimeniwezesha kutimiza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Kwao wote nasema, ”Ahsante sana”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu na mustakabali wa maendeleo ya Taifa: tulikotoka na tuendako. Si jambo la kubishaniwa kwamba elimu ni roho ya maendeleo

ya taifa. Elimu ni muhimu sana kwa taifa lolote kwani ndio silaha madhubuti ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha. Taifa lenye watu walioelimika, bila shaka huweza kirahisi kuvumbua mambo na vitu vipya ambavyo kwa ujumla wake vinahitajika na binadamu katika kumudu maisha na mazingira yake. Aidha, elimu hutumika kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayomkabili binadamu katika mapambano dhidi ya mazingira magumu yanayomzunguka.

Mheshimiwa Spika**,** kwa kutambua umuhimu wa elimu katika maendeleo ya Taifa, Rais Mstaafu wa Afrika ya Kusini Mzee Nelson Mandela mwaka 1991 aliwahi kusema:-

"...*elimu ni injini kubwa ya maendeleo ya mtu. Ni kupitia elimu ndipo binti wa mkulima mdogo anaweza kuwa Daktari Bingwa, kwamba mtoto wa kibarua wa mgodini anakuwa Mkuu wa Mgodi, na mtoto wa kibarua wa mashambani anakuwa Rais wa taifa kubwa".*

Mheshimiwa Spika, ni katika kutambua umhuhimu wa elimu, muasisi wa taifa letu aliweka elimu kama kipaumbele cha taifa. Itakumbukwa kwamba Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kutangaza vita dhidi ya Ujinga, Umasikini na Maradhi kama maadui watatu wa Taifa. Hata hivyo, alisema Ujinga ndio adui mkubwa zaidi kwa kuwa pasipo na ujinga ni rahisi kutokomeza umaskini na maradhi. Hivyo, Mwalimu alianzisha mikakati madhubuti ya kufuta ujinga.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mikakati hiyo, ni kuanzishwa kwa falsafa mpya ya elimu iliyojulikana kwa jina la Elimu ya Kujitegemea na kuanzishwa kwa Kisomo cha Watu wazima chenye Manufaa. Sambamba na mikakati hii, ilikuwa ni kutungwa kwa Sera ya Elimu na kuanzishwa kwa Taasisi ya Elimu pamoja na uundwaji wa Baraza la Mitihani la Afrika Mashariki. Jitihada nyingine zilikuwa ni ujenzi wa vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na kutolewa kwa tamko la Elimu kwa Wote (UPE), ujenzi wa vyuo vya ufundi kwa wahitimu wa elimu ya msingi na kuanzishwa kwa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, jitihada zote hizi za kuhakikisha taifa linaondokana na adui ujinga zilifanyika kati ya mwaka 1965 na 1980. Matokeo ya jitihada hizi yalionekana wazi kwa kuwa hadi kufikia mwaka 1986 kiwango cha Watanzania kujua kusoma na kuandika kilikuwa ni asilimia 91 (Maelezo na takwimu hapa yamefanyiwa marejeo katika utafiti uliofanywa na Elizabeth Missokia & Mtemi Zombwe chini ya udhamini wa Haki Elimu juu ya "Hali ya Elimu Tanzania: Tafiti na Uhalisia vinatuambia nini?") na hivyo kuiweka Tanzania katika nafasi nzuri katika nchi za Afrika zilizoongoza kwa kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Spika, maendeleo katika sekta ya elimu yaliendelea kwa kasi mpya kipindi cha awamu ya tatu mwaka 1995 hadi 2005. Kipindi hiki kilishuhudia kuanzishwa kwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu *(ESDP),* kuanzishwa kwa Mpango wa Maendeleo

ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) na hatimaye Mpango wa Elimu Maalum kwa Watoto Waliokosa (MEMKWA)

Mheshimiwa Spika, awamu ya nne imeendelea na mkakati wa kuendeleza sekta ya elimu kwa kutoa bure elimu ya shule ya msingi na kutekeleza mpango wa kujenga shule za sekondari kila kata. Aidha, kipindi hiki cha Awamu ya Nne ya utawala, Watanzania wameshuhudia kujengwa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma, chuo ambacho ni miongoni mwa vyuo vikubwa kusini mwa Jangwa la Sahara vilivyojengwa kwa fedha za ndani (Fedha kutoka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii). Jambo hili ni la kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, maendeleo haya katika Sekta ya elimu yamekwenda sambamba na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari. Hadi mwaka 2010 zaidi ya watoto milioni nane (8), ambao ni zaidi ya 90% ya uandikishaji halisi, wameandikishwa shule za msingi na takriban wanafunzi 1,638,699 wako katika elimu ya sekondari. Aidha, shule za sekondari zimeongezeka kutoka shule 937 hadi kufikia shule 4,266 mwaka 2010 (*BEST, 2010).*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshtushwa sana na kudorora kwa sekta ya elimu ambako kumesababisha kiwango cha elimu ya Tanzania kushuka kwa kasi kubwa licha ya mikakati na mipango mbalimbali ya kuboresha Elimu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Prof. Bhalalusesa, Mtafiti na Mhadhiri wa Elimu katika Shule Kuu ya Elimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, viwango vya kupunguza ujinga *(illiteracy)* tangu uhuru vimekuwa kama kama ilivyooneshwa kwenye jedwali namba 1 hapa chini.

JEDWALI NA. 1: MWENENDO WA KUPUNGUZA UJINGA (ILLITERACY) TANGU 1961 – 2000.

| 1961 | 1975 | 1977 | 1981 | 1983 | 1986 | 1992 | 2000 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 85% | 37% | 27% | 20% | 15% | 10% | 15% | 32% |

Mheshimiwa Spika, taarifa ya kitaifa juu ya mafanikio na changamoto za kufikia lengo la kutoa elimu kwa wote ya mwaka 2000 inaonesha kwamba ingawa Tanzania imeonesha nia ya kufikia lengo la kutoa elimu kwa wote, nia hiyo imekuwa ikitekelezwa taratibu sana kuliko ilivyotarajiwa. Aidha, taarifa hiyo ilionesha kwamba kiwango cha kujua kusoma na kuandika ambacho kilikuwa kimeshafikia asilimia 90 mwaka 1986 kilipungua hadi asilimia 84 mwaka 1992 na kimekuwa kinapungua kwa asilimia 2 kwa mwaka. Kwa sasa kiwango cha kujua kusoma na kuandika kimefikia asilimia 69. Hii ni kwa mujibu wa Prof. E.P. Bhalusesa, Mtafiti na Mhadhiri wa Elimu katika Shule Kuu ya Elimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi ni dhahiri kuna tatizo kubwa katika elimu hapa Tanzania. Kama mwelekeo ni kuwa kiwango cha kujua kusoma na kuandika kinapungua kwa asilimia mbili (2%) kwa mwaka ni kwamba kuna hatari ya kujikuta kwamba

nusu ya watu wote hapa nchini wakawa hawajui kusoma wala kuandika.

Mheshimiwa Spika, kitendawili kinachojitokeza katika sekta ya elimu ni kwamba wakati mipango na mikakati ya kuboresha elimu inafanyika kwa wingi, ndio kiwango cha wasiojua kusoma na kuandika kinaongezeka, kiwango cha ufaulu kinapungua na ubora wa elimu unazidi kuporomoka. Hapo ndio tunajiuliza CCM mnatupeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba wanafunzi wanamaliza darasa la saba hawajui kusoma wala kuandika. Kwa mujibu wa Taarifa ya HakiElimu ya Aprili 2012, ni kwamba wanafunzi 5,200 waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu 2012, hawajui kusoma wala kuandika. Hili ni jambo la ajabu kabisa na Tanzania inastahili kabisa kuingia kwenye Kitabu cha Kumbukumbu za Maajabu ya Dunia (*The Guiness Book of Records*) kwa kushika nafasi ya kwanza kwa kufaulisha wanafunzi wasiojua kusoma wala kuandika. Hii ni kashfa kubwa na kama kweli Serikali hii ingekuwa inafuata misingi ya utawala bora na uwajibikaji basi leo viongozi wakuu wa elimu wangeshaachia nafasi zao. Lakini tumeendelea na utamaduni uleule wa *"Business As Usual"*. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania ni nini hasa kilitokea hadi mwanafunzi ahitimu elimu ya miaka saba na afaulu na kupokelewa Kidato cha Kwanza wakati hajui kusoma, kuandika wala kuhesabu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashangaa kwamba mpaka sasa Waziri wa Elimu na Naibu wake bado wapo madarakani wakishangilia ushindi wa kuliongoza Taifa kushika nafasi ya kwanza duniani kwa kufaulisha wanafunzi 5,200 wasiojua kusoma na kuandika. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, hivi ni mpaka Waziri Mkuu atishiwe kupigiwa kura ya kutokuwa na imani naye ndio Waziri wa Elimu na Naibu wake wajiuzulu? Kwa nini wasiwajibike kwa uzembe na makosa ya waziwazi yanayotokea chini ya uongozi wao?

Mheshimiwa Spika, moja ya sababu za tatizo hili la kuhitimu elimu ya msingi bila kujua kusoma wala kuandika ni ufisadi wa aina yake katika sekta ya elimu ambapo baadhi ya watendaji wa elimu hawatimizi wajibu wao ipasavyo na kuamua kwa makusudi kujihusisha na vitendo vya rushwa jambo ambalo limesababisha kuvuja kwa mitihani na hivyo kuwalemaza wanafunzi kifikra kwa kuwaaminisha kwamba kufaulu kunawezekana bila bidii katika masomo. Ikumbukwe kwamba Baraza la Mitihani la Taifa liliwafutia wanafunzi 9,736 matokeo yao ya Darasa la Saba mwaka jana baada ya kugundulika walifanya udanganyifu katika mtihani huo. Huu ni ushahidi tosha kwamba katika sekta ya elimu kuna mafisadi wenye uchu wa utajiri wa harakaharaka kwa gharama yoyote ikiwa ni pamoja na kuiua elimu yetu kwa kuuza mitihani.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine inayopelekea wanafunzi kuhitimu bila kujua kusoma na kuandika ni maagizo wanayopewa Walimu Wakuu kutoka kwa

Maafisa Elimu kwamba lazima wahakikishe wanafunzi wanafaulu huku wakijua shule hazina Walimu wa kutosha wala vitendea kazi. Matokeo ya maagizo haya yasiyozingatia mahitaji ya msingi ili wanafunzi wafaulu, yanachochea Walimu hawa kufanya kila mbinu kufaulisha watoto. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwaeleza wananchi kupitia Bunge hili ni hatua zipi zimechukuliwa dhidi ya wale wote waliofaulisha watoto kwa njia ya udanganyifu?

Mheshimiwa Spika, kuporomoka kwa ubora wa elimu nchini sambamba na Serikali kushindwa kudhibiti mfumo mzima wa utoaji wa elimu kumetufikisha hapa tulipo; miaka 50 ya Uhuru bado tunaogelea kwenye dimbwi la umaskini wa kutisha licha ya rasilimali lukuki zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia historia fupi ya elimu hapa nchini ni kwamba tulikotoka kuna afadhali kuliko tunakoelekea. Kwa ujumla, hali ya elimu hapa nchini inazidi kudorora. Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba; kwa kuwa Sera za CCM zimeshindwa kuboresha elimu hapa nchini kwa muda wote wa miaka 50 ambao Serikali ya CCM imetawala; kunahitajika mabadiliko makubwa ya mfumo wa utawala. Kwa kuwa miaka 50 ni muda unaozidi kipimo cha kujipima kiutendaji na kwa kuwa muda wote huo Sera za CCM zimeshindwa kuleta mabadilko yaliyokusudiwa katika kuboresha elimu ya Tanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kukiunga mkono Chama cha Demokrasia na Maendeleo ili kiunde Serikali ifikapo 2015 na kiboreshe elimu kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu na Mwelekeo wa Maendeleo ya Elimu nchini. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa hotuba ndefu yenye mambo ya kawaida ambayo kamwe hayawezi kuleta maendeleo hasa katika kuongeza ubora wa elimu katika ngazi zote. Wasiwasi wangu unatokana na ahadi zilizotolewa na zinazoendelea kutolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambazo kutokana na ukosaji wa umakini hazijatekelezwa na kwa zile zinazotekelezwa kasi yake ni ndogo sana kiasi kwamba ni vigumu kuona mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kuwa mwaka jana alilieleza Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yake ilikuwa mbioni kukamilisha marekebisho ya Sera ya Elimu ya 1995 na kutengeneza Sera mpya ya Elimu. Kwa kuwa Sera ya Elimu ndio dira ya namna elimu inavyotakiwa kutolewa hapa nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze mbele ya Bunge hili kwamba, mchakato huo umefikia wapi na lini tutapata sera mpya?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba wakati Serikali inaendelea na mchakato wa marekebisho ya Sera, basi walau ifanye mapitio ya mfumo wetu wa elimu ya sasa ili kufanya marekebisho katika Elimu ya Msingi ya sasa. Kutokana na ubora wa elimu kushuka sana katika nchi yetu, tunashauri Elimu ya Msingi na ile ya Sekondari ya Kawaida (Kidato cha I – IV) iwe ni Elimu ya Msingi na iwe ni elimu ya lazima kwa watoto wote wenye umri

wa kuanza shule. Aidha, katika kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwe na msisitizo wa pekee wa kisera kuhusu elimu ya Watu Wazima. Serikali ielekeze nguvu kubwa kwenye utoaji wa Elimu ya Watu Wazima na elimu hiyo izingatie mahitaji ya watu wazima katika jamii husika. Lengo liwe ni kuwa na watu wazima wenye kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na wenye ari ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, Madai ya Walimu na Hatima ya Elimu nchini. Ni ukweli usiopingika kwamba Mwalimu ndiye kitovu cha wa elimu ya aina yoyote ile. Mwalimu aliyefuzu mafunzo yake vizuri, anayefanya kazi katika mazingira mazuri na anayepata stahili zake ipasavyo huwa na bidii katika kazi yake na tija yake huwa ni kubwa na matokeo yake ubora wa elimu huongezeka. Aidha, Mwalimu anayefanya kazi katika mazingira magumu, asiyethaminiwa kwa mchango wake wa kazi, asiyelipwa stahili zake ipasavyo, asiyesikilizwa anapodai stahili zake hukatishwa tamaa na bidii yake ya kazi hushuka na matokeo yake ni kushuka kwa ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Dkt. Kitila Mkumbo, Mhadhiri Mwandamizi na Mkuu wa Kitivo cha Elimu katika Chuo Kikuu cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), ‘Elimu ni Walimu’. *“Kuchezea Walimu ni kuchezea elimu, na Taifa lolote linalochezea elimu ni taifa linalojiandaa kujifuta duniani. Hata kama utaboresha kila kitu, ikiwemo majengo, maabara, ukaweka vitabu vyote bora duniani na ukaacha kumlenga Mwalimu ni kazi bure. Kinyume chake ni*

*kwamba ukiwa na Mwalimu bora aliyeamua kufundisha kwa dhati, mtoto ataelewa hata kama anafundishwa chini ya mti bila vitabu na bila maabara. Bahati mbaya maboresho ya elimu yanayoendelea hapa nchini yamemuengua na kumweka pembeni Mwalimu. Tumewekeza fedha nyingi katika kuboresha majengo na miundombinu mingine ya kujifunzia lakini Mwalimu amewekwa pembeni katika maboresho haya".*

Mheshimiwa Spika, si jambo geni kwa Serikali kwamba Walimu wa nchi hii wamekuwa wakilalamikia maslahi duni katika kazi yao ya ualimu, mazingira magumu ya kufanyia kazi na kutolipwa stahili zao kama vile malimbikizo ya mishahara, posho ya uhamisho, likizo, kutopandishwa madaraja na kadhalika. Kwa mfano Walimu 146 wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga ambao waliajiriwa mwaka 2008 kati yao wapo waliopandishwa madaraja lakini hawajalipwa stahili zao na wengine hawajapandishwa kabisa. Tafiti zinaonyesha kwamba, ni kada ya ualimu pekee ambapo mtu anaweza kuajiriwa na akafanya kazi kwa miezi sita au zaidi bila kulipwa mshahara kwa visingizio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa namna yoyote ile hali kama hiyo haiwezi kumwongezea Mwalimu ari ya kufanya kazi kwa bidii. Hakuna shaka pia kuwa mgomo wa Walimu ulitokana na Serikali kuendelea kupuuza na kutojali maslahi ya Walimu. Hata hivyo, Serikali imeendelea kutumia nguvu na vitisho dhidi ya Walimu kama njia ya kuwanyamazisha Walimu kudai haki zao. Kitendo cha Serikali kukimbilia Mahakamani ili

kuepusha masuala yenye mvutano kama madai ya Madaktari na madai ya Walimu yasijadiliwe Bungeni kunazidi kuzorotesha utoaji wa huduma katika sekta husika. Aidha, ni kulihujumu Bunge haki yake kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayolipa Bunge haki na nguvu ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Huku ni kudumaza demokrasia na kwa maana hiyo ni kudumaza maendeleo, kwa kuwa demokrasia huchochea maendeleo.

Mheshimiwa Spika kutokuwa na mgomo halisi *(Active Strike*) kusiifanye Serikali ifikiri kwamba imemaliza tatizo la madai ya Walimu, kwani kuna migomo baridi ambayo athari zake huwa ni mbaya zaidi ya mgomo halisi. Kwa mfano, baadhi ya vyombo vya habari vimewanukuu Walimu wakisema kwamba "Tunarudi kazini kwa kinyongo*".*

Mheshimiwa Spika, kama Walimu wataachwa na kinyongo kama walivyoachwa sasa na kama wataamua kulipa kisasi kwa kuwafundisha watoto vitu visivyo halisi basi kuna hatari kubwa ya kuja kuwa na kizazi kisicho na elimu kabisa na hatimaye kuwa na Taifa lisilojiweza katika nyanja zote na hapo ndipo kutakuwa na Anguko Kuu la Nchi (*Total State Collapse).*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba suala la mgomo wa Walimu lilishatolewa uamuzi na Mahakama. Kambiya Rasmi Upinzani ilidhani kwamba Serikali ingechukua nafasi hiyo ili kufanya mazungumzo na Chama cha Walimu ili

kufikia maridhiano na hivyo kusonga mbele katika kuboresha elimu yetu. Jambo la kushangaza na kushtusha ni kwamba Serikali badala ya kuhakikisha kuwa mgogoro huu unakwisha, inaanzisha mgogoro mwingine na Chama cha Walimu kwa kuanza kukisakama ili kikose heshima mbele ya Walimu na mbele ya jamii. Kambi Rasmi ya Upinzani inatafsiri Kauli ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 10 Agosti 2012 kuwa haina nia ya kusuluhisha mgogoro wa Walimu na Serikali, bali ina nia ya kukidhalilisha au kukiadhibu Chama cha Walimu na kudhoofisha umoja wa Walimu nchini. Huku ni kuwakandamiza Walimu kwa kuwanyima haki yao ya msingi ya kutoa madukuduku yao kupitia chama chao. Aidha Kambi ya Upinzani ina mtazamo kwamba hata kama madai ya Walimu yalikuwa ni makubwa kuliko uwezo wa Serikali, basi walau wangezungumza ili wakubaliane kuyapunguza na sio kusema kuwa “madai ya Walimu hayalipiki”.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina mtazamo pia kwamba baada ya hukumu kutolewa ambapo kimsingi Chama cha Walimu waliikubali na kusitisha mgomo kama walivyoamriwa na Mahakama, kusingekuwa na haja tena ya Serikali kuja kukazia hukumu kwa kutoa kauli iliyojaa vitisho kwa Chama cha Walimu.

Mheshimiwa Spika, ili kujenga mazingira ya amani, maridhiano na ushirikiano katika jitihada za kuboresha elimu ya Tanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali, kwa nia njema kabisa kutazama upya suala la Walimu kwa kufuta kauli yake ya tarehe 10 Agosti 2012

na kuzungumza na Walimu ili kuondoa hali ya uhasama iliyojengeka miongoni mwa Walimu na Serikali ambayo inatishia maendeleo ya Sekta ya elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Elimu na Kuporomoka Kwa Elimu ya Tanzania. Ukaguzi wa shughuli za kufundisha na kujifunza ni mizania muhimu ya kupima mafanikio au changamoto za kufanyia kazi ili kuboresha mfumo wa elimu wa nchi yetu. Ili kukidhi matakwa ya elimu bora ni lazima kitengo cha ukaguzi wa elimu kwa ngazi zote, yaani Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari kifanye kazi mara kwa mara na kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kukiachia kitengo cha ukaguzi kutegemea mawasilisho ya makato ya ada ya shilingi mia tano kwa kila ada ya mwanafunzi kwa kila shule ni kukifanya kitengo cha ukaguzi kudumaa na kutokufanya kazi yake ipasavyo. Hii maana yake ni kwamba kwa zile shule ambazo hazitaweza kuwasilisha kiasi hicho cha pesa ni kwamba hazitaweza kukaguliwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kitengo hiki, kiuhalisia kinaishi kwa kutegemea fadhila za vitengo vingine kwenye Halmashauri zetu. Wakaguzi wengi hawana magari wala pikipiki za kuwawezesha kwenda kukagua shule na kwa taarifa tulizo nazo ni kwamba baadhi ya Wakaguzi huacha kufanya ukaguzi hata kwa muda wa miaka miwili kutokana na kukosa fedha za kufanya kazi hiyo. Ushahidi wa jambo hili ni kwamba katika bajeti ya mwaka jana 2011/2012 kitengo cha Ukaguzi wa Shule kilitengewa kiasi cha

shilingi milioni 100 lakini hadi tarehe 30 Aprili 2012, kitengo hiki kilikuwa hakijapokea hata senti moja kwa ajili ya ukaguzi wa shule (Tazama Randama uk. 28). Matokeo yake shule nyingi hazikaguliwi na hivyo kufanya baadhi ya Walimu kutowajibika ipasavyo na kusababisha mdororo wa ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 shule za msingi 3061 (42.5%) tu kati ya shule 7,200 zilizolengwa na 935 za sekondari kati ya 2,100(43.3%) zilikaguliwa. Takwimu zinaonesha kuwa ni takribani 20% ya shule zimekaguliwa hivyo itachukuwa miaka mitano kukamilisha shule zote nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua, hadi sasa ni kiasi gani cha fedha kilichotolewa kwa ajili ya Ukaguzi wa Shule? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo kwamba shule moja inatakiwa ikaguliwe mara ngapi kwa mwaka ili kuhakiki ubora wa elimu inayotolewa?

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri akijibu swali namba 66 hapa Bungeni tarehe 14 Februari, 2011 alisema kwamba:-

*“Idara imeanzisha utaratibu wa ukaguzi wa shule kwa kuzingatia makundi ya ubora ambapo shule zilizo chini ya kiwango zitakaguliwa mara nyingi zaidi ili kuinua kiwango cha ubora. Vilevile Wizara katika utaratibu wake wa kuimarisha ukaguzi wa shule, imeandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Shule kwa lengo la kuwawezesha Walimu Wakuu na Waratibu Elimu Kata kama Wakaguzi wa Ndani na wa karibu wa shule, kusimamia shule ili ziweze kujiletea maendeleo*

*kwa kuzipatia msaada endelevu wa kitaalamu na kitaaluma".*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Rasmi Upinzani inaamini kabisa kuwa kazi ya ukaguzi haipaswi kufanywa na Walimu Wakuu wa Shule, kwani hata Mwalimu Mkuu naye anatakiwa kukaguliwa. Je, utaratibu upi utatumika? Ifahamike kuwa huyu ndiye msimamizi wa masuala ya shule hivi atakuwa tayari kujikosoa yeye mwenyewe?

Mheshimiwa Spika, ongezeko la udahili wa wanafunzi na ubora wa elimu: Ni nini Kipaumele cha Taifa? Serikali ya CCM kupitia Wizara hii imekuwa ikijigamba sana kwamba imepata mafanikio makubwa ya kutoa elimu kwa idadi kubwa ya vijana wa nchi hii. Kila mwaka Wizara imekuwa inatugawia kijitabu kinachojulikana kama *BEST*, (*Basic Education Statistics in Tanzania*) chenye takwimu za mafanikio hayo. Huu ukiwa ni upande mmoja tu wa shilingi kwani unaelezea tu idadi kubwa ya wanafunzi wanaodahiliwa katika shule zetu bila kuelezea maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi hao.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu za ufaulu ngazi ya sekondari, daraja la kwanza hadi la tatu, zinasikitisha na kukatisha tamaa. Kwa mfano matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2011, kati ya watahiniwa wote, ni asilimia 4.3 tu walifaulu kwa kiwango cha daraja la I – II na ni asilimia 7.1 tu waliopata daraja la III huku asilimia 38.6 wakipata daraja la IV na asilimia 50 walifeli kabisa kwa kupata alama sifuri.

Mheshimiwa Spika, sifa hizi zote mbaya za upande wa pili wa shilingi zinadhihirisha wazi jinsi Serikali ya CCM inavyozidi kuboronga katika utoaji wa elimu mbovu kwa sababu ambazo kamwe haitaki kuzitaja, huku Taifa letu likiendelea kutumbukia katika kilindi cha kuzalisha mbumbumbu. Ni kwa sababu hizi Kambi Rasmi ya Upinzani inaiona hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni ya kawaida sana isiyokuwa na mkakati wowote mpya na mbinu madhubuti za kuboresha elimu.

Mheshimiwa Spika, mikopo elimu ya juu na migomo vyuo vikuu. Kushindwa kwa Bodi ya Mikopo kusimamia utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kumeendelea kuwa chanzo cha migomo na kukosekana kwa amani katika vyuo vikuu vingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kushindwa kwa Bodi ya Mikopo kusimamia utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kumeendelea kuwa chanzo kikuu cha migomo na vurugu na ukosefu wa amani katika vyuo vya elimu ya juu. Kumekuwa na mvutano kati ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Utawala wa Vyuo Vikuu juu ya ucheleweshaji wa mikopo ya wanafunzi. Wakati watawala wa vyuo wanajiondoa kwenye tatizo hili na kuwatupia lawama watendaji wa Bodi ya Mikopo, Bodi ya Mikopo nayo imekuwa ikiwatupia lawama watawala wa vyuo kwamba inatuma mikopo ya wanafunzi kwa wakati ila watawala wa vyuo ndio wanawacheleweshea wanafunzi kwa kutopeleka majina ya wanaostahili hususan *continuing students.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na matatizo ya migomo katika vyuo vikuu, ambayo yanasababishwa sana na udhaifu katika mfumo wa utoaji wa mikopo, Rais Jakaya Kikwete aliteua Tume ya wataalamu 11 wakiongozwa na Profesa Makenya Maboko kwa ajili ya kufanya mapitio ya mfumo wa uendeshaji wa Bodi ya Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Tume hiyo ilipewa siku 60 kuanzia tarehe 14 Februari, 2011 na ilishawasilisha ripoti yake kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, jambo la ajabu ni kwamba ripoti hii bado haijawekwa hadharani hivyo kuendelea kuwa siri, hivyo matatizo ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu yameendelea kubaki bila kupatiwa ufumbuzi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iweke ripoti hii wazi pamoja na mikakati iliyopendekezwa ya kushughulikia matatizo ya Bodi ya Mikopo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze katika Bunge hili ni lini matatizo ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu yatakwisha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na suala hili la mikopo ya elimu ya juu kuwa tatizo la muda mrefu na kwa kuwa migogoro ya mikopo imesababisha migomo ya mfululizo katika vyuo vikuu na hivyo kusababisha vyuo kufungwa na baadhi ya wanafunzi kusimamishwa masomo na hivyo kuathiri sana taaluma na maisha ya wanafunzi kwa ujumla, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kufanya ukaguzi maalumu wa kiutendaji (*Special Performance Audit*) katika Bodi ya Mikopo na vyuo vinavyopewa mikopo ya wanafunzi ili kujua kiini cha tatizo.

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe wakati akiwasilisha hotuba yake hapa Bungeni tarehe 25 Juni, 2012 alitoa wito kwa Serikali kuwarudisha wanafunzi 260 wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* waliokuwa wamesimamishwa masomo kwa muda mrefu kwa sababu ya mgomo uliotokana na kutopatiwa fedha za mafunzo kwa vitendo. Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mara nyingine inaitaka Serikali kutoa tamko juu ya hatma ya wanafunzi hao na haki yao ya kupata elimu katika nchi yao. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali pia kueleza mbele ya Bunge hili kwamba huwa inatumia vigezo gani kuwarudisha wanafunzi waliokuwa wamesimamishwa masomo? Tunauliza swali hili kwa sababu kuna malalamiko kwamba kuna ubaguzi na upendeleo unaofanyika wakati wa kuwarudisha wanafunzi wa vyuo vikuu. Hali hii imesababisha wanafunzi 25 wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kutorudishwa masomoni mpaka sasa tangu wenzao warudishwe na hakuna sababu za msingi zinazotolewa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwarejesha wanafunzi hao ili waendelee na masomo kwani ni haki yao ya Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuamuru wanafunzi wote katika vyuo vyote waliosimamishwa masomo kutokana migomo iliyotokana na masuala ya mikopo warudishwe mara moja kuendelea na masomo kwa kuwa migomo hiyo ilisababishwa na matatizo ya Bodi ya Mikopo na utawala wa vyuo hivyo kuwacheleweshea mikopo vinginevyo wasingegoma.

Mheshimiwa Spika, ubaguzi wa mikopo kwa baadhi ya kozi za vyuo vikuu. Kwa mujibu wa Kitabu cha Mwongozo wa Udahili kwa Taasisi za Elimu ya Juu (2012/2013 – 2014/2015) *(Admissions Guide Book for Higher Education Institutions in Tanzania 2012/13 – 2014/2015)* ni kwamba kuna kozi zenye kipaumbele katika kupata mkopo na nyingine sio za kipaumbele. Kwa mfano kozi zote za Ualimu na baadhi ya kozi za sayansi zina kipaumbele cha mkopo *(Loan Priority)* wakati kozi nyingine hazina kipaumbele cha mkopo (*Non Priority).*

Mheshimiwa Spika, jambo hili limefanyika ili kuwavutia wanafunzi wengi zaidi kuomba kozi za sayansi na ualimu ili kukidhi upungufu wa wataalamu katika sekta hizo. Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni kwamba utaratibu huo hautakidhi mahitaji kwani mkakati ulitakiwa uanze katika ngazi za awali kabisa za elimu. Kama wanafunzi hawapati mvuto wa kusoma masomo hayo tangu awali, hata ukitoa mkopo asilima mia moja wakati wa kujiunga na chuo kikuu, bado hutapata waombaji kwani wenye msingi huo ni wachache au hawapo kabisa.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine la utaratibu huu ni kuwalazimisha wanafunzi kusoma masomo ambayo pengine kwao sio kipaumbele ila kwa kuwa hawana fedha za kujilipia itabidi tu wasome kwa lazima na matokeo yake ni kupata wataalamu wasio na mapenzi na kazi zao. Hivi Serikali haijiulizi ni kwa nini wahitimu wa taaluma ya elimu ni wengi kuliko taaluma nyingine lakini taifa bado lina upungufu mkubwa wa Walimu?

Aidha, watoto wa wakulima ambao wengi wao wamesoma katika shule za michepuo ya Sanaa (*Arts*) watashindwa kujiunga na chuo kikuu kwa kukosa mkopo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufuta ubaguzi huu wa kutoa mikopo kwa baadhi ya kozi na kuacha baadhi ya kozi na badala yake kutoa mikopo kwa kozi zote ili kumwachia mwombaji uhuru wa kusoma kozi anayoitaka. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta utaratibu wa kutoa mikopo kwa kufanya "*Means Testing*". Serikali itoe mikopo kwa wote kwa usawa kwani mikopo hii itarudishwa na wakopaji.

Mheshimimwa Spika, wahitimu wa vyuo vikuu kunyimwa vyeti kutokana na mikopo yao kutowasilishwa vyuoni. Wapo wanafunzi wawili katika Chuo Kikuu cha Dodoma walionyimwa vyeti vyao vya kuhitimu kutokana na kudaiwa ada ambayo ilitakiwa ilipwe na Bodi ya Mikopo. Wanafunzi hawa wakienda Bodi ya Mikopo wanaambiwa kuwa fedha ilishalipwa Chuoni, wakienda Chuoni wanaambiwa fedha haijalipwa, sasa wamebaki bila kujua cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kukiagiza Chuo Kikuu cha Dodoma kuwapatia wanafunzi hao vyeti vyao kwani si makosa ya wanafunzi bali ni Bodi ya Mikopo inahusika, hivyo Chuo kisaidie kuwasiliana na Bodi ili kujua ni nini kilitokea hadi ada hiyo isifike chuoni. Aidha, wanafunzi wa vyuo vingine wenye matatizo yanayofanana na hili wapewe vyeti vyao na vyuo husika na madai ya ada

yaelekezwe kwenye Bodi ya Mikopo ambayo ilishakubali kutoa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya kiutawala katika vyuo vikuu. Matatizo mengi katika vyuo vikuu yamefunikwa na tatizo la migomo inayosababishwa na kucheleweshewa mikopo. Hivyo nguvu kubwa huelekezwa katika kutatua masuala ya mikopo na kuacha mambo mengine muhimu kama ya uboreshaji wa miundombinu katika vyuo hivyo. Kwa mfano, katika Chuo Kikuu cha Ekenford – Tanga, wanafunzi wanalipa ada ya huduma ya *Internet* shilingi 350,000/- kwa mwaka wa kwanza na shilingi 60,000/= kwa mwaka wa pili lakini huduma hiyo haipo chuoni.

Mheshimiwa Spika, chuo hiki pia hakina Wahadhiri wenye Shahada za Uzamivu wanaofundisha. Yupo Profesa mmoja na Dokta mmoja ambao wanafanya shughuli za utawala na sio kufundisha. Chuo hiki hakina hosteli kwa ajili ya malazi ya wanafunzi. Uongozi wa chuo unachofanya ni kukodi nyumba za wageni "gesti" na kulazimisha wanachuo wakae humo lakini gesti hizo zinachanganya wanachuo na raia wengine wasio wanachuo yaani raia wa kawaida hivyo kusababisha usalama wa wanachuo kuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi katika chuo hiki hawana "*Prospectus*" jambo ambalo linawafanya wasome bila kufanya uchaguzi wa masomo ipasavyo na bila kujua masharti ya kozi mbalimbali wanazosoma. Aidha *"Almanac"* ya chuo haifuatwi jambo linalofanya mambo mbalimbali kufanywa bila kufuata ratiba.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukichunguza Chuo cha Ekenford ili kuona kama kina sifa ya kuendelea kuwa Chuo Kikuu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kukagua vyuo vingine pia ili kuona kama vinakidhi masharti ya kuendelea kuwa vyuo vikuu kwani kuna mambo mengi yasiyofaa katika vyuo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ajira vyuo vikuu nchini. Kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu na *Charter* za Vyuo Vikuu hapa nchini, ajira ya watumishi wa vyuo vikuu ni jukumu la Mabaraza ya Vyuo Vikuu. Hata hivyo, Serikali hii ya Awamu ya Nne imeanzisha utaratibu wa wataalamu wanaostaafu katika vyuo vikuu kuomba kibali cha kuajiriwa kutoka utumishi. Jambo hili limeleta usumbufu mkubwa kwa vyuo na kimsingi kunavunja dhana nzima ya uhuru ambao vyuo vikuu wanapaswa kuwa nao. Kambi ya Upinzani inataka Serikali itoe maelezo kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, wakati kuna upungufu mkubwa wa wanataaluma wenye Shahada za Falsafa, licha ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu mwaka jana kutoa ahadi za kufuatilia pendekezo la kuongeza umri wa kustaafu kwa hiari wanataaluma kutoka miaka sitini hadi sitini na tano na kustaafu kwa lazima kufikia sabini, ni kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi kutoa uamuzi wake kuhusu jambo hili? Kama kuna wanaowaonea gere wanataaluma wetu kwa nini wasijitahidi nao wakaona urahisi uliopo kupata sifa za kuwa mwanataaluma na hasa Profesa kamili wa Chuo Kikuu?

Mheshimiwa, Spika, Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi mbele ya Bunge lako Tukufu ya kuhakikisha kuwa mafao ya wanataaluma wanapostaafu yakaribie au yalingane na yale ya Maafisa Waandamizi Serikalini. Je, Mheshimiwa Waziri atawezaje kuidhihirishia jamii ya Wanataaluma kuwa Serikali ya CCM ni makini huku ikiendelea kutoa ahadi hewa?

Mheshimiwa Spika, mfumo wa mishahara na marupurupu ya wanataaluma nao ni mbovu, umepitwa na wakati, ni mkwamivu na hauna vivutio vya aina yoyote. Mwanataaluma mwenye kuchapa kazi, akipandishwa cheo na kuwa Profesa kamili hata kwenye umri wa miaka ya mwanzo ya arobaini, basi atabaki hapohapo hadi astaafu miaka ishirini au zaidi baadaye kwani atakuwa amefikia kiwango cha mwisho cha mshahara. Mwanataaluma huyuhuyu angekuwa nchi kama vile Japan mshahara wake ungaliweza kuongezeka toka dola 4,500 kwa mwezi hadi kufikia dola elfu nane kwani mishahara ina ngazi 32 ya nyongeza za kila mwaka. Kinachozuia Kuondoa '*bar*" – kizingiti kwamivu kwa wanataaluma wenye juhudi ni nini? Pia mwanataaluma akifanya safari na mtumishi wa Serikali, mtumishi wa Serikali yuko *'entitled'* kulipwa '*half per diem'* ambapo mwanataaluma anaweza akaomba tu *off pocket allowance* isiyozidi dola 100 za kimarekani. Kiwango hiki hakijabadilika kwa miaka 30 iliyopita. Wizara kupitia bajeti hii ina mpango upi wa kumboreshea wanataaluma wlaiofikia ukomo wa mshahara miaka mingi kuhusu kuongeza ngazi za mishahara ili kuwapa motisha?

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya vyuo vikuu vya umma hapa nchini, viongozi wa vyuo hivyo wamekwishastaafu lakini wanaendelea kushikilia nyadhifa zao. Aidha, katika baadhi ya vyuo vikuu, muda wa uongozi umeongezwa kwa Makamu wa vyuo vikuu huku umri wao wa kustaafu ukiwa umekaribia na utafika kabla ya muda wao wa uongozi kwisha. Kambi ya Upinzani ingependa kuihoji Serikali ni kwa nini utaratibu huu unaendelea kutumika kinyume na *Charters* za vyuo vikuu husika.

Mheshimiwa Spika, ushindani kati ya shule za Serikali na shule binafsi katika utekelezaji wa uchumi wa soko huria, Tanzania imeshuhudia kuongezeka kwa shule zinazomilikiwa na watu binafsi na taasisi zisizo za kiserikali kama mashirika ya dini katika kutoa elimu kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shule hizi zina mlengo wa kibiashara zaidi zinatoza ada kubwa zaidi kuliko shule za Serikali. Hata hivyo, kwa kuwa ziko kibiashara zinajitahidi kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu na hivyo kuwavutia wazazi hasa wale wenye uwezo mkubwa kifedha kuwapeleka watoto wao huko.

Mheshimiwa Spika, ili kuzifanya shule za Serikali nazo kuweza kushindana katika kukuza ubora wa elimu katika mazingira haya na kuondokana na ile kasumba ya kufanya kazi kwa mazoea *“Business As Usual”,* Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali itoe fursa sawa na vigezo sawa vya utoaji wa elimu kwa shule za umma na binafsi.

(ii) Serikali itoe ruzuku sawa ya elimu katika shule zote (za umma na binafsi).

(iii) Iundwe Mamlaka huru ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (*Tanzania Education and Training Regulatory Authority (TETRA),* ambayo itakuwa na majukumu ya kuhakiki mitaala, kuhakikisha ruzuku ya elimu inagawanywa kwa usawa na mazingira ya shule yanakidhi viwango.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, shule za umma na binafsi zitashindana kwa ubora ili ziweze kupata wanafunzi lakini pia ada zitapungua kwa kuwa kuna ruzuku ya elimu itakayokuwa inatolewa.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa wenye mahitaji maalum. Kundi la watu wenye mahitaji maalum ni kubwa lakini limesahaulika kwa kiasi kikubwa katika mfumo wa elimu hapa nchini. Pamoja na Serikali kujitahidi kujenga shule na miundombinu mbalimbali, miundombinu hiyo haizingatii mahitaji maalum ya wanafunzi wenye ulemavu. Aidha, kuna uhaba mkubwa wa Walimu na vitendea kazi kwa kundi hili jambo ambalo limesababisha wanafunzi wenye ulemavu kupata shida sana na hatimaye baadhi yao kukata tamaa na kuacha masomo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili kwamba ina mikakati gani ya dharura ya kujenga miundombinu

rafiki kwa wanafunzi hawa ili kuboresha mazingira yao ya kujifunza?

Mheshimiwa Spika, utekelezaji duni wa vipaumbele vya bajeti katika Wizara ya Elimu kwa mwaka 2010/2011 – 2011/2012. Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, malengo ya bajeti ya mwaka 2010/2011 na 2011/2012 hayakutimizwa kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, baadhi ya malengo ya Wizara katika bajeti ya 2010/2011 na 2011/2012 yalikuwa ni kufanya tathmini ya elimu kwa wote katika Wilaya 16, kuandaa rasimu ya kuanzisha Bodi ya Wataalamu wa Elimu, kuratibu mafunzo ya wasimamizi 45 na wakufunzi 360 wa kuwafundisha watu wazima kusoma na kuandika katika Halmashauri tisa (9) katika mradi wa “NDIYO NAWEZA”, kuandaa na kugawa vitabu maalumu kwa wasioona “*Braille Books* 450, kutathmini maendeleo ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi II (MMEM II) na kuanza maandalizi ya MMEM III).

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, mikakati yote hiyo niliyoitaja haikutekelezwa kabisa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili ni kwa nini mipango hiyo haijatekelezwa hadi sasa wakati fedha ya kutekeleza ilishatengwa? Aidha, Serikali ieleze fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili hiyo ilipelekwa wapi ukizingatia hivi ndivyo vilivyokuwa vipaumbele vya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2010/2011 – 2011/2012?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda Serikali ijue kwamba ni udhaifu mkubwa sana kujipangia majukumu na kushindwa kuyatekeleza.

Sasa kama Serikali inajipangia yenyewe majukumu ya kufanya bila shuruti na bila masharti na inashindwa kuyatekeleza wakati fedha ya utekelezaji ipo, je wale watumishi wadogo wanaopangiwa mambo ya kufanya tena wakati fedha haipo watafanya kwa kiasi gani ikiwa bosi wao haoneshi mfano?

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti 2011/2012. Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilikuwa ni jumla ya shilingi 659,296,862,000 ikiwa shilingi 523,778,766,000 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 135,578,096,000 sawa na asilimia 20 ya bajeti yote ikiwa ni fedha ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya maendeleo, fedha za ndani zilikuwa ni shilingi 41,098,534,000 sawa na asilimia 30.3 ya bajeti ya maendeleo na fedha za nje zilikuwa ni shilingi 94,419,562,000 sawa na asilimia 69.7 ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika licha na fedha hii ya maendeleo kuwa ni asilimia 20 tu ya bajeti yote na licha ya bajeti hii kuwa tegemezi kwa fedha za nje kwa takriban asilimia 70, bado fedha hiyo haikutolewa yote na Hazina. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012 ni shilingi 74,224,393,329 tu sawa na asilimia 55 ya bajeti ya maendeleo. Hii ina maana kwamba bajeti ya maendeleo hadi kufikia Aprili, 30 2012 ilikuwa haijatekelezwa kwa karibu ya nusu yake.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaihoji Serikali, hii asilimia 45 ya bajeti ya maendeleo ambayo

hadi Aprili 30 ilikuwa haijatumika, ilitumika yote kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha ambao ulikuwa unaishia tarehe 30 Juni, 2012? Kama haikutumika, hiyo fedha iko wapi?

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti ya elimu 2012/2013. Wizara hii kwa mwaka huu wa fedha inaomba kuidhinishiwa katika Fungu 46 jumla ya shilingi 722,471,937,000, sawa na ongezeko la asilimia 9.6 ukilinganisha na bajeti ya mwaka uliopita. Kati ya fedha za bajeti ya mwaka huu wa fedha 2012/2013, shilingi 631,890,621,000 ni matumizi ya kawaida na shilingi 90,581,316,000 sawa na asilimia 12.5 ya bajeti yote ikiwa ni fedha ya maendeleo. Hata hivyo, bajeti ya maendeleo ya mwaka huu 2012/2013 imepungua kutoka shilingi ikiwa ni bajeti ya maendeleo 135,578,096,000 mwaka 2011/2012 hadi kufikia shilingi 90,581,316,000 mwaka huu wa fedha 2012/2013 ikiwa ni anguko la asilimia 33.2

Mheshimiwa Spika, licha ya bajeti ya maendeleo kuporomoka kwa asilimia 33.2 bado imeendelea kuwa tegemezi kwa fedha za nje kwa asilimia 81.7 na pia miradi mingi ya maendeleo haijatekelezwa. (Tazama Randama ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ukurasa wa 28 na 29). Tafsiri ya utegemezi huu ni kwamba Serikali ya CCM imejitoa katika jukumu la kuwaelimisha wananchi wake na kuwaachia jukumu hilo wahisani na wafadhili.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kwa nia njema kabisa kuacha kufanya mzaha na suala la elimu kwani ndio injini ya

maendeleo ya Taifa hili. Inaweza kutegemea fedha za wahisana na wafadhili hata kwa asilimia 100 kwenye miradi mingine lakini sio katika elimu. Serikali iwekeze katika elimu kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaiuliza Serikali, kama nchi ndogo kama Rwanda iliyokumbwa na dhoruba mbaya ya vita vya kimbari mwaka 1994 imeweza kuwekeza dolo za kimarekani zaidi ya bilioni sita (6) katika elimu. Habari hii ni kwa mujibu wa Balozi wa Rwanda nchini Tanzania Dkt. Ben Rugangazi kama alivyonukuliwa na Gazeti la *'The Citizen'* la tarehe 7 Agosti, 2012. Rwanda pia hutenga 20% ya bajeti yake kulipia wananchi wake elimu kuanzia ngazi ya shule ya msingi, sekondari na huwafadhili wanafunzi wa elimu ya juu katika vyuo vikuu vya nje na ndani. Tangu bajeti yake ya 1995/1996, Tanzania imewekeza kiasi gani katika elimu hadi sasa?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge idadi ya nyie mnaotaka kuongea ni kubwa kwa hiyo muache habari ya kumuandikia SPIKA ya kwamba mnaomba mchangie kabla ya wengine, haiwezekani! Ambao hawajachangia kabisa wako watatu, waliochangia mara moja wako kumi na moja, waliochangia mara mbili wako thelathini na nne na idadi ambayo inaweza kuchukua siku mbili hizi ni ishirini na sita tu. Kwa hiyo, acheni kumuandikia Mwenyekiti kuomba kuchangia, naomba muache, hakuna utaratibu kama huo.

Tunaoanza nao sasa hivi ni Mheshimiwa Josephine Chagulla atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Hokororo.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia mchango wangu katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa leo nikiwa mzima wa afya njema kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze sana Waziri wa Elimu na nimpongeze Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya Wizarani. Ninaipongeza Serikali kwa mpango wake mzuri wa kujenga shule za sekondari za kata, mpango huu ni mzuri lakini ninaomba uboreshwe tupate mabweni ya kutosha kwa watoto wetu ambao wanakuwa mbali na shule hizi lakini pia tupate Walimu wa kutosha na maabara kwa ajili ya mazoezi kwa watoto hawa. Tatizo la ukosefu wa mabweni katika Mkoa wangu mpya wa Geita ni kubwa ukilinganisha na sehemu zingine.

Mheshimiwa Spika, mimi ninatoa masikitiko yangu makubwa kwa Serikali kwa jinsi ambavyo watoto hawa wanavyopata taabu katika kupata elimu katika shule hizi za sekondari za kata. Watoto hawa elimu wanayoipata ni nzuri lakini tatizo kubwa wanaishi mitaani na mitaani huko wanapata taabu nyingi, wanapata mimba hovyo pia wengi wao wamekuwa wakiambukizwa magonjwa ya UKIMWI pamoja na magonjwa mengine ya zinaa kutokana na

changamoto hizi ngumu za kimaisha. Ninaomba Serikali iweze kuliangalia tatizo hili na kuona ni namna gani itaweza kuwasaidia watoto hawa. Mimi ninaona ni muda muafaka kabisa kwa Serikali angalau kutumia mashirika ya umma kama vile *National Housing* kuweza kujenga mabweni katika shule hizi za sekondari za kata.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni vyuo vya ufundi, ninaishukuru Serikali kwa mpango wake mzuri kabisa wa kujenga vyuo vya *VETA* kila Wilaya lakini kuna Wilaya zingine zina *population* kubwa. Mimi naomba kwenye Wilaya hizi zenye *population* kubwa angalau kwa kuanzia tupate vyuo viwili vya *VETA* kuliko chuo kimoja, chuo kimoja hakitoshi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nina imani kuwa Serikali imenisikia na imesikia kilio changu kwa wananchi wa Geita, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninamshukuru Mwenye Mungu aliyenijalia afya njema na kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu ambayo tunaendelea nayo leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ningependa kuipongeza Serikali na pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote

wa Wizara ya Elimu kwa nzuri na hususani Serikali kwa ujumla kwa kazi nzuri inayoonekana katika taasisi hii ya elimu. Niombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri uendelee na ziara ambazo unaendelea kuzifanya na uwe ni utaratibu wa Wizara yetu sasa kwa sababu tumekuwa tukishuhudia katika ziara hizo ule upungufu mbalimbali unaojitokeza, ni wakati muafaka wa kuuchukulia hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano hivi karibuni wote tuliona katika vyombo vya habari kuna baadhi ya shule hasa shule za binafsi watoto wetu wanakatazwa kuvaa viatu lakini kama isingekuwa imefanyika hiyo ziara, ni dhahiri kuwa udhaifu huu ungeendelea kutokea. Kinachojitokeza hapa ni kwamba watu mbalimbali waliofungua shule zao za binafsi wanachukua utamaduni wao wanakuja kutuambukiza huku wakati sisi siyo utamaduni wetu wa kutokuvaa viatu, sisi kwenye idara zetu zote hasa Afya tunahimiza watoto wavae viatu. Kwa hiyo, niombe kuwa tuendelee na utamaduni huu wa kufanya ziara ili tuendelee kuona upungufu ambao umekuwa ukijitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kuchangia na niseme kuwa mimi ni Mwalimu, nilikuwa ninaomba leo niwakumbushe Walimu wenzangu. Ninayo hapa katiba ya CWT na madhumuni ya CWT katika Katiba yao kwa idhini yako, kifungu (a) kinasema kuendeleza na kulinda hadhi ya kazi ya ualimu pamoja na kusimamia viwango vya juu vya maadili. Kifungu (e) kinasema kuwahimiza Walimu kufanya kazi yao vizuri na kusisitiza waonyeshe mfano bora na hata mimi nilipokuwa chuoni nilijifunza hivyo. Leo niwaulize

Walimu wenzangu kule, hivi tumeshawahi kujiuliza ni kwa kiasi gani hiki chama chetu kinatusaidia kufanikisha haya yaliyomo kwenye madhumuni? Nilikuwa ninadhani siyo sahihi sana pamoja na madhumuni mengine lakini ni vizuri tukahakikisha kuwa hiki chama kinachosimamia mambo mengine ya Walimu kikawa na chenyewe safi.

Mheshimiwa Spika, ninafikiria kuwa niishauri Wizara ya Sheria na Katiba, ni vizuri sasa na ni wakati muafaka ikaleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria hapa Bungeni, Wabunge tukaona na tukachangia tufanye marekebisho kwa sababu Sheria inayounda CWT kwa kupitia Sheria ya *Trade Union* inayoelekeza kuwa wanachama wake wanapofikia 50% wengine wote watakuwa wanajiunga kwa mujibu wa Sheria hiyo ni kwa lazima, mimi nilikuwa ninajiuliza kwa nini Walimu wasiruhusiwe kujiunga kwenye chama ambacho wataona kinawashughulikia kwa hiari, kama ambavyo sisi humu ndani tulivyo kuna wanachama wa CCM humu kwa hiari, kuna wanachama wa CHADEMA kwa hiari na vyama vingine vya hiari. Sasa Walimu wetu kuwataka waingie kwenye hiki chama kwa lazima ninadhani wakati umefika Muswada uletwe hapa, tujadili tufanye marekebisho ya Sheria hiyo, siyo sahihi Walimu kuendelea kuwalazimisha kujiunga na chama hiki.

Mheshimiwa Spika, ni wakati pia Walimu wenzangu wangejiuliza, nilikuwa ninafikiria badala ya kuendelea kushinikizwa kufanya migomo bila kufuata taratibu, tungejiuliza ni Walimu wangapi kule vijijini kwenye Halmashauri zetu za Wilaya wanajua hata ule

mchango wanaochanga wa 2% ya lazima unatumikaje? Kwa mujibu wa Katiba hii kuna mikutano mikuu ya Taifa lakini pia kuna Mikutano Mikuu ya Wilaya inafanyika kila baada ya miaka miwili na nusu, ambapo kunajadiliwa mapato na matumizi ya baada ya miaka miwili na nusu lakini matumizi hayo na mapato hayo Walimu kule vijijini wanapewa taarifa? Hata wale wanaotuwakilisha kwenye mikutano mikuu ya Taifa hivi wanavyorudi Wilayani, wanatukusanya kutupa taarifa? Chama cha CWT kina vitega uchumi vingi lakini je, kwa nini isifike wakati tukajiuliza hivi tukipiga kura Walimu wote Tanzania hasa wale wa vijijini ni kweli kuwa wangependa kukatwa 2%? Kwa haraharaka kwa Mwalimu wa ngazi ya chini anayelipwa mshahara wa shilingi 250,000 ni bilioni moja na yule wa ngazi ya juu anayelipwa shilingi 800,000 ni zaidi ya bilioni moja kwa harakaharaka kwa mwaka mmoja ni bilioni mbili, kwa nini Walimu tusijiulize hivyo? Ninajua kuna baadhi ya Mikoa kuna vitega uchumi mbalimbali kama Arusha na hapa Dodoma imeanza lakini kwa kipindi chote cha utumishi wa ualimu hiyo 2% Mwalimu wa kijijini inamfaa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua masuala ya afya yanalipiwa kwenye Mfuko wa Bima ya Afya na huku wanakatwa na kupata huduma ya afya lakini mafao pia wanapata kwa kutumia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *PSPF,* je, baada ya utumishi, Mwalimu anapozeeka, CWT makato wanayokatwa katika utumishi wote yatawasaidia nini?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuzingatia mambo muhimu ambayo niliyachangia

katika bajeti hii mwaka jana, nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri ipo katika mchakato wa kuhakikisha kuwa Kitengo cha Ukaguzi sasa kitakuwa Wakala na hili ni jambo jema kwa sababu kitengo hiki kitakapokuwa Wakala kitaweza kufanya kazi yake ya ukaguzi kuliko ilivyokuwa sasa na hili Serikali sikivu imelisikia na inalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii sasa itasaidia ule ukaguzi tunaosema kwa kuwa ilivyo sasa tunakagua lakini unamrudishia majibu Katibu Mkuu ambaye ndiye mwenye shule, haikuwa sahihi lakini Serikali imelichukua na inalifanyia kazi, ninaipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye Katiba hii hapa kauli mbiu inasema Haki na Wajibu na mimi niombe kuwa ni vizuri tukazingatia hilo, kweli ni wajibu na haki kama Katiba ya CWT inavyosema lakini sasa tumeona Serikali imekuwa ikilalamikiwa na wakati mwingine kutukanwa bila sababu na hapa limesemwa kuwa wapo watoto wanaofaulu ambao wanachaguliwa kwenda sekondari na hawajui kusoma na kuandika, ninataka niseme hapa utafiti uliofanywa unatokana na baadhi ya Walimu wasiokuwa waaminifu na wasio wazalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimetangulia kusema kuwa mimi ni Mwalimu, ziko fomu za *TSM9*, Baraza la Mitihani linapofanya uchaguzi wa wale watoto kwenda kujiunga na sekondari wanafuata mapendekezo yaliyojazwa kwenye zile fomu. Mtoto anapokuwa darasa la tano anajaziwa fomu kuwa yeye ana urefu sentimita 120 na ana kilo 40, cha kushangaza kwenye

hizo fomu anapofika darasa la saba anajaziwa kuwa ana urefu wa sentimita 110 na kilo 30, unajiuliza hivi huyu mtoto kakatwa miguu au! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hata taarifa hizi za maendeleo ya shule mtoto anakuwa hajiwezi lakini inaonekana kabisa kuwa kuanzia darasa la kwanza mpaka saba alikuwa hafanyi vizuri, cha kushangaza darasa la saba Mwalimu anamjazia anapata alama (b) halafu yale maoni anapendekezwa aendelee na elimu ya sekondari, huu siyo uaminifu. Kwa hiyo, baadhi ya Walimu wenzetu kule hawafanyi vizuri na mimi napata wasiwasi, ninajiuliza kwa nini wanafanya hivi, kwa maslahi ya nani, hapa tunalalamikiwa kuwa tunaendelea kutowajali Walimu lakini je, haki na wajibu ambao sisi tumeahidi huku CWT tunahakikishaje kuwa unatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda hautoshi lakini kwa haraharaka niseme kuwa ninaipongeza sana hotuba ya Kamati ya Huduma za Jamii, mapendekezo yote waliyotoa kwa Serikali ni mazuri. Mimi niseme ninaamini Serikali ipo katika mchakato wa kulishughulikia hili na ninashauri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda!

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MAULIDAH A.V. KOMU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo nikawa mzima na kusimama kwenye Bunge hili Tukufu na kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni yetu sisi sote, Watanzania na wale ambao siyo Watanzania lakini wamependa kuishi Tanzania na wao pia wana haki zao. Wakati tunashika nchi hii tulikuwa tunatangaza maadui watatu, ujinga, umaskini na maradhi. Katika kuendelea kuishika nchi hii leo tumeongeza adui wa nne ufisadi.

Mheshimiwa Spika, maadui wanne hawa ambao wanaendelea kuzaliwa kwa sababu sasa hivi pia tunaikamata Mahakama, kila kitu ambacho Mtanzania atasimama kukidai kinakimbiziwa Mahakamani ili Mtanzania ndani ya Bunge lake asiweze kukihoji, hii ni hatari.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la ujinga, kama tunasema kwamba tunataka kumwondoa adui ujinga kwenye nchi hii ya Watanzania ambao walio wengi ni maskini, hawana kitu, lakini tunauondoa huu ujinga tukiendeleza kudumisha vitu vya ajabu, kuambiana vitu vya ajabu katika Bunge hili na kuambiana vitu visivyokuwa na maana. Ujinga, kuna watu waliamua wakasema kwamba kama unaona elimu ni ghali basi dumisha ujinga. Ni ghali zaidi. Kwa sababu unapelekea nchi inakuwa haina watalaam, ndiyo maana leo tunapitisha hata mikataba ya

ajabuajabu kwa sababu hatuna hao watalaam, leo *Ebola* inakwenda kupimwa nchi nyingine hapa kwetu hatuna watalaam, halafu tunakaa tunasema hapana. Maana yake mtu anachangia kitu cha maana halafu baadhi yetu tunacheka, tunacheka nini?

Mheshimiwa Spika, leo Mkoa wa Kilimanjaro tulivyokuwa tunainukia sisi tulikuwa tunaambiwa kwamba ndiyo Mkoa unaoongoza kwa elimu, lakini leo Mkoa wa Kilimanjaro Walimu ndani ya shule wanalalamika kuna wanafunzi hawajui kusoma na kuandika, sasa huko kwingine kwa watani wangu kukoje, si ndiyo itakuwa hatari zaidi!

Mheshimiwa Spika, leo bajeti ya Wizara kuna maeneo ambayo yana Kamishna ambaye anasimamia mambo ya elimu hajatengewa fedha, amewekewa sifuri, baadaye itabidi Waziri aniambie Kamishna anapata wapi hela ya kuendesha changamoto chungu nzima ambazo zimewekwa, ambazo wao itabidi wazishughulikie, wapi watatoa hela kama kuna sifuri?

Mheshimiwa Spika, ufaulu wa watoto wetu leo mwaka 2011 *percent* hamsini walipata sifuri, *percent* 38.6 walipata daraja la nne, hii inaonesha *percent* 88.6 hawajafaulu kabisa ni sifuri na daraja la nne. Waliofaulu kupata daraja la kwanza mpaka daraja la tatu ni asilimia 11.4 halafu tunaongea kwamba kuna vitu vya ajabu na vitabu vizuri vyenye sura nzuri, vyenye mambo mazuri tunaletewa vipo mezani. Tufuate basi haya yaliyomo humu ndani tuyatekeleze. Ukianza

kufuatilia hizi hotuba za Mawaziri tangu huko nyuma utakuta mambo yaliyomo humu yanaoana na mambo yaliyopo kule nyuma. Nachokiomba na nachoendelea kukiomba tafadhalini tukae kitako, tuitafakari elimu ya Watanzania, tutaondokaje kwenye ujinga wa Watanzania siyo kukaa kuchekacheka hakutusaidii kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi naamini kabisa asilimia mia kwa mia tunapolivalia njuga jambo tunaweza. Siyo kwa sababu kipindi cha nyuma tukisema sungura mdogo leo tunasema tuendelee kuvumilia, hapana! Tukiamua kitu tunaweza.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na pesa hapa tukiyaita Mamilioni ya Kikwete yalitoka kwenye mfuko upi? Tulikuja hapa mwaka jana Wizara ya Uchukuzi ikaongezewa pesa zilitoka wapi? Leo tunajenga barabara za kupitisha magari ya mwendo kasi Dar es Salaam, leo tuna maendeleo ya barabara chungu nzima hiyo pesa inatoka wapi? Kwa nini hatukai tukatafakari tukaiangalia elimu yetu, tukawaangalia watoto wetu wanakoelekea, tunajenga nchi ya wajinga, nchi ya watu mambumbumbu, tukaangalie ni wapi tutatoa pesa, tutakopa wapi, tutaomba wapi, tufanye nini ili tuweze kuikoa nchi hii na kitu kinachoitwa ujinga.

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Waziri tunaheshimiana vizuri tu, naomba sana kaka, hili ni jambo zito sana la elimu, ni nani atazungumza hapa ndani halafu aseme yeye hajapitia kwenye elimu hata

kama ndiyo Wabunge tunaambiwa tunatakiwa tujue kusoma tu na kuandika lakini ni elimu. Wengi hapa ndani wamesoma. Tusianze kutafuta sababu za kuwakorofisha Walimu.

Mheshimiwa Spika, sisi wakati tunasoma unakwenda shuleni mama anakupa mayai mpelekee Mwalimu zawadi. Walimu walikuwa wanatunzwa, Walimu wanaheshimiwa. Leo Walimu wanaposimama kudai, Madaktari wakisimama kudai, tunakimbilia Mahakamani bila ya kukaa na kutafakari mzizi wa haya ni nini? Mbona tunazungumza kuhusu posho tu na mishahara, hatuzungumzi vitendea kazi? Ina maana Walimu wanadai posho tu na mishahara lakini kwenye vitendeakazi wako vizuri kabisa hawana haja ya kudai? Mwalimu mmoja anafundisha watoto 45 hata sitini wanafika, wengine wanakaa chini, wototo wetu na wajukuu wameota vibyongo kwa kukaa chini kuandika, tunajenga Taifa la aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini hatukai tufikirie ni nini tufanye, tulete hapa kitu ambacho tutakuja kukizungumza, tutafute mchango wa wananchi waliopo kule kwenye shida, watuambie tufanye nini kuiokoa elimu yetu. Tusikae tukachekacheka hapa, tunafanya masihara na nchi hii, halafu wenzenu wanaposema wanachukua nchi hii mnakaa mnatikisa vichwa, itachukuliwa ndiyo! Kama hamko *serious* watu wakifika mahali wakachoka wanaamua kufanya lolote lile. Maana yake tunaleta nchi kwenye vita, maana yake tunaleta nchi sijui kwenye nini, kwani vita maana yake nini? Vita ni kupoteza maisha tu.

Mheshimiwa Spika, kama leo barabara zinaua, leo maji yanaua, leo wenyewe tunauana, vita maana yake nini? Hii yote ni kuchoka kwenye umaskini. Yote hii ni kuchoka kwenye ujinga, yote hii ni kuchoka na maradhi. Leo Madaktari wamegoma ni watu wangapi wamekufa hapa? Halafu tumekaa tunatikisa vichwa halafu tunasema vitu vya ajabu tu. Ufisadi umejaa kwenye nchi, hatari, tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, naomba tuzingatie kitu kinachoitwa elimu, naomba tukae kitako, Serikali yetu chonde jamani, ninyi ni wasikivu mnasema, tukae tufikirie ni kitu gani kifanywe kuiokoa elimu ya nchi hii. *Percent* kumi na moja, watu wapate *division 1-3, percent* 88 sifuri halafu tumekaa tunafanya utani hatukai tukafikiria, hatukai tukachekecha bongo zetu na sisi tumepewa akili. Wananchi wanatuangalia sisi tuliopo hapa, hawaangalii CCM hapa wala CHADEMA, NCCR, wala CUF. Wananchi wanaagalia waliomo humu ndani wanakwenda pale wanatutetea nini?

Mheshimiwa Spika, sasa tusikae hapa tukawa tunapeana vitu vya ajabu kwenye *percent* za kufeli hizi, Kilimanjaro wanasema wanao wanafunzi hawajui kusoma na kuandika, huko Lindi na Mtwara kwa watani wangu sijui itakuwaje. Tuende huko tukaangalie elimu imefika wapi, tukae kitako tuchekeche turudishe hali ya elimu ilikotokea kwenye nchi hii. Dunia nzima imejaa Watanzania wenye elimu wametoka wapi wale? Si wametoka humu humu?

Mheshimiwa Spika, leo tunajidai kuringia hii *percent* 11 inayotoka kwenye shule za seminari, hii asilimia 11 iliyopo humu daraja la kwanza mpaka *three* ni shule za seminari na *private*. Ukichekecha huko kwenye shule zetu za kata ni hatari, utalia.

Mheshimiwa Spika, ukimwuliza mwanafunzi *where are you going* anakuambia mimi ninakaa Kariakoo. W*hat is your name,* anakuambia aaha, wale mbuzi. Ukiamwambia aandike barua ya kuomba kazi, anamtafuta bibi amwandikie barua ya kuomba kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, samahanini sana siwezi kuendelea kuongea, nimechoka sana na hii nchi. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Nashukuru sana, lakini kengele ya pili ilikuwa tayari. Nashukuru sana kwa kuniachia muda na mimi nipumue.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea mchana, hii ni Wizara ya siku mbili. Kama nilivyosema walioomba kuchangia ni wengi mno, kwa hiyo nidhamu muwe nayo pia, kama uliomba, tumepanga kutokana na namna ulivyochangia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba nisitishe shughuli hizi mpaka saa kumi jioni.

**MBUNGE FULANI:** Watakaoanza?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge watakaoanza ni Mheshimiwa Thuwayba Muhammed, Mheshimiwa Margaret Sitta, Mheshimiwa Magreth Mkanga, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Godfrey Zambi inaweza pia kufikia hapo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nasitisha shughuli hizi mpaka saa kumi jioni.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa tunaendelea, kama mlivyotangaziwa mchana kwamba tutaanza na Mheshimiwa Thuwayba Muhamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na baadaye Mheshimiwa Margareth Mkanga ajiandae. Mheshimiwa Thuwayba!

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nashukuru sana kunipa nafasi hii na mimi kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu. Kama tunavyoelewa kwamba elimu ni moyo wa maendeleo ya nchi, nchi ikiwa na elimu iliyokuwa nzuri, maendeleo abadani yatakuwa ni mazuri. Lakini nchi ikiwa haina maendeleo mazuri ina maana kwamba wale watu

wake hawana elimu ya kutosha ya kuwawezesha kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia kidogo kuhusu mfumo wa elimu. Mfumo wetu wa elimu tunayotoa hivi sasa Tanzania kwa miaka hamsini, ni mfumo ambao haumfanyi mwanafunzi au kijana anapomaliza shule akaweza kujisaidia. Sasa kutokana na hali hiyo, utaona kwamba kuna ile dhana ya kumfanya mwanfunzi wetu aweze kupasi mtihani wa mwaka wa mwisho. Hii ina maana kwamba anasoma yeye kwa kupasi mtihani tu sio kwamba anasoma baadaye aweze kujisaidia yeye mwenyewe. Sasa kutokana na hali hiyo, utaona kwamba vijana wetu sisi wakitoka nje ya nchi hawawezi ku-*compete* na wenzao. Hii ni sababu ya huw mfumo ambao upo. Namwomba Waziri wa Wizara ya Elimu aweze kubadilisha mfumo huu na kubadilisha mitaala na kufanya mitaala hii iweze ku-*compete* na watu wa nchi za nje kama India, China na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sisi jamii pamoja na wazazi na Wizara yenyewe tuna dhana mbaya ambayo imetufanya tuwe katika hali ambayo tunatizama *school* gani inatoa *division one* ngapi, ikiwa *school* fulani imetoa *division one* 50, mwanangu namuhamisha kule, nampeleka kwenye *school* ile, hii ni mbaya sana. Tuangalie sasa hivi kwa kubadilisha mitaala, tuzungumze kwamba *school* gani inatoa watafiti wangapi ili tupate kuweza kuendelea vizuri.

Naomba Wizara ya Elimu ilifikirie hilo na kubadilisha mitaala yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea, nitazungumzia kidogo kuhusu somo la hisabati na kingereza. Somo la hisabati lina matatizo yake mbalimbali na hii inachangiwa na mambo mengi; mojawapo Wizara ya Elimu bado haijawa tayari kusambaza vitabu vya ziada na vya kiada kwa Walimu, pamoja na kwenye shule zote. Kutokana na hali hiyo kuwa hakuna vitabu hivi vya kingereza au vitabu vya hisabati, si rahisi Mwalimu kuweza kusomesha watoto 80 au watoto 46 kama mnavyosema sasa hivi Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 46 bila kuwa na vitabu. Lazima wawe na vitabu ili wakirejea nyumbani waweze kusoma vizuri. Mnaweza mkasema kwamba mmetoa vitabu, lakini vitabu hivi mlivyovitoa mmetoa kwa *school* za mjini tu. Je, *school* za vijijini tumeziangalia namna gani? Tufanye utafiti wa hali ya juu ili kujua namna gani somo hili tutaweza kulifundisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni vifaa vya kufundishia somo hili hakuna na kuna sababu nyingine ambayo hii ni tete zaidi, Mwalimu mwenyewe anayefundisha somo hili la hisabati, yeye mwenyewe amelifeli hapo alipokuwa anasoma, sasa vipi yeye ataweza kufundisha watoto? Vipi tutapata ile *fruit* ya somo hili ikiwa yeye mwenyewe amefeli? Haiwezekani! Sasa itabidi tumuangalie huyu Mwalimu, hata tukisema kwamba huyu Mwalimu amepita Chuo cha Uaalimu,

amesoma, amesomeshwa *methods*, lakini je anaweza ku- *impart knowledge*? Unaweza ukamkuta mtu ana *knowledge* ya hisabati lakini hawezi ku- *impart* ile *knowledge.* Sasa tuangalie namna gani tutawaangalia hawa Walimu ili tupate wale waliokuwa ndiyo hasa wa kulisomesha somo hilo. Wakaguzi nao waweze kuangalia kwa macho ya hali ya juu hasa kwa wale Walimu tunaowatoa *fresh from university*, tukawapeleka katika Vyuo vya Ualimu waende wakasomeshe, Wakaguzi waweze kuwapitia hawa mara tu wanapokuwa *posted* ili walitizame somo hili, halafu waweze kujua nani anaweza kulifundisha na nani hawezi kulifundisha *right from the beginning* sio iwe pale wakati ambao tumeshaharibikiwa halafu tena ndiyo tunahangaika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nililotaka kulizungumzia ni suala la mafunzo kazini. Kweli Wizara imetoa mafunzo mengi tu ya hisabati, kingereza na sayansi lakini kuna kitu kimoja mimi kinanitia wasiwasi na kitu hiki kinachonitia wasiwasi ni kwamba, je, *needs* za Walimu zimetafutwa? Kwa sababu huwezi kutoa mafunzo kama hujajua *needs* za Walimu ni zipi. Sasa ikiwa utajua *needs* za Walimu ni zipi, nafikiri mafunzo yatakwenda vizuri. Sasa namwomba huyu Afisa Mafunzo asikae ofisini tu aka-*plan programme* yake ya mafunzo, lakini aweze kutoa *circular* kwa *school* zote za Tanzania kutokana na zile za Kusini au Kanda ya Ziwa aweze kutoa *circular schools* zote halafu akae, a-*analyse*, atizame zile *topics* ambazo zinahitajika katika ma-*school* yenyewe, halafu na yeye mwenyewe atizame, je, hizi zangu ninazotaka kuzisomesha nazo zimejitokeza? Kama hazijajitokeza anaweza tu akatia

mbili, tatu, lakini nyingi zitoke kwa Walimu wenyewe. Sasa hapo *fruitful* ya yale mafunzo yanaweza yakapatikana ambapo *wastage of money* na *wastage of time* itakuwa haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine nilitaka kukizungumzia kuhusu Baraza la Mitihani. Baraza la Mitihani, huyu Katibu wa Baraza la Mitihani hataki kukubali wala kuamini kama mitihani inavuja. Kwa kweli mitihani inavuja, namwomba mimi afanye *survey* yake ya hali ya juu na utafiti wake, atajua namna gani mitihani inavyovuja. Haiwezi kuwa mtu wa chini apate *paper* ya mtihani kama ilivyo, siku ya mtihani inatoka ileile kisha yeye aseme mtihani haukuvuja kwa sababu eti hajapata taarifa kwamba mtihani umevuja. Ni vyema ukakaa, ukafikiri namna gani mitihani inavuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nimepata taarifa kidogo kwamba Mkurugenzi wa *IT* amesimamishwa kazi, sasa huyu Mkurugenzi wa *IT* amesimamishwa kazi kwa sababu ya kutoa matokeo vibaya ya *Islamic Knowledge*, nataka kusema, sio *Islamic Knowledge* pekee yake, lakini hata somo la *Art*, kuna baadhi ya *school* ambazo wamefanya mtihani wa somo la *Art* hawakupata matokeo. Sasa na hii pia Waziri aliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri aweze kuunda Tume kwa sehemu zote mbili ya Unguja na hapa Bara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*

*kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ashante. *(Makofi)*

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai hadi siku ya leo. Nampongeza Mheshimiwa Martha Mlata kwa kuwasilisha taarifa ya Kamati vizuri sana, nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ambao wananipa ushirikiano sana mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubishi kwamba Serikali imefanya juhudi kubwa sana katika kuendeleza elimu nchini. Imejenga shule nyingi na kwa kweli wanapaswa kupongezwa. Kitu kikubwa kilichobaki sasa hivi ni kuangalia ubora wa elimu yaani *quality* kwa kuwa *access* imekwenda vizuri. Lakini pamoja na kuangalia ubora wa elimu unaofanyiwa kazi nchini, tuangalie pia Walimu ambao ni muhimu sana katika kupatikana kwa elimu bora nchini. Kutokana na wingi wa Walimu, ndiyo sababu ya kuunda chombo kilichoitwa *Unified Teachers Service- UTS,* ili kuweka pamoja ajira ya Walimu ili wote wapate huduma kwa usawa na pia kuondoa urasimu. Baadaye ikaundwa Tume ya Walimu ambayo ni Utumishi wa Walimu yaani *TSC*, lakini kwa bahati mbaya sana Serikali ikaondoa *TSC* na ikaifanya kuwa Idara ndogo sana ndani ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi jambo ambalo limeuwa kabisa huduma kwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na chombo cha pamoja kilichokuwa kinajulikana kama *TSC* ambacho kazi zake zinafanywa na *TSD* lakini sasa kwa upungufu kwa sababu *TSD* hana uwezo, ni Idara ndogo tu. Kumekuwa na matatizo makubwa sana kwa sababu *TSD* ndiyo inayothibitisha Walimu kazini, ndiyo inayowapa namba ya usajili, ndiyo inayowachukulia hatua za nidhamu na kadhalika**.** Kwa kifupi shughuli nyingi za kupandishwa Walimu madaraja, kuthibitishwa kazini yalikuwa yanafanywa na *TSC* ambayo ilibadilishwa ikawa *TSC* yaani Idara ndogo sana. Sasa kwa kufanya hivyo, tayari walikuwa wameshagawa mwajiri pekee yake na chombo kinachowahudumia pekee yake na ndiyo hapa tatizo likawa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali irudishe *TSC. TSC* ilikuwa ni Tume ya Huduma kwa Walimu, iliyokuwa inamsaidia mwajiri katika kupandisha madaraja na mambo yote yanayohusu ajira. Mwalimu yeyote hapandi madaraja bila kupitia *TSC* ambayo sasa hivi imevunjwa na imekuwa *TSD*. Kwa hiyo, ili mwajiri aweze kumpandisha Mwalimu kwa wakati, kumuweka katika cheo kinachostahili, lazima afanye kazi karibu sana na *TSD*. Kwa hiyo, naiomba Serikali irudishwe *TSC*, itoke kule iliko ambako ilitengwa ambako haina mawasiliano ya karibu na mwajiri sasa hivi, halafu kiasi cha fedha wanachopewa hakiwawezeshi hata kufanya vikao vinne kwa mwaka ambavyo vinapaswa vifanywe kwa ajili ya kupandisha Walimu madaraja. Kwa hiyo, wako Walimu ambao wanashindwa kupanda madaraja kwa sababu *TSC*

haina uwezo wa kukaa vikao vinne kwa mujibu wa Sheria lakini mwajiri hata akiwa na *speed* ya aina gani, hawezi kumuwezesha *TSD* kwa sababu *TSD* siyo sehemu yake yeye, yuko Wizara nyingine kabisa, *TSD* iko Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi. Kwa hiyo, naomba Serikali na hasa kwa vile Serikali ya Mapinduzi ina usikivu, irudishe *TSC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati katika miaka ya themanini, wakati *TSC* kilikuwa ni chombo ambacho kilikuwa kinahudumia Walimu, ilibaki kidogo kabisa waweze kuanza kulipa mishahara ili Walimu wote wahudumiwe katika utawala wa aina moja, wathibitishwe kazini na chombo kimoja, walipwe mishahara na chombo kimoja ili kuwezesha Walimu wote wa nchi hii wapate huduma za aina moja. Narudia kuwaomba Serikali warudishe *TSC* kule huko iliko, mimi naamini hata Serikali imeshagundua kwamba ilikosea. Zamani *TSC* na Wizara ya Elimu walikuwa wanakaa pamoja kila mwaka kuangalia matatizo ya Walimu, lakini sasa hivi kutokana na *TSD* kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma hawakutani, hawazungumzi kuhusu masuala ya Walimu. Nawaomba kwa ajili ya kupunguza urasimu warudishe *TSC*. Hata ulipaji wa madeni, tumekuja kukuta kumbe kuna madeni mengine ambayo yalilipwa na Wizara ya Elimu, madeni mengine yamelipwa na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa hiyo hata hujui nani alilipa nini lakini wangekuwa chini ya chombo kimoja cha ajira, tungeweza kujua kabisa madeni ya Walimu yamelipwa kiasi gani na yamebaki kiasi gani. Kwa hiyo, naomba Sheria Na. 8 ya Utumishi

pamoja na Sheria iliyorekebisha hiyo Na. 18 ya Mwaka 2007 yaani zote mbili Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 na Na. 18 ya 2007, hizi sheria ziangaliwe upya, zifanyiwe marekebisho ili chombo cha Walimu kibaki kimoja, tutakuwa tumepunguza malalamiko mengi ya Walimu kwa sababu ajira itakuwa rahisi na tutaondoa urasimu ambao ndiyo unawafanya Walimu wapate matatizo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalotaka kuzungumzia ni suala la ukaguzi wa shule. Hakuna Mwalimu yeyote anayepanda daraja bila kukaguliwa mara tatu kwa mwaka ndipo athibitishwe kazini. Lakini sasa kutokana na fedha ndogo wanazopewa Ukaguzi hawawezi kufanya kazi, watafanya chini ya asilimia 50 ya lengo, wengi walifika asilimia ishirini. Naomba Idara ya Ukaguzi ipewe fedha zaidi, iwezeshwe kufanya kazi, iwe na *account* yake maalum. Zaidi ya yote, naiomba Serikali Idara ya Ukaguzi iwe taasisi inayojitegemea ili ipate fedha za kutosha na ifanye kazi yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyenkiti, la tatu nataka kuzungumzia suala la wanafunzi wenye ulemavu. Wanafunzi wenye ulemavu wana mahitaji yao maalum, kuanzia maadishi yao, lugha ya alama yaani matumizi ya alama, lakini zaidi ya yote jamani wanapokwenda chooni mimi ndiyo jambo huwa linanisikitisha sana, kweli wajengewe vyoo vyao tofauti. Ukifikiria mtoto asiyeona kwenda kwenye choo cha watoto wa kawaida, kwa kweli ni kuwapa adhabu kubwa sana. Naomba Idara inayoshughulikia

wanafunzi wenye mahitaji maalum iwezeshwe ili waweze kusoma vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni suala la watoto wa kike wanaopata ujauzito wakiwa shuleni. Kweli wako watoto wengine kutokana na utundu wao ndiyo wanapata ujauzito, lakini wako wengine ambao wamejikuta katika hali hiyo kutokana na jamii ilivyo na matendo ya uonevu. Je, wote hawa wanapata adhabu kwa kufukuzwa na kuachishwa masomo? Lakini kwa bahati mbaya sana wanaopata matatizo na kufukuzwa na kushindwa kuendelea na masomo ni watoto wa wazazi wasiokuwa na uwezo. Wazazi wenye uwezo watoto wao waliopata mimba katikati ya masomo wanawapeleka kusoma sehemu zingine. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie katika Sera ya Elimu ambayo inafanyiwa kazi, wapate maoni zaidi ya wadau, lakini hili suala la watoto wa kike wanaopata mimba, wasiachwe hivihivi, waendelezwe kwa utaratibu wowote ambao itaonekana inafaa hapa nchini. Lakini pia tujifunze kwa majirani, twende Zambia, Malawi ambako wanaruhusu watoto baada ya kuzaa wanarudishwa shuleni kwa utaratibu maalum uliowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mihula ya shule za sekondari. Tuseme ule ukweli, mihula ilivyobadilishwa *form five*, mimi napendekeza turudi kwa utaratibu wa zamani kwa sababu utaratibu huu ulioko sasa hivi, Walimu wanavyomaliza kusahihisha mitihani ya kidato cha nne, mara wanajikuta tena wanaingia kwenye kusahihisha mitihani ya kidato cha

tano na kuwafanya muda mwingi wawe wanasahihisha kuliko kuwapa nafasi ya kutosha ya kufundisha. Naomba mihula hasa ya kidato cha tano ibadilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi sana katika Wizara ya Elimu, lakini mimi nafikiria kitu kizuri sana ambacho kinaweza kuharakisha utatuzi wa yote haya kama nilivyosema mimi kwa upande wa Walimu ni kuwa na chombo cha kuhudumia Walimu yaani Teachers Service Delivery kwa sasa hivi ni mbaya, tujitahidi tubadilishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono taarifa kama ilivyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii kwa sababu mimi ni mjumbe, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kiasi kidogo Wizara hii na mambo yake ambayo ndiyo tumewasilishiwa asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze alipoanzia Mheshimiwa mwenzangu wajina. Mimi ni Mwalimu kwa *profession* na mpaka kesho kutwa mimi ni Mwalimu. Yaliyosemwa ndiyo yalikuwa yananisibu au ndiyo tuliyokuwa nayo yaani si mgeni sana katika hayo. Ni kweli kuondolewa chombo kile imekuwa tatizo na tusishangae tukajikuta kila siku tuna vuruguvurugu tu kwa sababu chombo kile si tu kwamba kulipa lakini

ilikuwa pia ni sehemu ya nidhamu. Unaandikiwa barua na wao wanakukanya, unajirekebisha. Sasa chombo cha kudhibiti hiyo nidhamu kiko wapi? Kwa hiyo, mimi ninaunga mkono kilichosemwa pale kwamba jamani kukosea sio vibaya lakini pia ukirudi nyuma kwani kuna ubaya gani? Ndiyo vizuri zaidi kwa sababu wakati mwingine katika kusonga mbele lazima ukosee ndipo urudi urekebishe. Kwa hiyo, kile chombo kirudi, hata kama kitarudi kwa *style* tofauti lakini kazi zake ziwe zile na chini ya Wizara hii kwamba sasa hawa Walimu wanakuwa pamoja; mwajiri na wewe wa kukudhibiti inakuwa sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulichangia hapa, mimi nawakilisha watu wenye ulemavu, kwa hiyo, ndani ya elimu siwezi kucheza nje ya masuala ya wanafunzi, watoto wenye mahitaji maalum. Nimeshukuru nimepata taarifa hapa kwamba shule zinazohudumia watu hawa zimeongezeka kutoa 35 mpaka 39 na watoto wenyewe wameongezeka wako kama thelathini elfu na kitu hivi na vyuo vikuu huko watasaidiwa sijui **wanafunzi mia moja.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu bila Mwalimu aliyeandaliwa sawasawa ni *zero,* hakuna kitu. Tutakuwa na wanafunzi tutakuwa na vifaa, bila kuwa na Mwalimu aliye mahiri, kuelekeza vifaa hivyo vitumikeje na mwanafunzi huyu aende vipi, ni hamna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio changu. Walimu wa Elimu Maalum wengi hasa kwa *level* ya *Primary School,* wanajitolea wenyewe kutoka makazini kwenda kusoma Patandi au sijui wapi au wapi, kuji-*up grade.* Kinachonisikitisha hawa, hawataongezeka wakakidhi mahitaji ya hata hizo shule zinazoongezeka kwa sababu, baada ya kujisomesha wenyewe, wakirudi kwenye Vituo vyao vya kazi ambako ndiko walitoka, wanapanguliwa, wanapelekwa kwenye shule ambazo sio hata za wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai, wengine wanapata *promotion,* ili mradi tu. Sasa hii idadi haitatimia. Kwa misingi hiyo, watoto hawa wataendelea kutopata elimu inayokidhi haja yao kabisa na uwezo wao, kama walimu wenyewe hata wanaojitahidi kujiandaa wanahamishwahamishwa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndio wale wako *victims* kwa kazi nzito wanayoifanya. Anafundisha na kuwa mlezi hapo hapo, anambeba mwenyewe, huyo huyo ndio amrudishe kwa mzazi, kesho ndio amlete darasani, Walimu hawa wanavyojitolea jamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana wanafanya kazi ya Mungu. Ndio hawa ambao hawapati *promotion* wakirudi, ndio hao hata mazingira magumu ya ufundishaji, ndio hao ambao hata kwa posho ya ziada hawaangaliwi; maana mtoto anatoa udenda, wewe unabaki hapo kumfuta wenzake wameshapepea nyumbani, hawaangaliwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hiki kinanisikitisha, nitaendelea kusema. Pamoja na walimu wengine wote kuwa na matatizo, lakini hawa wana matatizo zaidi jamani, waangalieni na wao, sio wengi kwamba, labda bajeti, fedha zitakwisha, sio wengi. Kazi wanayoifanya ni ya Mungu, hebu tuwaunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu ameshasema, mimi nimeshasema na nitaendelea kulia hivyo hivyo; mazingira yasipokuwa muafaka kwa mtoto mwenye ulemavu wa aina yoyote, akili hiyo anaitumia kwa nguvu zaidi ya ziada kwa sababu ya vikwazo vya kawaida, vyoo hakuna. Tuliopita hapa walikuja watoto kutoka Tanga, yule binti alisema mwenyewe; wanashika chini huku, kweli ni afya ya wapi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanaoweza kutambaa, haya; wale wanaokwenda na viti vyao, sijui? Yaani, kila siku naongea kuhusu ramani tunazotoa, naambiwa wajenzi tunawaambia. Hivi kuwaambia tu, mnawakagua na kweli mmezitoa au ni basi tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani mambo mengine ni ya kawaida sana sana, hayahitaji hata pesa. Basi ni kuyachunguza na kuyahimiza yafanyike. Watoto wale wanapata shida, wengine wanaachilia mbali kusoma, hata kama Mungu, kidogo aliwaruhusu huku kichwani kuweza kuelewa vitu, wanakata tamaa. Anapata na magonjwa mengine. Sasa hii haki ya elimu inakuwaje, ni nini hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, jamani kwa elimu maalum, kubalini kutumia fedha au gharama ili wenye ulemavu hawa na wao waweze kujitegemea. Kwanza, mnapowaacha solemba solemba, ndio wanakuja kuwa wa barabarani baadaye, nani anataka kuzagaazagaa barabarani jamani? Nani anataka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuwa mzigo zaidi wa mzazi; mzazi amekosa au ameingia kwenye janga kwa kupata mtoto mwenye ulemavu? Wengine wanazaliwa wazima, wanapata ajali, wanaumia na kumbukeni, hujafa hujaumbwa. Tufanye wajibu wetu kwa sekta hii ya watoto, kwanza sio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, nimefarijika watapewa huduma sijui huko wa Vyuo Vikuu, inasikitisha mpaka sasa hivi hawa wa Vyuo Vikuu wenye ulemavu, hawapati ajira. Bado jamii na waajiri wanaona wenye ulemavu hatufai, hatuna maana; si kweli. Ukimpa kazi akafanya, anajua mimi msaada wangu ni kazi hii na chochote nilichonacho, anafanya kazi kwa bidii, sasa hatupewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Interview,* ukifika kwenye *interview,* tena sasa hivi kuna kile sijui chombo cha kuajiri peke yake, mimi nadhani hata kile hakina *disability,* yaani huoni u-*disability,* hakuna kabisa kwa sababu, wana-*apply,* hawapati. Mimi sasa hapa naombwa hivi, mama tutafutie kazi, wapi na wapi? Ninawaombeni sana, wale ambao wanakidhi haja

jamani, wana uwezo, wapeni, wajaribuni, wakishindwa ndio muwafukuze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulichangia hapa, kuhusu hawa watoto wenye ulemavu. Hawa ni kwamba, katika ngazi ya *Primary School,* pana matatizo sana kwamba, hesabu hawasomi, Sekondari hasa, hawasomi wasioona, mimi wananilalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na Mwalimu ambaye alijitoa wakati fulani, alikuwa anafundisha Tanga. Wajina wangu samahani, sikuweza kuku-*consult* mapema, lakini tunamfahamu. Alijitoa huyu Mwalimu asiyeona, akatafsiri vitabu hivi vya kufundishia hesabu kwa lugha ile ya nukta. Hivi ile *program* imekwenda wapi? Wanakosa kufanya mitihani, basi wanashuka kwa sababu, ile hesabu wanahesabiwa kwamba, hawakufanya. Jamani ni uonezi, wapeni nafasi, washindwe wenyewe, lakini wapeni nafasi, wanaweza, wanamudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi katika suala la watoto wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vifaa. Sasa kama mtaweza kuwapata Walimu wa kutosha na wanafunzi wanaongezeka na hii ni kushukuru ni hamasa za wazazi, wanajua kwamba, kumbe kumficha mtoto haina maana, wewe msukume. Kesho anaweza akaja akawa ndio Waziri wa Elimu huyo huyo na miguu yake ngwende ngwende ngwende na macho yake yasiyoona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona nchi nyingine wana nafasi nzuri tu, wana uwezo vifaa, lakini, ili wamudu yale masomo, pamoja na huyo Mwalimu, *braille* kwa wasioona, shinikizo za masikio sijui kwa wale wenzangu viziwi, msiseme wasiosikia wasiosikia ni mtu sugu, viziwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, lakini naomba haya mwakani nisiyasemee tena. *(Makofi*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa, napenda niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kueneza mtandao wa shule za msingi Tanzania nzima na shule za sekondari Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipotea njia Tanzania hii, tafuta kibao kinachokuonesha shule. Hongereni sana Wizara ya Elimu, hongereni sana sana sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, lazima tusema ukweli. Kila unapokwenda unakuta mtandao wa elimu, yaani shule ya msingi, sijui Chuo cha Ualimu, hiyo sio kazi ndogo. Lakini napenda niipongeze Serikali, kwa wingi wa wanafunzi walioko Chuo Kikuu. Leo Dodoma nzima imetapakaa wanafunzi, hii ni kazi ya nani kama sio kazi ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi? Kazi ya nani kama sio ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi? Naipongeza Serikali ya Chama changu na naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi zangu za dhati, napenda pia nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Walimu wenzangu wote ambao hawakushiriki katika mgomo. Walimu wenzangu, nilikaa katika dawati hili hili nikawaambia, Walimu wenzangu, msidanganyike. Leo Walimu wenzangu hamkuchukuliwa kwenye sensa, mnahangaika. Sensa, ilikuwa inatusaidia kama Walimu, lile dodoso kwetu tumelizowea, halitusumbui. Sasa Walimu wenzangu, mmeingia kwenye majaribu ya kuingia kwenye mgomo. Hili suala la sensa ni la Kitaifa, hivi leo ni nani atakuwa na uhakika kwamba, wewe uliyegoma hutagoma tena katika siku ya sensa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Walimu wenzangu, hebu tutafakari kwanza. Tukae chini tutafakari, tuangalie kuna nini, tuangalie kuna nini kinatakiwa au Walimu hawa, wanatutakia heri kweli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu nitajikita katika maeneo yafuatayo; kwanza nitakizungumzia Chama Cha Walimu, pili nitazungumzia matatizo ya Walimu na tatu nitazungumzia matatizo ya wanafunzi na mwisho kabisa nitaishauri Serikali yangu sikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nikianza na Chama cha Walimu. Chama cha Walimu, kazi yake mojawapo ni kuwaunganisha Walimu na kuwasemea matatizo yao. Mimi napata kigugumizi na sielewi kabisa jinsi gani Walimu na hasa Walimu wa Shule ya msingi tunadhalilishwa hovyo hovyo hivi. Leo Walimu tunaonekana wa Shule za Msingi kwa kuwa, wototo

wamefeli, sijui watoto hawajui kuandika na kusoma, tunasemwa, tunaonekana hatuna maana na tunadhalilishwa; hii si kweli na hii si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu wa Shule ya Msingi ndio daraja. Wote hapa tulitoka shule ya msingi ,tukaenda sekondari, uwezo wetu katika shule ya msingi, ndio uliotupeleka sekondari na kutufikisha kwenye Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwa nini, Mwalimu wa Shule ya Msingi, amekosea tu, kitendo cha mwanafunzi mwenyewe kwenda kule hajui kusoma, mzazi wa mwanafunzi anatoka na mwanafunzi kamshikilia mkononi, anakwenda naye kwenye magazeti au kwenye redio, mimi mwanangu hajui kusoma na kuandika. Hukumu ya mwanafunzi iko kwa Mwalimu na mzazi; wewe mzazi kama unaona mwanao hajui kusoma na kuandika na Mwalimu akathibitisha, futa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara yangu iangalie, ifanye kazi zake. Tunaingilia mno kazi za Serikali, jamani mpaka Serikali inashindwa kufanya maamuzi. Mbona Vyuo Vikuu jamani watu wanadesa, wanakamatwa hovyo? Mbona hawatangazwi? Lakini Walimu wa Shule ya Msingi, kila siku.

Mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri wangu na Wizara yangu, fanyeni kazi yenu, msitusikilize sisi wanasiasa. Fanyeni kazi yenu na Walimu mfanye kazi yenu, msitusikilize wanasiasa sisi, tutarudisha nyuma hili gurudumu la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, hiyo hali ya kufeli kwa wanafunzi, hebu angalia dawati kama hili ninalokaa mimi, wanakaa watoto wawili siku ya mtihani, wataacha kutazamiana hapa? Hapa wataacha kutazamiana? Lakini hii yote, hukumu hii inamwendea Mwalimu wa Shule ya Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wamehukumiwa, wameshushwa madaraja, wengine wamepelekwa Mahakamani. Leo mimi nasimama hapa kwa uchungu kwa niaba ya Walimu wenzangu wote wa Shule za Msingi, naiomba Serikali, iangalie adhabu iliyowapa Walimu, wawaondolee. Wanafunzi wameadhibiwa na watafanya mtihani mwaka huu, lakini Walimu, wataendelea kuadhibiwa, wameshushwa madaraja, watastaafu vibaya. Naomba jamani, ile ni ajali kazini, wasameheni Walimu. Muwasamehe walimu, kwa adhabu waliyoipata inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano wa dhati. Kuna Mwalimu mmoja, anaitwa Mwalimu Manoni, alipeleka wanafunzi Manyara, Singida, kote huko wanamjua, anapeleka wanafunzi wake wa darasa la saba, ana mchango mkubwa wa elimu katika Mkoa wa Dar-es-Salaam, lakini leo Mwalimu Manoni amepewa *demotion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wangu nilikuwa nawaambia mwenyewe, hebu nendeni kwa Manoni mkajipime, mkiona mmepata 40, huko au 45, nina uhakika mtakwenda Sekondari; leo Manoni kwa kosa dogo, ameadhibiwa na Walimu wengine wote wa

shule za msingi. Tunawaona Walimu wenzetu, yaani Walimu wetu tunawanyanyasa na hatujui hiki kitu kinatoka wapi jamani? Si kweli, watoto wakafeli hivi. Kila siku hamna maneno, maneno Walimu wa Shule ya Msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Bunge hili, leo iwe basi, waachwe. Muwaache Walimu wafanye kazi zao, tunawaingilia mno, eeh! Kama Mwalimu amekosea, kuna vyombo vya kumuadhibu Mwalimu, lakini sio Wanasiasa tunayumbisha, mara huyu hivi na hivi, hiyo isiwepo tena. Walimu nao watu na wanastahili heshima. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nije kwenye mchango wangu kwa Chama cha Walimu. Haya ninayoyasema hapa, ndio kazi ya Chama cha Walimu, kuwasemea Walimu, leo Mwenyekiti gani wa Chama cha Walimu aliyewasemea hawa Walimu? Walimu wanaadhibiwa, wanapigwa mpaka na wanafunmzi wao. Walimu wana maisha magumu, alichokiona yeye Mwenyekiti wangu ni kuanzisha mgomo, mgomo si suluhisho la matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgomo sio suluhisho la matatizo. Nawaomba hao Viongozi wangu wa Chama cha Walimu, na mimi ni Mwalimu pia. Naongea, yaani naomba ku-*declare,* huyo Kiongozi wangu wa Chama cha Walimu, hebu akapange *plan* zake vizuri; kuna *plan one* Mgomo, *Plan two* Kuwaacha Walimu hewani? Sensa hakukubalika, sehemu yoyote hatakiwi, yeye anawaacha hewani, ndio *plan* yake namba mbili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo sivyo, hivyo sivyo; *plan two,* hebu ajijengee uwezo, kama Chama *CWT* kipo na kinapata fedha nyingi, kiangalie jinsi gani ya kuwasaidia Walimu wake, jinsi ya kupunguza makali ya maisha. Kiwasaidie wakajenge uwezo kwa Polisi na Wanajeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi ni mfano wa kuiga, nimekuta wana tangazo, leo Kambi fulani sijui itapewa sukari kwa bei nafuu; hivi Chama cha Walimu na hizi hela, leo Kambi fulani itapewa madawati kwa bei nafuu, Chama cha Walimu kinangoja nini kutufanyia hivyo? Ni aibu, Mwalimu anapokufa *CWT* inatoa Sh. 100,000/=, Chama Cha Walimu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu toka naingia ualimu ninakatwa hela zangu 2% mpaka leo na uzee huu na miaka 50 na miaka 35 ya kufundisha. Kama hujafa, basi hujaionja wewe hela ya Mwalimu; hivi kweli hii jamani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie ukweli. Waheshimiwa Walimu wenzangu tutafakari, haya mambo sio. Naungana na Mbunge mwenzangu Hokororo, ifike sehemu sasa hiki Chama kiwe cha hiyari. Bora hela yangu nikaiweke bima, itakuja kunisaidia au nikaiweke *NSSF,* kuliko kuweka kwenye hiki Chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama hakina msaada, msaada wake ni kuwashawishi Walimu waende pabaya? Hii si sawasawa. Niombe kibadilishe mwelekeo leo. Chama changu kama kinaelekea kweli,

kibadilishe mwelekeo, kiwasaidie Walimu kwa ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye matatizo ya wanafunzi. Wanafunzi nao wanaadhibiwa pasipo adhabu. Kama ninavyosema hili dawati moja wanakaa wawili. Lakini teknolojia imekuwa, watoto watundu, lakini pia sisi wanasaikolojia hatuamini kwamba, kuna mtu asiye na akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwanafunzi au kila binadamu aliyeumbwa na Mungu, ana akili kichwani. Kwa hiyo, yule anaweza hata kumuibia mwenziwe mtihani, ni akili na ile ni kukua teknolojia. Hivihivi huwezi ukaiba mtihani wa mtu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko Mwanasayansi mmoja ambaye anarusha hata ndege anaitwa Ensem, yeye mpaka anafika darasa la nne, hawezi hata kuzungumza lugha ya kwao. Lakini leo yeye ndiye mwanasayansi maalum na ndiye anayefanya vitu vizito vizito. Kwa maana hiyo, tusiwahesabu watoto hawa kama wajinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwadhalilishe, mtoto wako ukimwimbia wimbo mbaya atakuwa mbaya. Hebu tuwaache hawa wanafunzi, tutafute lugha ya kuwaambia. Hivi kuwambia watu wamefeli, sijui wamefanya hivi, mara nini, sio vizuri jamani. Hii ni nini? Ni siasa au nini? Mimi nashindwa kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niishauri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa*

*muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Tayari?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa dhati kabisa kwa kunijalia mimi na Wabunge wenzangu wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo hii kuwa tupo hapa katika hali nya afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, pia sina budi nikushukuru wewe Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Elimu, ambayo iko mbele ya Meza yetu hii. Kwanza kabisa, nitajikita kidogo katika suala la madai ya madeni ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya Walimu, kwa Taarifa Rasmi ya Wizara, hadi kufikia Novemba 2011, yamefikia kiasi cha shilingi bilioni 7,177,043,245.6/=. Deni kama hili linavyojionesha, inaonesha dhahiri kwamba, si kwamba utendaji wa Waziri pamoja na Naibu Waziri una makosa, bali matatizo haya yatakuwa yanasababishwa na Serikali, kwa upande wake. Kwa kweli, madeni kama haya ni kitendo kinachorudisha

nyuma maendeleo ya nchi hii, kuhusiana na suala zima la elimu, ukizingatia umuhimu wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu ni kiungo muhimu sana katika Taifa letu au Taifa lolote duniani. Lakini cha kusikitisha, madeni haya ya Wizara ya Elimu yanafikisha mahali kuweza kusababisha matatizo, ikiwemo migomo, vurugu mbalimbali ambazo zilisababishwa na madeni, ambayo ni stahili za wafanyakazi, hususan Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni haya yaliundiwa Tume Maalum kuchunguzwa na ikapatikana idadi hii. Tume hii baada ya kuwasilisha taarifa yake katika Wizara, madai haya yanagawika katika sehemu mbili kiubwa, sehemu moja ni malimbikizo ya mishahara na sehemu ya pili ni malimbikizo ya stahili za posho na stahili nyingine zinazowahusu wadau hawa wanaoshughulikia suala zima la elimu, yaani Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa upande wangu binafsi, naishauri Serikali, ichukue hadhari sana na suala hili la madeni. Japokuwa tayari katika fedha hii nusu ya fedha imeshatolewa na kuandaliwa malipo kwa wahusika, lakini ichukue tahadhari na ile ahadi iliyoitoa muda wake wa kulipa madeni yaliyobakia waweze kutekeleza ahadi hii kwa wakati wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dhahiri kwamba inaonesha, aibu kwa sababu tukiangalia suala la elimu ni suala ambalo haliwezi kujionesha kama liwekwe katika nafasi nyingine au nafasi ya nyuma katika nchi yoyote. Tegemeo letu ni kupata Walimu wazuri na

kupata wanafunzi wazuri ambao watakuwa tegemeo la maendeleo ya Taifa letu baadaye lakini watoaji wa elimu inaonesha dhahiri wanaweza wakavunjika moyo na ikawa elimu hiyo haiwezi kupatikana hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara husika kupitia Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, ule umahiri wao wa kushughulikia suala hili la elimu kwa kupitia na kufanya ziara mbalimbali za kuangalia maendeleo ya elimu waendelee nao. Vile vile Kitengo cha Ukaguzi wakipe nafasi yake maalum ya kukitengea fungu ambalo litatosha katika kuifanya kazi hii iwe rahisi ya kushughulikiwa na hao wakaguzi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudi kuelezea changamoto zilizopo kwenye Wizara ya Elimu. Changamoto zilizopo katika Wizara ya Elimu ni nyingi na ni za kupigiwa mfano. Walimu stahili zao zinakuwa hazipatikani kwa wakati jambo ambalo linawafanya wasiweze kumudu kazi zao kikawaida. Changamoto nyingine ni kuhusu vifaa vya kutendea kazi katika shule, hakuna au ni duni kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile changamoto nyingine inayoikabili Wizara kwa upande wa Walimu ni kutopatikana Walimu ambao wana uwezo katika sehemu za msingi katika kushughulikia suala zima la utoaji wa elimu kwa sababu matokeo kila yanavyojionesha yanaonesha kudidimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoka hapo na naomba Waziri atakapokuja katika majumuisho atueleze kwa sababu tunakumbuka kama Wizara

iliunda Tume kushughulikia suala la *NACTE* kupitia mitihani ya *Islamic knowledge*. Kwa hiyo, baada ya kuunda Tume hiyo kuna taarifa zilizopatikana kwamba kuna mtendaji mmoja katika Wizara katika shughuli za *Computer* amesimamishwa. Kwa hiyo, namwomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho suala hili aliweke wazi ili tupate kuridhika, aturidhishe katika Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya Walimu ni mengi, lakini naomba niishauri Serikali mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia stahili za Walimu za posho zao wapatiwe kwa wakati. Pia, naomba niishauri Wizara isimamie vizuri masuala ya stahili za Walimu kwani ndiyo yanayosababisha matatizo yote yanayopelekea mpaka kufikia Walimu kugoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kabla sijasahau, naiomba Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa James D. Lembeli na Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa ajiandae.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii ili na mimi kwa siku ya leo niweze kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu na ni hoja ambayo kwa kweli Watanzania wote sasa hivi wanataka kusikia Waheshimiwa Wabunge wanasema nini kuhusu mustakabali wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema kwa kifupi sana kwa sababu hoja yangu hasa itajikita katika hali ilivyo hivi sasa hapa nchini kuhusu elimu. Lakini nimekuwa nikijiuliza kwa muda mrefu Watanzania walikuwa wakiimba nchi yetu ni nchi ya Ujamaa na Kujitegemea. Watanzania walikuwa wakiimba wimbo kwamba nchi yetu ni ya wakulima na wafanyakazi. Sasa *slogans* zote hizi ziko hoi, chali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa pamba wako hoi wanalalamika, wakulima wa kahawa matatizo hayo hayo, wakulima wa korosho matatizo ni hayohayo na tunasema nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi. Sasa wafanyakazi nao ni mchezo huo huo wa kilimo, wako hoi, migomo kila kukicha! Sasa Serikali inasema nini? Nashindwa kuelewa ni kwa nini Serikali ambayo iko madarakani kwa niaba ya wananchi haiwasikilizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha juzi cha Serikali kukimbilia Mahakamani kuwashtaki wafanyakazi ambao ni Walimu kwa kweli ni kitendo ambacho tusema ukweli Walimu wanatakiwa kusaidiwa, hawatakiwi kubezwa, kuzomewa wala kupelekwa Mahakamani. Ni sawa na baba ndani ya

nyumba anagombana na mama na watoto halafu yeye ndiye anakuwa mtu wa kwanza kwenda Polisi kuwashitaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusidanganyane, Walimu wamerudi kazini lakini hawafanyi kazi, nchi nzima. Kwa hiyo, Serikali inajifurahisha kwamba mgomo haupo makazini, hawa watu hawafanyi kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge, nataka niseme, mshahara wa sh. 250,000/= kwa Mwalimu anayeishi hapa mjini Dodoma ataishije? Kama sisi Wabunge tunalalamika kwa nini hatuwatetei Walimu? Nafikiri iko haja kwa Serikali kukaa chini na kuzungumza na Walimu, Madaktari na wakulima kwa sababu wao ndiyo wameiweka Serikali madarakani, sasa mimi nakuweka madarakani halafu asubuhi unakwenda kunishtaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya kufichaficha mambo imekwisha. Mimi nitazungumzia uzoefu nilioupata wakati nikifanya kazi Ujerumani Mashariki, kabla ukuta wa Berlin haujabomoka. Naona hali inakuwa ni hivyo hivyo kana kwamba hatuelewi na hatuoni hawa watu wetu wana matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawafanyi kazi, ukiona meseji wanazopelekeana. Sasa Serikali inaposema kwamba mgogoro umekwisha njooni mezani, basi ianze Serikali yenyewe kuwaita wakatae wenyewe. Ukifumbia macho ugonjwa, kilio kitakuumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona hili ni tatizo kubwa, nikimaliza kikao cha Bunge nitakwenda kijijini, nitawaambia nini Walimu? Kwamba ninyi ni wakorofi? Halafu wanasoma kwenye magazeti kila siku mimi nadai posho zaidi, mbona mimi sijapelekwa Mahakamani? Tufikie mahali tukubali ukweli kama pesa haipo basi waambiwe haipo, kila mtu ajifunge mkanda, lakini siyo wengi wajifunge mkanda wachache wanufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mazingira haya huwezi kusema kwamba nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi bali ni ya watu tofauti. Naona nchi hii ni ya wafanyabiashara, matapeli na wahuni kwa sababu ndiyo wanaoweza kufanikisha mambo yao yaende vizuri. Kitendo cha Walimu, Walimu wana matatizo makubwa na Serikali yetu isipowasaidia wataendelea na mgomo mpaka mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali iko sawasawa kwenye hospitali, vijijini wananchi wanahangaika hawapewi dawa wala hawapewi kitu chochote, Serikali inasema Madaktari wamerudi hospitalini. Kama mtoto wako ni mgonjwa ukimpeleka *KCMC* unampeleka kufa kwani hawafanyi kazi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nimezungumza haya kwa sababu nasema ukweli na msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Nataka kusema ukweli na ukweli unauma. Walimu tuwahurumie, Walimu ndiyo waliotuchagua kuja hapa Bungeni, sasa kama leo utasema hawa ni wahuni na kadhalika, hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nitasema machache lakini nataka nimsikie Waziri wa Elimu aseme na aeleze kwamba nchi hii sasa ni ya watu gani? Ni nchi ya wakulima na wafanyakazi au ni ya watu wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lembeli kwa mchango wako na sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa na Mheshimiwa Mary Chatanda ajiandae.

**MHE. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, nami ni Mjumbe katika Kamati ya Huduma za Jamii, hivyo naiunga mkono hotuba iliyotolewa kwa Kambi ya Upinzani na naiunga mkono hotuba iliyotolewa na Kamati kwa sababu na mimi nilishiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekeze mchango wangu kuhusiana na elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na wimbo mzuri tu tukisema kwamba, tunatengeneza ajira kwa vijana wetu, tukisema kwamba tunataka tuwaondolee

umaskini vijana wetu lakini hali hii imekuwa haitekelezeki na hali hii imekuwa haiwezekaniki kwa lugha nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kulikuwa na mpango mzuri wa kujenga vyuo vya *VETA* ambavyo vingewasaidia kuwajengea uwezo vijana wakajiajiri wenyewe wakaondokana na dhana ya kutegemea kuajiriwa. Leo hii tunategemea vijana wetu wengi wanaomaliza kidato cha nne hawana sehemu ya kwenda tofauti na wale wachache ambao wanapata kwenda kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika wanaomaliza kidato cha sita wapo wengine wanaobaki ambao hawapati nafasi ya kuendelea na chuo kikuu, hao watu tutawaweka wapi? Hao watu wana ajira gani na wameshajenga mazingira ya kwamba lazima waajiriwe, suluhu pekee ni kuwajengea vyuo vya *VETA* ili kusudi waweze kupata ufundi ambao utawasaidia kujiajiri wenyewe na waondokane kuwa tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikipitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri imenichanganya na naomba labda anisaidie. Wakati nikisoma katika ukurasa wa 35 katika mipango iliyokuwepo katika hotuba ya mwaka jana inaonekana kuna vyuo ambavyo vilijengwa na nitaongelea chuo cha Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *paragraph (f)*, inaonekana kwamba chuo hiki kimekamilika kwa 98%,

lakini ukifungua kitabu hiki cha hotuba ambacho amekisoma leo Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 57 *paragraph (b),* inaonekana kimekamilika kwa 75%, sasa kuna vyuo viwili au ni chuo kimoja ambacho kimejengwa katika mazingira haya? Naomba Waziri anipe jibu atakapokuja kuhitimisha, ni chuo kipi ambacho kimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado katika kitabu hiki cha hotuba ukienda ukurasa wa 84 inaoneka mpango uliopo mwaka huu ni wa kujenga vyuo vinne katika Mikoa minne mipya na Wilaya nne. Hii kwa kweli inakuwa si sahihi. Kama tutakwenda kwa utaratibu huu vijana wetu hatuna jinsi ya kuweza kuwasaidia kupata ufundi na kuweza kujiajiri wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango wa kuendeleza vyuo vya *FDC,* lakini sijaona mpango mkakati uliopo ni vyuo vingapi ambavyo vimewekewa bajeti na ni vyuo vingapi ambavyo mnategemea mwaka huu vitaweza kufanyiwa kazi ili kusudi viweze kuchukua wanafunzi na kuwafundisha au kuwapa mafunzo ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tupate mpango mkakati kuhusu *FDCs* zilizoongelewa, ni zipi zitakarabatiwa na ni zipi zitajengwa na mpango wa kuwachukua vijana ukoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la kufuta ujinga. Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusu takwimu mbalimbali tu za vijana ambazo sasa

wanaonekana kuna mambo makubwa mawili. Hatua ya kumaliza darasa la saba na hatua ya kujiunga na kidato cha kwanza bila kujua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna kundi la watu ambao wako nje ya mfumo rasmi wa elimu na huko tuna takribani 30% ya watu wasiojua kusoma na kuandika katika vijiji vyetu na katika miji yetu. Watu hawa kulikuwa na utaratibu wa kuwasadia angalau waweze kujua kusoma na kuandika. Leo hii Walimu waliokuwa wanajitahidi kufundisha, inasikitisha kuonekana kwamba japo posho yao ni ndogo ambayo wanapaswa kulipwa lakini hawalipwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Walimu wa MEMKWA na Walimu ambao walikuwa wanafundisha program ya MUKEJA lakini Walimu hawa bado wanadai posho zao kwenye Halmashauri nyingi na hawalipwi. Inakuwaje jamani tusiwalipe watu hawa? Watu hawa wanajitolea, wanafanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbaya zaidi hata ukienda kwenye Halmashauri zetu ukaomba tu kwa Afisa mhusika kwamba, naomba idadi au orodha ya Vituo vya MEMKWA vilivyopo vinavyofanya kazi ni vingapi, orodha hiyo haipo! Ukitaka kujua vituo hivyo vimefanyaje kazi, hakuna taarifa wala takwimu, hivi tunafanyaje kazi katika hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa suala hili liangaliwe kwa ukaribu sana, kama kweli tunataka kupunguza kiwango cha kutokujua kusoma na kuandika, basi vigezo hivi tuviangalie. Haiwezekani leo

hii tumlaumu mtoto ambaye ameshindwa kujifunza kusoma na kuandika na amepelekwa *form one,* wakati mzazi wake huyo ambaye angeweza kufundishwa huku naye akapata elimu angalau akajua jinsi ya kufuatilia mtoto, hapewi hiyo nafasi. Leo hii atamfuatiliaje huyo mtoto? Inakuwa ni vigumu sana. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha atuambie kuhusu suala la MEMKWA na MUKEJA linafanyiwaje kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Idara ya Ukaguzi. Idara hii kwa kweli imekuwa ni idara ambayo imetelekezwa, haiwezekani Idara itegemee kupata sh. 500 kwa kila ada inayotozwa kwa mtoto iweze kujiendesha. Leo hii Wakaguzi ni chombo muhimu sana katika shule zetu na bila ukaguzi hakuna chochote kitakachofanyika, lakini tumewaacha tu wanaeleaelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti waliyotengewa ni kidogo mno, naomba Idara hii sasa iwe huru na itengewe fedha za kutosha ili iweze kufanya kazi yake vizuri na iweze kuboresha kiwango cha elimu ambacho kinatolewa hapa nchini. Lakini kama hatutawatengea pesa za kutosha, Idara ya Ukaguzi hatutakuwa tumefanya lolote katika kuboresha elimu yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo suala la wenzetu walemavu. Kwenye Kamati yetu tulibahatika kufika Shule ya Bohangija na Shycom. Inasikitisha sana kuona mashine za kuandikia maandishi nundu ni mbovu, hazipo na mbaya zaidi hata

wataalam wenyewe hawapo, shule kubwa kama Shycom ambayo ni ya siku nyingi, tumekuta Mwalimu mmoja ambaye naye amestaafu anaomba Mkataba aendelee kuhudumia Taifa hili la wana wa Mungu, amenyimwa mkataba. Tunamuuliza mkuu wa shule maelezo anayotupa hayaeleweki, hayaridhishi.

Tunaomba tafadhali wahusika ndani ya Wizara kwa utaratibu mnaoujua tafadhali teremkeni huku chini muangalie matatizo yaliyopo. Naomba mtoke ofisini, vinginevyo kama mtasubiri kuletewa ripoti watawaletea ripoti nzuri sana, lakini yanayotendeka huku chini ni madudu tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mulugo, Naibu Waziri kwa kazi anayoifanya na nampongeza sana. Tafadhali tembeeni, nendeni muone yaliyoko huku, lakini kama mtajikita ofsini ndugu zangu kila siku mtapata ripoti nzuri, lakini matokeo yake hayatakuwa ya kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kabisa suala hili la hawa walemavu, hawa wenzetu ambao wanahitaji mashine, lifanyiwe kazi kwa haraka. Ikiwezekana walimu wanaofundisha watoto wetu walemavu tafadhali waangaliwe kwa jicho la pekee, waongezewe nafasi za kwenda kujiendeleza, waletewe vifaa na wapewe mazingira mazuri ya kufanya kazi. Leo hii nashukuru tulionao wanajitolea, lakini unaona jinsi walivyokuwa *committed* kufanya kazi yao vizuri. Tuwasiwavunje moyo, tuwape nafasi

wajiendeleze na wanaporudi kazini basi tuwape vitendea kazi vizuri waweze kufanya kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru pia kwa mchango wako sasa nimwite Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Abia Nyabakari ajiandae.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya katika mazingira magumu ya migomo pamoja na maandamano. Lakini hata hivyo, bado Mwenyezi Mungu anawawezesha kufanya kazi yao vizuri na *inshallah* watafikia mahali mambo yatakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba niipongeze Serikali kwa kuanzisha shule za Kata. Naomba niseme kwamba, mwanzo ni mgumu, lakini *inshallah* Mwenyezi Mungu atatufikisha pale ambapo kwa sasa tunakusudia kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala zima la bajeti. Bajeti ya Wizara yetu hii ya elimu bado haikidhi au kutatua kero na changamoto za Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo baadhi ya mambo ambayo wenzangu wamekwishayazungumza, lakini na

mimi nilifikiri ni vizuri nikayasemea. Kwanza kabisa naishauri Serikali kwamba, yako baadhi ya mambo ni vizuri tukawasikiliza Walimu na tukayatolea ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza kabisa ni la kuwapatia walimu posho ya kufundisha. Posho hii inaweza kuwa kama motisha ili waweze kufanya kazi yao vizuri. Ukiwapa hii posho nadhani hata upungufu mwingine uliopo ambao wanaulalamikia unaweza ukapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara hii ziko fedha ambazo zinapelekwa hizi za *OC*. Nashauri Idara hii ya Elimu ni vizuri ikaweka wazi juu ya suala zima la fedha za matibabu kwa Walimu pamoja na za nauli pale wanapokwenda likizo. *OC* haioneshi kabisa kwamba fedha za matibabu kwa Walimu ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa walimu wakishafahamu kuwa fedha zao za matibabu zipo basi wanaweza wakatibiwa na hatimaye wakachukua risiti zile wakapeleka ili waweze kurejeshewa fedha zao. Hayo ni mambo madogo madogo na marupurupu ambayo labda hao Walimu wakitekelezewa wanaweza wasifanye migomo hiyo ambayo wanaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri vile vile katika suala zima la ucheleweshaji wa kuwapandisha madaraja Walimu. Wako Walimu au Maafisa wa Elimu ambao hawapandishwi madaraja. Wanachelewa kupandishwa na wale ambao wanapandishwa madaraja, lakini hawapewi haki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali, Walimu wanapokuwa wamepandishwa madaraja, basi waende sambamba na malipo yao. Isifike mahali Walimu wanakaa muda mrefu ndipo sasa haki zao zinaanza kushughulikiwa. Hii yote inaleta matatizo ya kuandamana. Sasa niombe Serikali ihakikishe kila Mwalimu anayepandishwa daraja basi kupandishwa huko kuambatane na malipo yake aende nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Idara ya Ukaguzi. Tunazungumza kwamba wanafunzi wanafeli, ni kweli wanafunzi wanafeli, lakini wanafeli kwa sababu kwanza wakaguzi wenyewe wana kero ambazo hazitatuliki. Kwa mfano, kero ya kwanza fedha za kuendeshea ofisi hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile magari ya hawa Wakaguzi yanakosa mafuta. Mara nyingine wanatia hata huruma, magari yao yanaweza yakawa yamekosa hata matairi, wanafika mahali wanasubiri mpaka labda Mheshimiwa *DC* ametoa matairi yake ili aweke mapya, basi wanaomba matairi yake ya zamani ndiyo wanaweka kwenye magari yao. Hivi kweli hii kazi ya ukaguzi itafanywa kwa njia hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe hawa Wakaguzi wafikiriwe na wapewe zana za kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na fedha. Lakini wakiendelea kuchukua matairi ambayo *DCs* wameondoa kwenye magari yao ndipo wao wachukue, hii kwanza inaweza ikasababisha hatari za ajali. Ni vizuri hawa nao

wakafikiriwa ili kusudi waweze kufanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linachangia katika kushuka kwa elimu ni pamoja na mabadiliko ya mitaala. Tunapobadilisha mitaala mara kwa mara kunakuwa na upungufu wa vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyote vile unapobadilisha mitaala vinakuja vitabu vingine. Sasa mpaka kuja kupata vitabu ambavyo vinafanana na mitaala ile, tayari tunakuwa tumeshaharibu utaratibu mzima wa elimu kwa watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba, Wizara hii ni vizuri ikawa inapewa kipaumbele ili kusudi iweze kufanya kazi yake vizuri, labda malalamiko haya ambayo yako kwa Walimu yanaweza yakapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Mary Chatanda. Namwita Mheshimiwa Abia Nyabakari, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi. Mheshimiwa Ntukamazina ajiandae na pia Mheshimiwa Ezekiel Wenje na Rosweeter Kasikila wajiandae.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja nitaanza kulisema kwamba, viongozi wenye uchu wa madaraka

wanaotaka kuingia Ikulu kwa nguvu huwa ni matatizo dunia nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukawa na kiburi fulani, ukatoa maneno laini na watu wakahadaika, lakini siyo kila lugha inayozungumzwa inaweza kutawala nchi ndugu zanguni. Kuna viongozi waliopita kama Napoleon, Churchill na Kenedy ambao walikuwa viongozi hodari walioitetemesha dunia, lakini hata wao wenyewe walishindwa kuitawala dunia na hatimaye kutaka kupoteza maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya nchi hii inasema watoto wasifanye kazi na huku vitabu vingine vinasema mlee mtoto katika njia impasayo naye hataiacha hata atakapokuwa mzee. Mtoto huyu tunamlelea wapi? Miaka mitatu unamtupia Mwalimu anakwenda kutawaza mavi huko, kila kitu Mwalimu! Hatuna muda wa kulea watoto wetu. Watoto wetu wanakaa muda mrefu na Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, sheria nyingine iko inanyemelea inasema mtoto asipate mapigo. Biblia inasema katika Methali 23:13 kwamba: "Usimnyime mtoto wako mapigo maana hujapompiga kwa fimbo hatakufa." Lakini leo sheria moja baada ya nyingine zinatolewa, tutakuja kuishi kwenye ulimwengu usiokuwa na sheria na utatupa shida. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wanaomaliza darasa la saba bila kujua kusoma na kuandika tumlaumu nani? Uzembe huu ni wa nani? Lazima tujue hapa kuna matatizo, lakini matatizo yako wapi?

Inawezakana matatizo yako kwa Walimu Wakuu hawasimamii kazi zao vizuri. Yawezekana katika Wizara zetu napo kuna matatizo, hawasimamii vizuri Wakurugenzi na Walimu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, kama mwenzangu alivyotangulia kusema Idara hii ya Ukaguzi inakagua shule ngapi kwa mwaka? Mnaziwezeshaje shule hizi? Wamepewa kifungu gani cha kusimamia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu zimekuwa na matatizo. Watoto wanaokwenda mpaka vyuo vikuu nao imekuwa ni matatizo. Matokeo yake wanapomaliza shule siyo wote wanaopata ajira; wengine watakwenda ofisini na wengine kwenye makampuni. Lakini wengi wanaishia kwenye vijiwe usiku na mchana, kutwa CHADEMA, CCM, CUF, akiingia Mbowe tutapata nafuu, hakuna unafuu ndugu zangu, kama hamuwezi kufanya kazi. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sema wewee!

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Wakati fulani unaweza ukapita pale kama ni Mbunge usiyependwa utasikia wanasema “Yah yaa, yaa Mbunge! Yah yaa, Mbunge Nyabakari, *anyo melile*. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake Mbunge ni yule wanayemtaka. Ndugu zanguni vijana wetu wana njonzi za kuwa na maisha ya kifahari bila kufanya kazi, wana njonzi za kuwa na majumba ya kihafari bila

kufanya kazi, wana njonzi za kuwa na magari ya kisasa bila ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usiku kucha watoto wetu wamekuwa ni msalaba sasa kwa sababu hatukuwalea katika njia iwapasayo. Maana tangu wakiwa wadogo wamelelewa hivyo hivyo mpaka chuo kikuu, *chips* mayai na hata wanaporudi wamekuwa ni misalaba hawataki kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke utaratibu. Sasa ni muda muafaka wa kutoa elimu baada ya kumaliza darasa la saba, *form four, form six* na vyuo vya elimu ya juu, wajifunze kazi za mikono hata zile ndogo ndogo angalau kwa muda Fulani. La sivyo wazazi tutateseka maana watoto wetu wamekuwa vitanzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni rahisi kwa kusema, lakini watoto hawa watatutoa macho. Hata kwa wale wanaosema Serikali haifanyi kazi wao wenyewe watakuwa wa kwanza kutolewa macho. Ni lazima kila mtu afanye kazi! Biblia inasema asiyefanya kazi asile. Watoto wetu wanaishi bila kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaombeni sana Serikali sasa iweke mikakati ni vipi itawawezesha watu hawa kujua kufanya matumizi mazuri ya fedha na kuepuka maisha ya anasa, maana mawazo yao na fikra zao ziko kwenye njozi ya kuwa matajiri bila ya kufanya kazi. Mnawatoaje huko? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofi /Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa mchango wako Mheshimiwa Abia, wewe ndiye Abia *original*, ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo bajeti ya Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuipongeza Wizara. Wizara inafanya kazi nzuri, maana mtu anayefanya kazi vizuri ni vizuri mkampongeza, kama kuna upungufu muuzungumze, lakini ni vizuri tukawapongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Naibu Waziri wa Elimu ndugu yangu Philipo Mulugo kwa kazi nzuri ambayo amefanya katika kusaidia Wizara hii. Lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri maana ndiye aliyempa fursa Mheshimiwa Mulugo kufanya kazi. Kama Waziri angekuwa mgumu bila shaka hata Naibu Waziri asingeweza kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri umefanya vizuri kugawanya madaraka kwa msaidizi wako na bila shaka hata viongozi wengine wa Wizara

yako. Tunaomba ushirikiano huo uendelee ili sekta ya elimu iweze kwenda vizuri katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nichangie mambo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni jambo ambalo limekuwa linaendelea nchini hasa la kuwafutia wanafunzi matokeo ya mitihani baada ya kubainika kwamba *either* walipewa majibu na Walimu wao au wao wenyewe inawezekana wamepata majibu kwa njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachozungumza na kusikitika hapa ni kwa wale Walimu au wasimamizi ambao wanawapa wanafunzi majibu ya mitihani yao, lakini mwisho wanafunzi na wenyewe wanakuja kupewa adhabu. Hilo mimi nadhani lisikubalike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kipindi kilichopita baadhi ya wanafunzi ambao walikuwa wamefanyiwa mitihani wakafutiwa matokeo ya mitihani na baadaye wakaambiwa miaka mitatu wasingeweza kufanya mitihani yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wananchi wengi pamoja na Bunge lako Tukufu kusema kwamba, si haki kuwafutia wanafunzi hao na kuwapa adhabu, Serikali hatimaye ilisikia na kuwaambia hawa vijana sasa nadhani watafanya mitihani yao mwaka unaokuja. Nataka niipongeze sana Serikali kwa kusikia kilio cha wananchi lakini pia na wanafunzi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hatua za dhati kabisa tena kali zichukuliwe kwa miaka inayokuja kwa wasimamizi wote wa mitihani na Walimu ambao watabainika wanawapa watoto hawa mitihani ambayo haitawasaidia sana katika maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumze kwa ujumla kuhusiana na haki za watumishi. Najua suala hili lina mgogoro, sitaki kulizungumza sana, lakini niseme hivi, suala la migogoro ya maslahi kwa watumishi wetu limekuwa endelevu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili kama wenzangu walivyotangulia kusema, limewafanya wakati mwingine hata vijana wetu ambao hawana hatia na hawajui hata yanayoendelea kuathirika kwa sababu wameshindwa kupata elimu katika muda muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali iliangalie jambo hili sawasawa. Ni lazima zipo sababu za msingi kwa watumishi wakiwepo Walimu kuendelea kugoma kwa sababu ya maslahi duni. Ni ukweli usiopingika kwamba maslahi ya watumishi wengi wa Serikali katika nchi hii wakiwemo Walimu ni duni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali isipuuze jambo hili. Lazima tuendelee kuzungumza tufikie muafaka, lakini tufanye hivi bila kuumiza upande wowote; Walimu wasiumie na Serikali isiumie. Tufanye hivi kuhakikisha kwamba Walimu na watumishi wengine wanaweza kutendewa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunazungumza hapa Bungeni kwamba Walimu wengi wanaishi katika mazingira magumu. Walimu wengi wanafanya kazi kubwa, lakini pia sisi wote tuliopo humu ndani wale ambao wanajiona ni kada muhimu labda Madaktari, Wahandisi, wote wametokana na huyu mtu anayeitwa Mwalimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri, pamoja na hotuba nzuri ya Waziri ambayo ameiandika, lakini bado kuna haja ya Serikali kuendelea kukaa na watumishi hawa, kukaa na viongozi wa Vyama vya Walimu na wafanyakazi ili kuweza kuzungumza na kubaini tatizo ni lipi halafu tuweze kulirekebisha, vinginevyo kuendelea kuvutana, kupelekana Mahakamani, kwenda wapi, hatuta-*solve* mjadala huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema hakuna mgomo mbaya kama ule ambao Walimu wataamua kwenda madarasani lakini hawafundishi. Utakuwa ni mgomo mbaya sana ambao hautatusaidia sisi kama Serikali. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie jambo hili kwa umakini, iendelee kukaa meza moja na Walimu na watumishi wengine ili kuangalia maslahi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nishauri kwamba, hivi Serikali haiwezi kuanzisha chombo maalum ambacho kinajitegemea ambacho kinaundwa na wataalam, maana tuna wataalam wengi katika nchi hii ambao wamebobea kwenye masuala ya maslahi, lakini...

*(Hapa Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni alikatiza katikati ya Mwenyekiti na mchangiaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masauni rudi kule ulikotoka! (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uangalie dakika zangu hapo kama mbili au tatu hivi zimeharibika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri ni vizuri Serikali ifikirie kuunda chombo maalum ambacho kitapitia malalamiko ya Walimu. Badala ya Serikali na chombo hiki ambacho wamekaa kwa muda mrefu wakishindana nadhani wanafunzi watakuwa wanaumia zaidi kuliko Walimu wenyewe. Kwa hiyo, tuunde chombo ambacho kitapitia maslahi ya watumishi hawa na baadaye kije na mapendekezo Serikalini. Najua zipo jitihada za Serikali, lakini nadhani hazitoshi twende tukafanye vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza jambo hilo, naomba kidogo nizungumzie Sekondari za Kata. Wenzangu wamezungumza, naomba nianze kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga Sekondari nyingi za Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana maana wapo vijana ambao wamekwenda Vyuo Vikuu ambao ni matunda ya Sekondari za Kata. Hatuna sababu ya

kuendelea kuzibeza, lakini tuipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kujenga sekondari hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kujenga sekondari hizo bado upo upungufu mkubwa. Tunahitaji kurekebisha hali iliyopo na nafikiri labda umefika wakati kwa vile tumejenga sana sekondari hizi, sasa tuache kujenga Sekondari mpya tuboreshe zilizopo, maana zilizojengwa nyingi bado hazipo kwenye hali nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna haja ya kuziboresha hizo zilizopo ili ziwe katika mazingira mazuri zaidi kwa maana ya kwamba tuweke vitabu, tujenge mabweni zaidi ya watoto hasa hosteli kwa wanafunzi wa kike. Kwa kweli wanaishi katika mazingira hatarishi zaidi au kwa kutembea mwendo mrefu kutoka shuleni kwenda nyumbani na kutoka nyumbani kwenda shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani wakati mwingine kukumbana na vishawishi mbalimbali njiani na wengine wameishia kupata mimba au ujauzito na kwa maana hiyo kushindwa kumaliza masomo yao kwa kukosa mahali pa kulala pale shuleni, kwa hiyo nashauri Serikali iangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine wananchi hawa tumeshawachangisha sana jamani, wananchi wamechoka sana. Naomba Serikali ifikirie tusimame kuwachangisha wananchi, tuwaache wafanye shughuli nyingine, lakini Serikali isimamie kuhakikisha kwamba tunaboresha sekondari zilizopo maana tunakwenda kwa wananchi, tunawachangisha mpaka

wanafika mahali sasa unakuwa ni ugomvi kati ya Serikali na wale wananchi ambao wanachangishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanakimbia majumbani kwenda kujificha kwa sababu ya michango hii. Niishauri Serikali tupunguze ugomvi na malalamiko mengi yanayotoka kwa wananchi kwa sababu ya michango ambayo Serikali inaweza ikaamua kuifanyia kazi yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie malipo kwa watumishi wanaoanza kazi. Mwaka jana karibu miaka miwili mfululizo Walimu ambao wametoka kwenye vyuo na kwenda kuajiriwa wamepata tabu sana ya kulipwa fedha zao. Hii imesababisha malalamiko mengi sana kwa Walimu ukizingatia kwamba hawa vijana wanatoka vyuoni wanakwenda kuripoti hawana fedha mfukoni, hawana nini, wamekaa katika mazingira mabaya sana na magumu sana na wengine kuwaingiza kwenye vishawishi ambavyo wameshawishika na baadhi ya watu wasio wazuri na wengine wanajikuta kwamba wameingia katika mtego ambao haukuwa na sababu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ndio nasema tuangalie namna ya kuandaa mafao ya vijana ambao wanatoka vyuoni. Wanapoingia tuhakikishe kwamba fedha zao wa kuwalipa zipo na kusiwe na usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze suala la mikopo. Bodi ya Mikopo imekuwa

inalalamikiwa sana na vijana wetu wa Vyuo Vikuu wengi wanaokwenda huko. Hebu Serikali iliangalie jambo hili gumu, najua kwamba lilishakwenda kwenye Kamati inayohusika na Kamati inayohusika ilishalifanyia kazi, lakini bado malalamiko hayajakwisha. Kuna nini kwenye Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanaotoka hata Jimboni kwangu wamelalamika sana hawapati mikopo muda unaostahili, hivi kwa nini tunapitisha bajeti hapa. Fedha zipo, lakini vijana wanapotakiwa kupata zile fedha wanacheleweshwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine hata Serikali imechangia migomo ya wanafunzi kwa sababu ya kuchelewesha kuwapatia mikopo yao kwa wakati unaostahili. Kwa hiyo, ninaisihi sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi ihakikishe kwamba, vijana ambao wanakwenda vyuoni wanaopata mikopo ya Serikali, basi wanapatiwa mikopo hiyo mara moja bila ya kuchelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kwa sababu najua dakika zinakwenda, nizungumzie suala la Elimu ya Watu Wazima. Elimu ya Watu Wazima nimesoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri anaonekana kwamba kazi nzuri imefanyika na mipango ipo, lakini tukienda kwenye ukweli wenyewe vijijini Elimu ya Watu Wazima imekufa haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tunaandika kwenye vitabu, lakini vijijini Mwenyekiti nakuhakikishia kweli

Elimu ya Watu Wazima imekufa, haipo. Naomba Idara inayohusika na Elimu ya Watu Wazima kuanzia Wizarani mpaka kwenye Wilaya zifanye kazi sawasawa vinginevyo Elimu ya Watu Wazima ambao tulikuwa tunaipata huko nyuma imekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na niseme naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Ntukamazina, Mheshimiwa Wenje ajiandae na Mheshimiwa Rosweeter Kasikila ajiandae.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitazungumza kama Mwalimu *by profession.* Nianze kwa kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote walioko chini ya Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya bajeti ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu, naomba nirudie msimamo wangu ambao nimekuwa nikiutoa mara kwa mara ambao baadhi ya viongozi Serikalini hawaupendi msimamo wangu. Bado nasema kwamba...

**MWENYEKITI:** Nawaomba msikilize ndani, *order in the House!*

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Bado nasema kwamba tulifanya makosa kuhamisha Idara ya Elimu ya Msingi na Idara ya Elimu ya Sekondari

kuzipeleka TAMISEMI. Mimi nilishiriki katika kuunda TAMISEMI nilipokuwa nasimamia *Reform* za Serikali na tulisema tunaunda TAMISEMI kufanya kazi mbili. Moja, kuwa kiungo kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu na pili kusimamia uendeshaji wa kila siku wa shule za msingi. *The day to day running of Primary Schools not the management of education as a discipline.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the management of education as a discipline* ni kazi ya Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu ndiyo ina *instutional memory.* Hii inanikumbusha maneno ya mwisho ya Gavana wa mwisho mwaka 1962, Desemba alikuwa anaitwa Sir Richard Turnbull wakati Mwalimu Nyerere anamsindikiza kwenye meli, alimwambia maneno machache lakini mazito. Alimwambia Rais Nyerere maana ndio alikuwa amekuwa Rais akasema "*You can politicise everything, but not education*", "Unaweza ukafanya kila kitu kikawa siasa, lakini sio elimu".

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huo ndio msimamo wangu, mimi wananifananisha kama Yohana Mbatizaji aliyekuwa anahubiri nyikani kuhusu ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo kwa wale ambao ni Wakristo, lakini hakuna mtu aliyemsikiliza, sasa ngoja niendelee kuitwa Yohana Mbatizaji. Lakini Mheshimiwa Waziri nenda Uganda zungumza na mwenzako wa Uganda, walijaribu ku-*decentralize primary education* na *secondary education* kuzipeleka Serikali za Mitaa wakapata matatizo makubwa sana, ikabidi Idara hizo wazirudishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya msimamo wangu huo, naomba nianze kuchangia*, I know it is a voice in the wideness* na mimi nazungumza sauti inayolia nyikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye bajeti. Bajeti hii ni ndogo sana ukizingatia kwamba elimu ni kipaumbele cha kwanza. Nilipokuwa nachangia Wizara ya Afya nilisema elimu na afya ndiyo kipaumbele cha kwanza katika kuelekea nchi ya ahadi. Nchi yenye uchumi wa Kati, kilimo kinakuja cha pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bajeti hii ni ndogo sana, lakini hii bajeti tutakayoipitisha asilimia 85, itakwenda kwenye Bodi ya Mikopo kulipia ada za vijana wetu katika Vyuo Vikuu na asilimia 15 zitakazobaki ndio zitagawanya kati ya Idara ambazo ziko pale Wizara ya Elimu pamoja na Baraza la Mitihani, Taasisi ya Kukuza Mitaala na Vyuo Vikuu vya Umma watakuwa wanagawana asilimia 15 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kuwekeza kwenye elimu, *investment in the human capital* haina maana tu ya kulipa karo za wanafunzi, kuna mambo mengine ambayo lazima tuyaangalie. Kwa mfano, lazima tuangalie masuala ya vitendea kazi katika Vyuo Vikuu, vitabu, vifaa vya maabara, kuboresha maslahi ya Walimu na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivyo vyote vitategemea asilimia 15, sasa *are we serious* katika

kuwekeza kwenye elimu. Kwa mfano, Vyuo vya Elimu ya Juu vinapata matatizo sana vinapewa *personnel emoluments,* yaani fedha za mishahara, lakini wanapewa fedha kidogo sana za matumizi ya kawaida pamoja na *development* na hivi ni vyuo vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi ni Mwenyekiti wa Chuo Kikuu cha Muhimbili, Chuo Kikuu cha Madaktari tangu mwaka 2007 mpaka sasa. Nikichukua chuo hicho kama mfano vyuo vyote vina matatizo, lakini kwa miaka zaidi ya mitano hatujapata *other charges* zaidi ya asilimia 14 ya fedha ambazo tumeziomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye *development* mwaka 2007/2008 tulipata asilimia tano tu, mwaka 2008/2009 tukapata asilimia 13, mwaka 2009/2010 tukapata asilimia tatu, mwaka 2010/2011 tukapata *zero*, mwaka 2011/2012 tukapata asilimia 12. Sasa huo ni mfano tu wa *MUHAS*, lakini vyuo vyote vina matatizo kutokana na kugawana ile asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Idara ya Ukaguzi, wenzangu wote wameizungumzia Idara hii. Nilikuwa na swali juzi juzi nikasema huko Ngara shule ziko 114 za Msingi, 24 za Sekondari hazikaguliwi kwa sababu Idara ya Ukaguzi haina fedha. Lakini tujue kwamba kazi ya ukaguzi ni kuhakiki ubora wa elimu inayotolewa kwenye shule zote za msingi. Kama ukaguzi haupo Walimu hawatatayarisha *lesson notes* na Walimu hawatamaliza *syllabus* kwa hiyo elimu inashuka. Idara ya Ukaguzi ni kitu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Elimu ya Watu Wazima, nimefanya utafiti nilishiriki katika kueneza Kisomo cha Watu wazima Tanzania miaka ya 1970, tukafikia asilimia 95 ya *literacy* kujua kuandika, kusoma na kuhesabu. Sasa hivi nimesikia juzi tumefika asilimia 40 na wala sio 69 iliyotolewa na Upinzani, ni asilimia 40. Maana yake Watanzania asilimia 40 ndio wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu. Sasa *are we serious* kufikia ile nchi ya ahadi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msingi huo kuna soko la ajira la *East Africa* na *Central Africa* vijana wetu wataweza ku-*compete* katika soko la ajira katika hali ya elimu ya namna hiyo. Niende kwenye Ualimu (*Teaching),* mimi ni Mwalimu *by profession.* Vijana wetu wanaokwenda kwenye Vyuo vya Ualimu ni wale waliomaliza Kidato cha Nne *Division IV* pointi 27. Wanapokwenda kwenye vyuo wanakutana na Walimu pia na Wakurufunzi ambao sio mahiri, kinachotokea ni *bare foot teachers*, sio Walimu waliokamilika kutokana na zile *points* wanazozipata na Walimu ambao wako kwenye vyuo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu walioko kwenye vyuo vyetu sio kama sisi tuliokuwa *trained* zamani na sisi tulikuwa tunajifunza nadharia mbalimbali. Kwa mfano, Walimu walioko kwenye vyuo sidhani kwamba wanaijua nadharia ya Profesa Benjamin Bloom’s *taxonomy of education*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nadharia inawafundisha Walimu kwamba muwaandae watoto kuhakikisha kwamba wanapitia hatua sita za

kuhakikisha kwamba watoto wanaelimika vizuri. Hatua hizo ni kutoa *knowledge, comprehension, application, analysis, synthesis* na *evaluation.* Walimu wa siku hizi mambo hayo hawawezi kuingia ndani wakayajua hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za binafsi nasema kwamba ni biashara. Tena mara nyingine ni biashara haramu. Kwa nini nasema hivyo, shule hizi nyingi zinasajiliwa bila kufikia viwango, shule hizi zinapandisha *school fees* na sijui kwa nini Wizara ya Elimu haiwezi kudhibiti *school fees* za shule hizi kwa kutumia *unit cost*. Wanasajili watoto ambao hawakushinda vizuri ili mradi wapate *school fees,* shule hizo hazikaguliwi, lakini shule hizo naambiwa zimewaajiri Waganda na Wakenya ambao sio Walimu *by profession,* lakini sifa yao ni kujua kuzungumza Kiingereza tu, sasa sijui katika hali hiyo tutafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ufundi nakubaliana na wenzangu kwamba tunahitaji Vyuo vya Ufundi na Ilani ya Uchaguzi inazungumzia Chuo cha Ufundi kila Wilaya na Ngara sina Chuo cha Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Kasikila ajiandae na Mheshimiwa Obama ajiandae.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa. Huwa naamini kwamba duniani hapa mtu akipata fursa ya kufanya

kazi yoyote kwa nafasi yoyote lazima mtu ujitahidi kuweka *mark legacy* kwamba utakapotoka ni nini kitafanya, watu wakukumbuke kwamba fulani alikuwepo kwenye hii ofisi na alifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu miaka mitano itakapokwisha Mheshimiwa Waziri amekaa kwenye Wizara hii kama Waziri sijui ni *legacy* ipi atakayoacha, itakayofanya akumbukwe kwamba alikuwepo Mheshimiwa Kawambwa kama Waziri wa Elimu na alifanya *transformation* moja, mbili na tatu. Nasema hivi kwa sababu tumewahi kuona Mawaziri wengi wa Elimu nchi hii, sasa sijui kama Mheshimiwa Waziri anataka kwenda kwenye rekodi tu kwamba na yeye aliwahi kuwa Waziri wa Elimu na sababu ni hii hapa inayonifanya kuhoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu ya Tanzania uko vile vile *almost* toka enzi za Wakoloni ni mfumo wa elimu ambao dunia ya leo inatoka kwenye *analogue* tunaenda kwenye *digital,* lakini mfumo wa elimu wa Tanzania bado uko kwenye *analogue.* Humu ndani wamejaa wazee, ukienda kwenye *syllabus* ya hesabu waliyofundishwa babu zetu shuleni ndio bado ipo, watoto wetu wanafundishwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *syllabus* ya sayansi kwa mfano, waliyosoma hao akina mzee Wassira, ndiyo mpaka leo bado ipo *syllabus* hiyo hiyo. Sasa kama tuna mfumo wa elimu ambao ametoka babu mpaka vijukuu, tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimnukuu jamaa mmoja anaitwa Bill alikuwa anajaribu kutoa maana ya elimu ni nini, akasema naomba nimnukuu kwamba:

"*The aim of education should be to teach us rather how to think than what to think*" Akaendelea kusema: *"The aim of education should be to improve our minds so has to enable us to think for ourselves than to load the memory with the thoughts of other men.* "Elimu ya Tanzania ina *load memory* ya wanafunzi wetu *with thoughts of other men*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tukiendelea na mfumo wa elimu ambao haitusaidii kufikiria kwa ajili yetu sisi wenyewe hatuwezi tukaenda. Elimu *should be dynamic.* Kama itaendelea kubaki hivi hata Mheshimiwa Waziri atatoka kwenye hii Wizara itabaki yale yale, mfumo ni ule ule ambao hautatusaidia ni mfumo wa *white collar job* iliyoanza kipindi cha Wakoloni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana leo mtu anamaliza Chuo Kikuu asipopata ajira *then that is the end of him.* Yaani elimu ya leo ambapo kuna changamoto ya ajira haimwezeshi huyu mtu *life after school,* atakwenda kufanya nini. Natoa rai kwa Serikali, sasa ni muda muafaka wa kutoka kwenye mfumo wa *analogue* ya elimu twende kwenye mfumo wa *digital* ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la Elimu ya Juu *(TCU)* pamoja na Bodi ya Mikopo.

Leo mfumo wa kuomba nafasi ya kujiunga na Chuo Kikuu Tanzania wanafunzi wote wanatakiwa waombe kupitia *TCU*. Sasa wanapoomba *TCU* ndio inaamua iwapangie Chuo kipi wanafunzi wakishaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna wengine wanapelekwa kwenye vyuo ambavyo ni vya binafsi ambavyo ukilinganisha ada kwenye hivyo vyuo ukalinganisha na vyuo vya Serikali kule ada iko juu sana, lakini mkopo wanaopewa ni ule ule *unless* kama Serikali inaweza ika-*regulate* ada kwenye vyuo vyote nchi hii bila kujali vyuo vya binafsi na vyuo vya Serikali ada iwe katika *level* moja ili hata mwanafunzi akipelekwa *Tumaini University* au *Saint Augustine* na anayekwenda *University of Dar es Salaam* ada yao ya chuo ibaki katika *level* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahoji kwa nini mtu kwa mfano anayesoma Sheria anasoma *University of* Dar es Salaam, mwingine anasoma Mzumbe ambavyo ni vyuo vyote vya Serikali kwa nini ada iwe tofauti. Vyuo vyote vya Serikali mtu anasoma Mzumbe anasoma kozi ile ile mwingine anasoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anasoma kozi ile ile ya Sheria halafu ada ni tofauti kwenye vyuo vya Serikali kwa nini tofauti iwepo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa wanafunzi wa *Saint Augustine University,* Mwanza wengi sana walinipigia simu wakilalamika kwamba walipangiwa *field* wakaenda kwenye *field* wamekaa *almost* mwezi mzima hawakupata hata fedha ile ya kujikimu wakiwa kwenye mafunzo huko ya *practical*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kufuatilia nikaongea mpaka na viongozi wa Bodi ya Mkopo wakaniambia tatizo walilokuwa nalo ni kwamba Hazina inachelewa kuwapa fedha ili wao waweze ku-*disburse* hizo fedha kwenda kwa wanafunzi wanaohusika. Sasa nikagundua wakati mwingine tunalaumu sana Bodi ya Mkopo ya Elimu ya Juu kwamba ina matatizo, haipeleki fedha kwa wanafunzi katika muda unaotakiwa na ndiyo maana wakati mwingine wanafunzi wanaandamana, kumbe tatizo sio Bodi ya Mikopo, tatizo ni Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha uko hapa kusaidia wanafunzi wa Tanzania ambao ni watoto wa Mama Ntilie ambao ni watoto wa waendesha pikipiki, ambao ni watoto wa wakulima jitahidini basi kupeleka fedha mapema huko kwenye Bodi ya Mkopo ili wanafunzi wanapokuwa huko kwenye *field* wasipate shida. Leo hii tunazungumza hapa wanafunzi wa *CBE* hawajapata fedha zao za *field* mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Sera ya Elimu ya mwaka 1995, Sera ya Elimu inasema kwamba *medium of instruction* kwenye shule za msingi Tanzania itakuwa ni Kiswahili. Lakini leo humu karibu sisi wote hapa hakuna hata Mbunge mmoja au Kiongozi humu ndani ambaye mwanawe anasoma kwenye hizi shule za Serikali wanazofundisha Kiswahili, wote hapa wamepeleka watoto kwenye *English Medium School.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sikiliza, tukisema leo kwamba, tufute basi Kiswahili ili shule zote hata hizi za Serikali basi wanafunzi wa watu maskini wanaosoma pale wapate pia hicho Kiingereza tokea shule za msingi, mnapiga kelele hapa kwa unafiki mnasema eti Kiswahili ni lugha, tunaipenda sana lugha yetu, lugha yenu mbona nyie watoto wenu hawasomi hicho Kiswahili kuanzia shule ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni unafiki hatuelewi *media of instruction* katika *primary school* ni Kiingereza au ni Kiswahili. Mimi nina wa-*challenge* acheni unafiki, tukubaliane kama ni Kiswahili iwe ni Kiswahili kwenye *primary school*, kama ni Kiingereza na hizo shule za Serikali zifundishwe Kiingereza ili wanafunzi wapate *knowledge* ya Kiingereza ili watoto wa watu masikini wapate kama watoto wenu wanavyopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la motisha kwa Walimu, Walimu wanagoma, halafu Serikali inakimbilia Mahakamani. Kama Serikali haina pesa siyo lazima utoe pesa kwa mtu ndiyo iwe motisha, naomba nitoe pendekezo kwa Serikali, mnachoweza kufanya ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha namba moja kwa Mwalimu kuna maduka ya wanajeshi ambayo mwanajeshi anakwenda kununua na kupata punguzo anapotaka kujenga nyumba. Kwa nini Walimu pia wasitengenezewe maduka yao ambapo hata vifaa vya ujenzi vitakuwa havitozwi kodi ili hata kununua bati iwe rahisi hata upatikanaji wa simenti uwe rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mshahara wake mdogo Mwalimu hawezi kujenga nyumba, siyo lazima aongezewe mshahara tu tunaweza kuangalia mbinu nyingine za kutoa motisha kwa Walimu, kwa mfano, mtoto wa Mwalimu kama akisoma mpaka Chuo Kikuu kwa nini asipewe mkopo asilimia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Kasikila na Mheshimiwa Obama atakuwa wa mwisho.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Nitachangia machache kwa sababu hata muda wenyewe ni mdogo sana. Wako Waheshimiwa ambao wamezungumzia kuhusu walemavu, mimi nitazungumzia walemavu ambao ni viziwi na mabubu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabubu na viziwi watanisamehe kama hawawi-*adressed* namna hii, lakini mabubu na viziwi ni kundi dogo sana hapa nchini, lakini nao ni wananchi, ni Watanzania walio na haki kama watu wengine, tumekuwa tukizungumzia sana walemavu wa miguu wanaotembea kwa *wheel chair* hawawezi kupanda ngazi, hawezi kupanda maghorofa, lakini kwa nini hatuwazungumzii hawa mabubu na viziwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokuwa hospitali na-*witness,* ninapokuwa hospitali mabubu na viziwi wanapata shida sana kwa sababu mtu wa kwanza

wanaomkuta hospitali mawasiliano ni magumu sana. Huyu bubu anapofika hapa inakuwa ni shida haijulikani anataka kumuona Daktari au kaja kumuona mtu mwingine lakini inapogundulika kuwa amekuja kutafuta huduma akipelekwa kwa Daktari, Daktari hupata shida ya mawasiliano.

**MWENYEKITI:** Tunaomba utulivu, msikilizeni anayechangia.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Daktari hupata shida sana namna ya kuwasiliana na huyu kiziwi au bubu maana wengi anapokuwa ni bubu anakuwa ni kiziwi pia. Ni vipi Daktari anaweza kumhudumia, inakuwa ni shida labda kwa kumshikashika, akiona kuwa ana homa ndiyo aanze kuandika *investigations* alizoziona yeye mwenyewe Daktari akimpeleka maabara, mtu wa maabara naye anapata shida, hawezi kuwasiliana naye, akipelekwa kwa Daktari labda ameandikiwa dawa. Pale wanapotoa dawa inakuwa shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tusisahau kuwa mlemavu huyu tatizo lililompeleka hospitali ni siri yake yeye na Daktari na walio wengi hawaendi na ndugu zao anakuja mwenyewe lakini hata kama anakuja na ndugu yake mara nyingine ugonjwa alionao hatakiwi kumwambia ndugu yake anatakiwa kuongea na Daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Daktari hawezi kuwasiliana na huyu mtu wa *dispencing,* hata akipelekwa kupigwa mionzi *x-ray,* hawawezi

kuwasiliana. Naiomba Serikali kwa kuwa suala hili ni mtambuka Wizara ya Elimu wangeliangalia hili mitaala kwa watalaam wa vyuo mbalimbali waweze kuingiza hii lugha ya alama hata kama ni kwa dozi ndogo ili huyu mlemavu ambao ni bubu na kiziwi popote anapokwenda afurahie na aweze kuwasiliana na yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili halipo hospitali tu nataka kuuliza hapa Bungeni hizi *session* zote zinazoendelea hapa hao ndugu zetu walemavu wananufaikaje, kuna anayewalezea kwa kutumia lugha ya alama kuwa huko Bungeni kinachozungumzwa ni hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatafsiriwaje kuwa Mbunge wako leo ametetea kuwa uhaba wa maji upo wanajuaje? Wanajuaje kuwa Mbunge wao amezungumzia kuhusu masuala ya Walimu? Nadhani pia kuwa Bunge lingeona umuhimu wa kutafuta watumishi wa Bunge kwenda kwenye mafunzo haya ili mambo yanayoendelea hapa wale mabubu na viziwi wajue kinachoendelea katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwaweke pembeni, tunaweza kuwa tunatetea makundi makubwa kwa kujua kuwa kuna kura nyingi lakini hawa nao ni wananchi wanahitaji ku-*enjoy life* katika nchi yao, wanatakiwa kujua kinachoendelea Mabwana Shamba huko kwenye mashamba darasa wanawasilianaje na hawa mabubu na viziwi, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maaskari, Wanasheria, Wanasheria wanaofundisha haki za binadamu huko vijijini na kwingineko hawa

mabubu na viziwi wanaelewa nini au tumewaweka pembeni, tunawasaidiaje hawa ndugu zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mtaala, naona kuwa vyuo vingi au karibia vyuo vyote hii alama ya lugha ingetiliwa maanani ili na hawa Mabubu na viziwi tuweze kwenda nao pamoja wajue kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni mtambuka niishukuru Serikali kuwa imeanzisha ule mpango wa MMAM kwamba zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila Kata, lakini pamoja na hayo kumekuwa na *crash programme,* Wauguzi wana muda wa miaka miwili, hao ambao wanatakiwa kwenda kufanya kazi zahanati, ni miaka miwili, mwaka mmoja ni Uuguzi na mwaka mwingine inatakiwa iwe ni Ukunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuwezi kusema kuwa wanapokuwa wanajifunza Ukunga hawatoki *competent* kwa sababu miaka ya nyuma Ukunga ulikuwa unafundishwa kwa mwaka mmoja mzima. Lakini hivi sasa katika huu mwaka mmoja kama *crash programme* una mambo mengi ndani ambapo kuna *mental health* ambayo ina vitu vingi, *communicable disease* ina mambo mengi, kuna mambo ya *management and leadership*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi, kwa hiyo, siyo rahisi hayo mambo yote yakaunganishwa na shughuli za ukunga, halafu tukasema huyu amehitimu kwenda zahanati kumsaidia mama mjamzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ili suala la mwaka mmoja lifikiriwe, Wakunga wajifunze kwa miaka miwili au mitatu ili wakitoka hapa wawe wameiva maana haiwezekani mjamzito kule Songwe kwa Mheshimiwa Mulugo, kule Kerege, Mjamzito wa kule tumpelekee Mkunga aliyefuzu kwa miezi sita tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjamzito wa Dar es Salaam karibu karibu na Muhimbili ahudumiwe na wale wenye *degree* waliosomea miaka mitatu ambao ni *competent,* mjamzito wa kijijini ni sawa na mjamzito wa mjini na ni sawasawa na mjamzito wa Marekani, wote wajawazito hawa wanahitaji huduma inayofanana. Naomba kuwa hili suala Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya wakae pamoja waangalie jinsi ya kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania *Midwife Assosiation na Tanzania Nurses Midwifes Council* wamekaa pamoja na wakawa wameshirikiana na *International Confideration of Midwifes,* sehemu zote Wakunga watakuwa wanaingia darasani kwa Ukunga tu na hawachanganyi na *Nursing.* Hiyo itakuwa ni miaka mitatu, huyo hata ukimpeleka kijijini aliko mama mjamzito ambaye pengine hana a*wareness* kubwa kwa kuwa tumempeleka Mkunga ambaye ni competent atafanya kazi vizuri, lakini pale tu atakapokuwa amepewa madawa na vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza inaweza ikaonekana ni Wizara ya Afya, lakini tunazungumzia kuhusu elimu, elimu ya juu miaka iwe ni

mitatu na siyo mmoja uliochanganywa na masomo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa machache juu ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwanza nitumie nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa Wizara ya Elimu, Mawaziri pamoja na watendaji wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika changamoto kubwa ambayo ina wa-*face* kulingana na bajeti yao kuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara ya Fedha inapotoa fedha za mikopo kwa wanafunzi wetu siku nyingine isizichanganye kwenye Wizara ya Elimu, zipelekwe moja kwa moja kwa sababu ni mikopo. Tunaona kuwa bajeti ya Wizara ya Elimu imekuwa kubwa, lakini takribani bilioni 326 ni kwa ajili ya mikopo hilo lilikuwa ni ombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni malipo kwa Walimu, hata kama hawapo kwenye mazingira magumu Kigoma haimaanishi kuwa ni mazingira magumu na mimi sitaki kuwaaminisha Walimu wangu wa Mkoa wa Kigoma kuwa sisi tupo kwenye maeneo hatarishi. Kigoma ni sehemu safi, tunaishi vizuri na Obama naishi kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukisema ni kwamba, Walimu wetu kule wanapata matatizo

mawili, kwanza vifaa vya ujenzi wanapotaka kujenga nyumba zao bei ni kubwa kwa sababu ya usafiri. Sasa kile kidogo ambacho Wizara ya Elimu mnawapa kinakuwa kinamezwa ukilinganisha na wale wa mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mikopo maalum kwa watu wanaoishi mbali na sehemu zenye viwanda vya kuzalishia, sijui hiyo mtaifanyaje, lakini sitaki nioneshe kuwa ni mazingira magumu, kwa Obama hakuna mazingira magumu, wote wanaishi vizuri, tunaomba malipo yao yaboreshwe yawe makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilalamikie Wizara tulipokaa na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kawambwa akasema kuwa tarehe 30 Juni, atakuwa amekamilisha malipo yote ya Walimu, lakini naomba nitoe masikitiko yangu kuwa Mheshimiwa Waziri hakututendea haki kwenye Kamati na madai mengine walimu bado wanadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemwomba tutakapomwita atuambie kwa nini aliidanganya Kamati, kwenye hotuba yake amejaribu kuonesha kuwa Chama cha Mapinduzi kimesema katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 sekta ya elimu ilielekezwa kutekeleza yafuatayo:-

Kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi ina darasa la elimu ya awali, kujenga vyoo kwa ajili ya watoto wa elimu ya awali, nikuulize Mheshimiwa Waziri, je, ni vyoo vingapi vya watoto wadogo ambavyo vimejengwa Tanzania katika shule zetu? Ni vyoo vingapi vya watoto

ambavyo ni tofauti na vile vya wakubwa kwa sababu wale ni watoto wadogo ambayo kwenye hotuba yako unaweza kutuambia kuwa umevijenga kwa ajili ya watoto wetu. Kwa hiyo, usiandike vitu ambavyo huwezi kuvitekeleza siku nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo hivi vyuo vyetu vya *VETA,* ni hakika mwaka huu kulingana na Wizara hii imepanga kujenga vyuo vinne tu katika Tanzania. Waziri amekuwa akisimama hapo mbele akijibu kuwa tutajenga *VETA* kila Wilaya ambayo kwenye bajeti hii imeonesha kuwa bado hawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nishauri kwa nini *VETA* sasa isianzishe kama ni *mobile training* ambazo zinaweza kuwa zinafanyika katika *Headquarter* za Wilaya au Kata ili wale akinamama wanaofanya ujasiriamali wakawa wakikusanyika pale wanapewa mafunzo ya muda mfupi na huku Serikali ikitafuta hela kwa ajili ya kujenga vyuo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kwamba, Walimu hawana mtu wa kuwasimamia kama Serikali, naomba tuendelee kukubali kuwa Walimu mpaka sasa hivi hawajui washike wapi.  Kukiwa na tatizo wapige simu TAMISEMI, wampigie Mulugo, Wizara ya Elimu, wapige Utumishi au waende Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeiomba Serikali wala siyo Wizara, tunaomba Serikali Kuu itutengulie kitendawili hicho ambacho ni kikubwa na huenda Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete asikie na aweze kufanyia kazi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha umesikia? Umezidi kutufanya vijana wetu wawe na migomo, anayesababisha migomo nchi hii ni Waziri wa Fedha. Naomba uende ukijua kuwa Obama amekwambia kuwa unachangia kuleta Tanzania kwa kutopeleka pesa mashuleni mapema.

Kwa hiyo, usiwe unatupia lawama Wizara ya Elimu ijibu au TAMISEMI ijibu, wewe peleka hela mapema kama ulivyoahidi, watoto wasiwe wanapata shida, watu wanaenda *field* miezi nane hawajapata hela, ukienda kuuliza TAMISEMI wanasema Wizara ya Fedha haijatoa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa nchi hii ya Tanzania tuepushie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba usimamizi wa shule na ukaguzi upewe umuhimu. Naomba nimpongeze Mulugo amekuwa ndiyo askari wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba niwashukuru sana kwa michango yenu jioni hii na kwa mashirikiano yenu. Kabla ya kuahirisha naomba niwataje ambao kesho wataanza kuchangia.

Baada ya kipindi cha maswali na majibu tutaanza na Mheshimiwa Mabumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Mashishanga

na Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, kwa hiyo, wawepo wakati huo.

Nawashukuru na naahirisha shughuli za Bunge mpaka hapo kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 14 Agosti, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*